ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed		-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Farida Amour Mohammed - Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe	- Jimbo la Chake-Chake
62.Mhe. Panya Ali Abdalla	- Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Rashid Seif Suleiman	- Jimbo la Ziwani
64.Mhe. Raya Suleiman Hamad	- Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rufai Said Rufai	- Jimbo la Tumbe
66.Mhe. Saleh Nassor Juma	- Jimbo la Wawi
67.Mhe. Salim Abdalla Hamad	- Jimbo la Mtambwe
68.Mhe. Salma Mohammed Ali	- Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Salma Mussa Bilali	- Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salmin Awadh Salmin	- Jimbo la Magomeni
71.Mhe. Salum Amour Mtondoo	- Jimbo la Bububu
72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	- Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	- Jimbo la Mwanakwerekwe
74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	- Jimbo la Dole
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	- Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	- Jimbo la Konde
77.Mhe. Ussi Jecha Simai	- Jimbo la Chaani
78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	- Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	- Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Sita – Tarehe 24 Juni, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 64

Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo

(Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 110

Serikali kugharamia Mafunzo ya Askari na Maofisa wa Vikosi vya SMZ

Mhe. Ussi Jecha Simai – Aliuliza**:-**

Askari na Maofisa wa Vikosi vya SMZ wanapokwenda kwenye mafunzo ya Uongozi yanayotolewa katika vyuo vyao vilivyopo nchini, wanatakiwa wajihudumie wenyewe kwa kukatwa kila mwezi posho lao lote la chakula, hali inayowaathiri sana kiuchumi na kisaikolojia na hatimae huishi maisha magumu pamoja na familia zao.

(a) Kwa kuwa Wizara inalifahamu suala hili. Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba kufanya hivi ni kuwasababishia ugumu wa maisha wafanyakazi wa vikosi hivi.

(b) Kwa kuwa kwenda masomoni kwa wapiganaji wetu ni sawa na kuwaongezea umasikini na matatizo ya familia zao.

Je, Wizara haioni kwamba wakati sasa umefika wa Serikali kugharamia kwa ukamilifu mafunzo hayo badala ya kuwataka wapiganaji wetu kugharamia ama kuchangia kwa kukatwa maposho yao.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi niungane na wenzangu kukupongeza sana kwa kukalia kiti asubuhi ya leo. Nakutakia kazi njema katika shughuli zako za uenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa kwa idhini yako kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 110 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, madhumuni makubwa ya kuweka posho la chakula *(ration allowance)* ilikuwa ni kulisha maafisa na askari wote wanaokaa kambini kwani huwa wanakula chakula cha pamoja. Nakubaliana na maoni ya Mhe. Mwakilishi kuwa utaratibu wa mwanzo ulikuwa kulikata posho hili hata kwa wale wanaohudhuria mafunzo si jambo jema.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali imezingatia kasoro zilizojitokeza katika ulipaji wa posho la chakula na kuanzia mwezi Julai, 2011 basi wale askari wote watakaokwenda mafunzo hawatokatwa tena posho hili.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana pia nakupongeza kwa kukalia kiti asubuhi hii na ni kweli wanawake wakiwezeshwa wanaweza.

Mhe. Mwenyekiti pamoja na majibu mafupi ya Mhe. Waziri naomba kujua moja kati ya wizara ambazo huongoza kwa kutiliwa fedha nyingi hapa Zanzibar ni wizara yako. Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali inaonesha kwamba matumizi ya fedha za wizara yako hayaendi vizuri maana yake kunakuwa na matumizi ya fedha endelevu. Huoni kwamba sababu hii ndio inayopelekea askari wetu hawa kunyimwa posho kwamba kunakuwa na matumizi yasiyokuwa sahihi katika wizara yako.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Mhe. Mwakilishi kachanganya mambo mawili, kwanza jambo la tenda na pili suala hili la maposho. Suala la tenda kama yeye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza Fedha za Serikali nafikiri hayo mapungufu aliyoyabaini na naahidi mbele ya Baraza lako tukufu tutayafanyia kazi, hayo mapungufu tena ya kukopwa wasilipwe yasikuwepo katika makambi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kukopa serikali si jambo geni ni jambo la kawaida lakini kutokulipa ni vibaya sana. Kwa hivyo, hilo jukumu tutalisimamia ipasavyo kwamba kila panapokopwa panalipwa. Suala la msingi ilikuwa ni suala la

posho, tumekiri kwamba posho hii ilikuwa inakatwa kwa wote lakini sasa ukenda mafunzo ilikuwa inazuiliwa ndio tukaona kidogo tunawapa usumbufu wale askari. Sasa kwa nini tuwape usumbufu ile ni *privilege* wanakwenda kusoma waje watumikie vizuri vikosi. Kwa hivyo, tumeona sasa kuanzia mwaka ujao wa fedha tutatoa kwa wote.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, huko mitaani kunasemekana kwamba kuna uandikishaji wa wafanyakazi wa serikali ili kujua wale wafanyakazi hewa wasiweze kuirubuni serikali katika kulipa mishahara. Sasa huko mitaani kunasemekana kwamba kuna askari wa KMKM ambao wamepewa fomu zile lakini katika kujaza fomu hawakutakiwa kujaza mishahara yao. Je, hili ni kweli na kama ni kweli ni kwa sababu gani.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, naomba sana sisi waheshimiwa tusi-*conclude* mambo kwa usemi wa mitaani twende kwa mambo ya uhakika. Taratibu zimewekwa za kujaza hizo fomu na taratibu zinafuatwa lakini ufahamu kwamba unapo-*deal* na vikosi ujue kidogo ni sehemu ambayo lazima uingie kwa utaratibu maalum tofauti na pengine. Wale ni askari na kuna miiko ya uaskari.

Nam. 157

Watumishi wa Pemba kupokea Mishahara
PBZ Chake-Chake

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Aliuliza:
Kwa kuwa umeandaliwa utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba watumishi wote wa Serikali wanapokelea mishahara yao benki. Kwa kuwa benki ambayo tunaitarajia kubeba mzigo huo ni Benki ya Watu wa Zanzibar na kwa upande wa Pemba tawi la benki hiyo linalotegemewa ni lile liliopo Chake-Chake tu.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kwamba uwezo wa benki hiyo wa kutoa huduma kwa watumishi wote utakuwa ni mdogo na hasa kutokana na ufinyu wa tawi hilo.

(b) Kwa kuwa tawi la benki hiyo lipo Chake-Chake na watumishi wa SMZ wapo Pemba nzima. Je, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba watumishi walio mbali na Chake-Chake wanapata usumbufu wa kupata huduma hiyo.

(c) Je, Mhe. Waziri ni mikakati gani ambayo itafanywa katika kuieneza huduma hii kisiwani Pemba.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nafanya majumuisho ya hotuba yangu ya bajeti nilieleza kwamba kila penye mafanikio ya mwanamme na mwanamke yuko pembeni. Mimi nataka nikupongeze sana kwa kukalia kiti kwa kweli kimetosha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshina kubwa kabla ya kujibu swali la Mhe. Mwakilishi lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu uliobuniwa na Serikali kwa watumishi wa Umma kupokelea mishahara yao benki unalenga katika kupunguza ubadhirifu, wizi wa mishahara na watumishi kulipia mikopo yao moja kwa moja benki. Pamoja na kwamba Serikali imeamua mishahara ya watumishi wa Umma italipwa kupitia benki, Serikali haiwalazimishi watumishi wake kufungua akaunti zao katika Benki ya Watu wa Zanzibar tu. Wanaweza kufungua katika benki yoyote iliopo Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Mwenyekiti, uwezo wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuwahudumia watumishi wa Umma sio mdogo. Kinachohitajika ni kwa uongozi wa PBZ waweze kujipanga vyema katika suala zima la utoaji wa huduma hiyo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwa upande wa Pemba tawi la PBZ liko Chake-Chake na watumishi wa SMZ wako Pemba nzima. Ili kuwaondolea usumbufu watumishi wetu PBZ itafungua vituo vya huduma Mkoani na Wete ndani ya mwaka huu wa fedha. Pamoja na vituo hivyo vya huduma vitakavyofunguliwa PBZ itaongeza *ATM machines* kwa Unguja na Pemba.

(c) Mhe. Mwenyekiti, Pemba inakua sana kiuchumi, kwa maana hiyo, kuna haja kubwa ya kuwepo huduma za kibenki katika maeneo mbali mbali ya Pemba. Hivyo basi, Serikali itaendelea na mkakati wake wa kuzishawishi benki zilizopo Tanzania kufungua matawi yao Pemba na hasa katika maeneo ambayo hakuna benki. Vile vile, nichukue fursa hii kuwaomba wananchi wa Zanzibar waanzishe benki zao za jamii *(Community Bank)* ambazo zitawasaidia sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa PBZ ilikuwa na matawi katika miji ya Wete na Mkoani Pemba. Kwa kuwa matawi yale yalifungwa.

(a) Je, ni sababu gani za kimsingi ambazo zilipelekea matawi yale kufungwa.

(b) Je, vituo hivi vya huduma watakavyovifungua hivi karibuni haitakuwa katika mtiririko ule wa baadae kuvifunga na hatimaye Wapemba kupata shida.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, katika miaka ya 90 Benki ya Watu wa Zanzibar ilikuwa ina hali ngumu sana kiasi ambacho hata leseni kama benki ilikuwa inatoa miezi mitatu mitatu kitu ambacho kilikuwa ni kinyume cha taratibu za kibenki.

Hatua hiyo ilipelekea Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kui-*restructure* PBZ na kulazimika kuanza kupunguza baadhi ya huduma zake. Hivyo kupelekea kupunguzwa baadhi ya wafanyakazi na kupelekea kufungwa baadhi ya matawi yake ikiwa ni pamoja na Mkoani, Kivunge na Wete Pemba. Hii ndio iliyoinusuru benki na hadi kufikia hatua ya leo Benki yetu ya Watu wa Zanzibar inafanya shughuli zake vizuri zaidi. Vyenginevyo Benki ya Watu wa Zanzibar ingekuwa sasa hivi imeshakufa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi hatua ambazo tumezichukua katika kipindi hichi cha kuiimarisha *PBZ* ni dhahiri kwamba matawi tutakayofungua hayatafungwa tena. Kwa sababu sasa hivi inajiendesha vizuri na inajiendesha kibiashara na wala serikali haitii mkono wake wa kwenda kukopa kupitia *PBZ.*

Mhe. Abdulla Juma Abdulla: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri ametaja kwamba *PBZ* ina mpango wa kufungua vituo zaidi vya *ATM*. Kwa kuwa *ATM* ni njia moja nzuri zaidi ya kuhudumia watu kwa wepesi. Lakini kwa kuwa *network* ya *ATM* kule Pemba ni tatizo, unaweza ukenda mara tatu kila ukiomba pesa unaambiwa *network* hakuna.

Je, Mhe. Waziri ana mpango gani wa kuzungumza na hawa wahusika wa hizi *network* wakazipeleka Pemba ili wafanyakazi wa kule nao wapate hii huduma kwa wepesi zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nataka nitoe maelezo kidogo kuhusiana na *ATM*. Kwanza nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi na wananchi kwa ujumla kwamba *PBZ*

itaongeza *ATM* 10 za ziada katika mwaka huu wa fedha katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba ili kuwasaidia wananchi waweze kupata pesa bila ya usumbufu wowote.

Lakini vile vile nataka niseme tu kwamba *ATM* za *PBZ* na *ATM* za benki nyengine zozote zile zina uwezo maalum kulingana na *ATM machine* yenyewe. *ATM* ya *PBZ* ina *capacity* ya milioni 52 lakini kutokana na hali ya *insurance PBZ* yenyewe wanaweka milioni 50 ili ziweze kutumika kwa wananchi.

Tutakachokifanya ni kuhakikisha kwamba hizi *ATM* zinafanya kazi kwa muda wote ili ziweze kuwasaidia. Hapa pale ambapo pana matatizo ya mitandao basi tutahakikisha kwamba *ATM* zinapata fursa ziweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Nam. 126

Kujengwa Kituo cha Afya pamoja na kupatiwa Usafiri Chuo cha Kiislam – Micheweni

Mhe. Farida Amour Mohammed – Aliuliza:-

Kwa kuwa Chuo cha Kiislam kilichopo Micheweni - Pemba ni miongoni mwa vyuo vinavyotoa elimu bora na kutoa wanafunzi wanaofaulu vyema na hatimae kuendelea na masomo katika ngazi ya juu.

Kwa kuwa chuoni hapo hakuna Kituo cha Afya wala usafiri wa kuwahudumia walimu na wanafunzi jambo ambalo linaleta usumbufu mkubwa hususan pale wanapopata matatizo ya ugonjwa.

Je, ni lini Serikli itafikiria kununua usafiri pamoja na kujenga Kituo cha Afya katika chuo hicho.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwanza nikupongeze kwa leo kukalia kiti na hii inadhihirisha kama kweli wanawake tunaweza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 126 kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa Chuo cha Kiislam kilichopo Micheweni – Pemba ni miongoni mwa vyuo vyetu vinavyofanya vizuri na kutoa wanafunzi wanaofaulu na kuendelea na masomo katika ngazi za juu. Pia ni kweli kuwa

Chuo cha Kiislam – Micheweni hakina Kituo cha Afya ndani ya maeneo ya chuo kwa ajili ya kuwahudumia walimu na wanafunzi waliopo hapo. Vituo cha Afya vya karibu vipo Kiuyu Mbuyuni na Kiuyu Maziwa Ng'ombe.

Kuhusiana na usafiri, chuo kina usafiri wa gari ya aina ya *TATA* ambalo hutoa huduma kwa wanafunzi na walimu pindipo inapotokea dharura ya ugonjwa ambao utahitaji mgonjwa kufikishwa Hospitali ya Wilaya iliyoko Micheweni. Gari hiyo hivi sasa inafanyiwa matengenezo ya bodi lake.

Kuhusiana na kutokuwepo Kituo cha Afya katika maeneo ya chuo wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Afya kuangalia uwezekano wa kuanzisha Kituo cha Afya ndani ya chuo au kupeleka huduma ya afya kwa wanachuo kwa baadhi ya siku.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wanafunzi wanaosoma chuoni hapo ni wanafunzi wanaotoka pembe nne za kisiwa cha Pemba na wazazi wao ni watu wa kipato cha chini sana.

Je, Mhe. Waziri wizara yako ina mpango gani wa kuwatayarishia huduma muhimu zikiwemo hizo za afya wakati wanapopata matatizo kuwaondoshea usumbufu wao pamoja na walimu wao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika jibu langu mama kuwa wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Afya kuhakikisha kama tunawapatia wanafunzi na walimu waliopo pale huduma za afya.

Mhe. Mwenyekiti, kinachotakiwa pale ni kuweka kama chumba tu na kupata nesi kwa ajili ya *first aid* kwa sababu Hospitali ya Wilaya ya Micheweni haiku mbali sana. Kwa hivyo, ni tatizo dogo tu liweze kufanyiwa matibabu pale pale lakini kama ni kubwa hii gari ambayo tunaitengeneza na kuifanya sasa muundo kama wa daladala kwa sababu tunaitia bodi itaweza kuchukua wagonjwa pale kama kesi ni kubwa na kupeleka Hospitali ya Micheweni.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, mimi kama Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni ni juzi tu baada ya kuondoka kuja huku nilikwenda chuoni na kuona matatizo ya chuo ili nitakapokuja huku lile nitakalolizungumza iwe nalizungumza kama ni la ukweli.

Mhe. Mwenyekiti, katika bajeti zilizopita mimi nilipiga kelele sana kuhusu suala la Chuo cha Kiislam kilichoko Micheweni kuwa hakuna usafiri wa aina yoyote na kuna haja ya serikali kuangalia jinsi ya kuwapatia gari kwa sababu wanafunzi wanaosoma pale wanapata usumbufu usiku.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hivyo, Mhe. Waziri amesema gari liko la *TATA.* Gari lilioko limechoka kabisa na haliwezi kufanya kazi, ni gari la kupakilia kuni tu na leo wanasema kama wanalijenga bodi ili wanafunzi walitumie gari lile.

(a) Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kama sasa wakati umefika Chuo cha Kiislam Micheweni kupatiwa gari la uhakika ili wanafunzi waepukane na usumbufu walionao.

(b) Mhe. Waziri amesema kama pale panahitaji pawe na *first aid* kwa sababu hapana Kituo cha Afya na hospitali ipo karibu ya Micheweni. Je, kama hilo amelikubali atakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya kupeleka madaktari kwa sababu pana watu zaidi ya 600 wanaokaa pale ili linapotokea tatizo waweze kukabiliana nalo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli gari lililopo ni *TATA* na mimi nilikiri kwenye jibu langu la nyongeza na ni kweli bovu na kama si bovu tusingesema kama tunalifanyia marekebisho. Tunalifanyia marekebisho kwa sababu ni bovu na baada ya matengenezo hayo ninahakika gari hiyo itafaa kwa ajili ya kuchukulia wagonjwa kutoka skuli na kupelekwa vituo vya afya vilivyo karibu.

Lakini kama nilivyojibu katika jibu langu mama kuwa tutashirikiana na Wizara ya Afya kuhakikisha aidha wanatujengea kituo ndani ya skuli au kutupelekea madaktari. Kwa hivyo, nakubaliana na suala lako ambalo uliuliza na mimi tayari nilikuwa nimeshalijibu.

UTARATIBU

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni maswali ya nyongeza yanakuwa ni matatu na inaelekea hii mashine inatuziba hatuonekani huko. Hii kompyuta iliyopo hapo inaelekea inakuziba Mhe. Mwenyekiti. Sasa kama kuna utaratibu mwengine tuufanye ili uweze kutuona.

Mhe. Mwenyekiti: Katibu naomba muongozo wako.

Katibu wa BLW: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba kwa mujibu wa Kanuni hakuna kanuni iliyoweka kiwango cha maswali ya nyongeza. Ni *description* ya kiti kusema maswali ama moja, mawili au vyenginevyo.

Nam. 88

Michango Wakati wa Matibabu

Mhe. Asha Abdu Haji - Aliuliza:-

Mara baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964, Serikali iliwatangazia hadharani watu wake kwamba huduma za afya zitakuwa bure (bila ya malipo) kwa watu wote wa Zanzibar. Hali halisi ya hivi sasa ni kwamba ili upate huduma za afya ni lazima fedha zitangulie mbele.

(a) Je, Mhe Waziri kuna sheria yeyote iliyopitishwa na kubadilishwa azma ya mapinduzi ya 1964 ya matibabu kuwa bure.

(b) Kama azma ile ya mapinduzi ya kutoa matibabu bure bado ipo, ni sababu zipi zinazopelekea kudaiwa malipo kwa wagonjwa wetu ambapo wengi wao ni masikini.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 88 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe naomba kutoa maelezo machache kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba mara baada ya mapinduzi matukufu ya mwaka 1964. Serikali katika kutekeleza *manifesto* ya Chama cha *Afro Shirazi Party (ASP*) ilitangaza huduma za afya kuwa bure kwa watu wa Zanzibar.

Utekelezaji wa *manifesto* hiyo ulifanikiwa kwa kiasi kikubwa katika miaka ya mwanzo ya mapinduzi kutokana na hali nzuri ya uchumi kwa wakati huo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kumjibu swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, hakuna sheria iliyopitishwa kubadailisha azma hiyo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, mnamo miaka 1990 hali ya uchumi Zanzibar ilianza kushuka ongezeko la kasi la idadi ya watu, gharama za uendeshaji zilipanda, wahisani walisita kutupa misaada. Hali ambayo ilipelekea kusababisha uwezo wa Serikali kuhudumia sekta ya afya kupungua.

Mhe. Saheh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, angalau na mimi kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Chama cha Mapinduzi kinaamini kuwa ili tuendelee tunahitaji mambo matatu:-

watu, siasa safi na uongozi bora.

Kwa kuwa rasilimali watu ni moja kati ya nguzo muhimu ya maendeleo ya nchi, tena watu wenye afya. Je, kuendelea kuchangia huduma ya afya si kudhorotesha maendeleo kwa taifa letu na kwenda kinyume na imani ya Chama cha Mapinduzi ambapo Naibu Waziri ndio chama chake.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, swali lililoulizwa hapa ni kipi kilichofanya tulipishe watu, hilo ndio suala la msingi. Hali ya uchumi sio ya Chama cha Mapinduzi wala sio ya chama cha CUF. Kama uchumi umeshuka hata kama CUF ingekuwa ndio inatawala basi mambo yangebaki hivyo hivyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia. Naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa nini serikali isitangaze wazi wazi kuwa huduma za afya sio bure tena kama mwaka 1964 ilivyotangazwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, serikali haitotangaza kwamba huduma za afya haziko bure kama zilivyokuwa zimetangazwa kwa sababu Serikali inachofanya inasema kwamba wananchi wachangie, kama kuchangia inawashinda basi sikwambii kulipia. Serikali inawajibu wa kutoa huduma za afya kwa wananchi wake na ndicho inachokifanya. Yale mapungufu yaliopo ndio yanayojalizwa na wananchi.

Kwa mfano, kama jambo linatakiwa litolewe kwa asilimia 100 basi mwananchi anachangia kama asilimia 10, kwa hivyo asilimia 90 zilizobakia serikali inahudumia, tunachofanya ni kupunguza yale makali, lakini sio kwamba tunajivua jukumu la kuwa wananchi wajihudumie. Serikali itaendelea kuwahudumia wananchi wake na kama tutafikia hali nzuri ya uchumi basi hata huko kuchangia kutaondoshwa, lakini kwanza tupate kile cha kufanyia ile shughuli.

Nam. 99

Hifadhi ya Mali Asili

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) – Aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko kubwa la kuhamishwa mali asili nyakati za usiku husasan kuni, chokaa na mawe kwa lengo la kukwepa kukata kibali.

Je, Serikali imejipanga vipi katika kupambana na jambo hilo ili kuhifadhi maliasili hizo na wakati huo huo kujipatia mapato kutokana na mavuno ya maliasili hizo.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako, ninaomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 99 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba lipo wimbi kubwa la usafirishaji wa maliasili za kuni, chokaa, mchanga na mawe wakati wa usiku kwa lengo la kukwepa kukata kibali halali cha usafirishaji wa bidhaa hizo. Hali hii inapelekea kwa kiasi kikubwa kupotea mapato ya serikali ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Pia kutokana na ukwepaji huo pia kunachangia kuongezeka kwa uharibifu mkubwa wa mazingira kwani mara nyingi wahalifu hawa huwa wanakata kuni, majengo, kuchoma makaa, chokaa au kuchimba mchanga na mawe katika maeneo yasiyoruhusiwa. Matokeo yake ni kuongezeka kwa athari kubwa za uharibifu wa mazingira zikiwemo za kupotea kwa wanyama na miti muhimu ya asili na matunda. Kuongezeka kwa ukame na upungufu wa maji kutokana na uharibifu huo ni pamoja na kuongezeka kwa kasi ya mmong'onyoko wa ardhi hususan katika maeneo ya kilimo na fukwe.

Mhe Spika, Wizara yangu kwa kukabiliana na matatizo hayo, imelazimika kujipangia mikakati ya ziada ya kukabiliana na matatizo hayo. Miongoni mwa juhudi hizo ni pamoja na kuongeza ulinzi na doria za mara kwa mara za usiku na mchana kwa ajili ya kuwakamata na kuwachukulia hatua za kisheria wahalifu hawa.

Katika juhudi hizi mafanikio yameanza kupatikana kwani ile kazi ya usafirishaji wa maliasili hizo kinyume na taratibu imeanza kupungua, hususan baada ya wahalifu hao kukamatwa na kufikishwa katika vyombo vya Sheria. Katika kipindi cha hivi karibuni jumla ya magari 4 ya mawe, 3 ya kuni, 2

mchanga, 14 Punda na ng'ombe pamoja na misumeno 10 ya moto tayari imeshakamatwa na wahusika kuchukuliwa hatua mbali mbali za kisheria, ziliwemo za kufikishwa Mahakamani, kutozwa faini kati ya shs.300,000/= hadi 2,000,000/= kulingana na uzito wa kosa lenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, katika kukabiliana na tatizo hili, wizara yangu kwa kushirikiana na Idara ya Mazingira pamoja na washiriki wengine inaandaa kanuni ya kudhibiti msumemo wa moto na vile vile kanuni za uvunaji wa maliasili zisizorejesheka.

Wizara yangu inaamini kwamba kanuni hizi zitakapokamilika zitasaida kwa kiasi kikubwa kupunguza kasi ya ukataji miti, uchimbaji na usafirishaji wa maliasili kinyume na sheria.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, duniani kote mawe na mchango vimewekwa kwenye Idara ya Nishati na Madini, kwa maana kwamba taasisi ya jiolojia wapate kuvifanyia uhakiki na kujua adhari zake kimaumbile. Kwa Zanzibar maeneo ya michanga kwa sasa yako chini ya Idara ya Misitu na mali zisizohamishika.

Je, huoni kwamba kuyaweka maeneo ya michanga kwenye Idara ya Misitu kunaweza kusababisha migongano ya kitaalamu, kwa sababu maeneo ya michanga yanafaa kuwekwa kwenye Idara ya Nishati na Madini.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, hii ni Idara ya Maliasili zisizorejesheka sio Idara ya Misitu na michanga na mawe ni maliasili zisizorejesheka. Kwa hivyo, hapa ndipo pahala pake, taaluma uwezo wa kusimamia ili viendelee kutumika kwa uendelevu uko hapa maliasili hizo zilipowekwa.

Mhe. Raya Suleiman Hamadi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe Mwenyekiti, kwa vile uharibifu ni mkubwa sana katika vitu vyetu vya asili kuanzia mawe na miti.

Je, Mhe. Mwenyekiti, kuna watu wanaingia nyuma ya sheria katika nchi hii kukata miti yetu na watu hawa wakifika mahakamani hawana vibali wala hakuna hukumu yoyote, haoni Mhe. Waziri ni uharibifu mkubwa huu kwa miti yetu kutoweka.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Majumbe kwamba uharibifu uliopo hivi sasa ni mkubwa na una athari kubwa katika ustawi wa nchi yetu. Kama nilivyokwishakueleza katika jibu mama,

hatua mbali mbali za kukabiliana na tatizo hilo zitachukuliwa na wizara yangu, zinaendelea kuchukuliwa na wizara yangu na wizara yangu itaendelea kujipanga zaidi ili rasilimali zisizorejesheka za nchi yetu ziendelee kutumika kwa utaratibu na matumizi yake yawe endelevu.

Nam. 121

Kukomesha Ajira za Watoto

Mhe. Bikame Yussuf Hamad - Aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Micheweni ni moja kati ya Wilaya zenye tatizo kubwa la ajira za watoto kama vile kupara samaki bandarini, kubanja kokoto na kadhalika.

Na kwa kuwa Serikali ya awamu ya Sita pamoja na *NGO's* mbali mbali zilijitahidi kuwashajiihisha wananchi waachane kabisa na suala hilo ingawa bado kwa kiasi fulani linaendelea.

Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba ina mpango gani endelevu utakaoondosha kabisa ajira za watoto na kuwawezesha watoto hao kurudi skuli.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto) - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 121 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Wilaya ya Micheweni ni moja kati ya Wilaya zenye tatizo kubwa la ajira mbaya za watoto. Kama vile kupara samaki, kubanja kokoto ambako kunakosababisha kupata madhara ya kiafya na kuwakosesha watoto haki zao za msingi za kupata elimu na afya bora.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli pia Serikali ya Awamu ya sita pamoja na *NGOs* mbali mbali zinajitahidi sana kuwashajihisha wananchi, pamoja na kutoa misaada mbali mbali ya kimaisha kwa familia zenye matatizo ili waachane kabisa na suala hilo la ajira mbaya za watoto.

Juhudi zote hizo zilizofanywa na Serikali kushirikiana na washirika wa Maendeleo na *NGOs* inaonekana bado hakuna mafanikio ya kutosha yaliyopatikana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa utafiti mdogo uliofanywa na wataalamu wa Wizara yangu, unaonesha kwamba tatizo la ajira mbaya za watoto linachangiwa sana na wazazi wenyewe wa watoto ambao wengi wao hawaoni umuhimu wa mtoto kwenda skuli kusoma. Aidha, tatizo hilo linakosa msukumo na kupata mafanikio kutokana na tabia ya wazazi iliyozoweleka na kujengeka kwa muda mrefu miongoni mwa jamii hasa ya Micheweni.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuarifu Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako tukufu kuwa, Serikali ya Mapinduzi ya Awamu ya Saba yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa, chini ya usimamizi wa Wizara yangu ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwamba inayo mipango mizuri endelevu kwa lengo la kulipunguza na kulimaliza kabisa tatizo la ajira ambayo ni mbaya kwa watoto. Mipango hiyo ni pamoja na:

- Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu tayari imeshatunga Sheria inayokataza na kupiga vita ajira mbaya kwa watoto, Sheria ambayo imepitishwa na Baraza lako tukufu hivi karibuni. Sheria hiyo imefafanua vizuri kuhusu uzuiaji wa ajira hizo za watoto na namna gani sheria hizo zinawalinda watoto hao na kwa atakaye kwenda kinyume basi sheria hiyo itatoa adhabu kali kwa mujibu wa matakwa ya sheria kama inavyoeleza.

  Kwa sababu hizo Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu imejidhatiti kuwasaidia watoto hao na kuhakikisha kwamba sheria hiyo tutaitekeleza kikamilifu ili lengo lililokusudiwa ndani ya sheria liweze kupatikana.

- Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu itaendelea kuzishawishi Jumuiya za Kimataifa, *NGOs* na washirika mbali mbali wa maendeleo kuandaa miradi na *program* zitakazosaidia kuwajengea uwezo wananchi wetu wenye mazingira magumu ya kipato katika familia, ili waweze kujiendeleza na kuendesha maisha yao kwa shughuli mbadala, badala ya kuwatumia watoto kwa kuwafanyisha kazi zisizostahiki.

- Mhe. Mwenyekiti, sote lazima tukubali kwamba suala la ajira mbaya kwa watoto ni tatizo kubwa la kila taifa, na linaweza kuathiri kiwango kikubwa kwa mandeleo ya taifa. Kwa hivyo, hatuna budi sote kwa pamoja tuungane na kupiga vita ajira zote mbaya kwa watoto ili tuwe na watoto wa baadae wenye mustakabali mwema watakaoweza kuendeleza nchi yetu. Natoa wito kwa viongozi, Wajumbe wa Baraza lako tukufu na jamii kwa ujumla tushirikiane kwa pamoja katika kuondosha ajira mbaya kwa watoto, kwa kuwapa maelekezo mazuri na mawaidha mazuri kuhusu maisha yao ya baadae.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri aliyonijibu, lakini naomba nimuulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa sababu *NGOs* moja ilikuja pale ikawagawa watoto kwenye makundi mawili.

Kundi moja ambalo watoto walikuwa na umri mdogo wakarudishwa skuli, lakini kundi jengine walikuwa ni watoto ambao hawana uwezo wa kurudishwa skuli, basi walikuwa wakipatiwa kazi za amali kama vile kushona na kupelekwa viwandani kwa ajili ya kujipatia ajira za uhakika.

Je, Serikali hii ya Awamu ya Saba yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa ina mpango gani.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba serikali hii ina hisia kubwa sana kwa watoto wetu hawa. Ndio maana tukatunga sheria ambayo inawakinga na kuwalinda dhidi ya uajiri wa utotoni, ili kuwapa fursa watoto hawa waweze kwenda skuli kusoma na kuelekezwa maisha yao ya baadae.

Mhe. Mwenyekiti, tunajaribu kuzungumza na *NGOs* na mashirika mengine ni namna gani watoto hawa tunaweza kuwasaidia ili waondokane na ajira hizo ziliopo hivi sasa. Lakini juhudi kubwa tunazofanya ni kujaribu kuwashawishi watoto hawa kwa kupitia wazee wao ili waone umuhimu wa watoto hawa kwenda skuli na baadae hapo wanaweza wakaajiriwa baada ya kumaliza skuli.

Hata hivyo, kwa wale watoto ambao wameshakuwa wakubwa na hawawezi tena kwenda skuli tutajitahidi pia kwa kupitia *NGOs* na mashirika mengine ili kuweza kuwapatia ajira. Pia napenda niseme kwamba serikali imeanzisha vituo vya elimu mbadala, vituo hivi ni muhimu sana kwa watoto hawa na wengine. Kwa hivyo, ni ombi langu kwa kupitia wizarani kwetu kwamba watoto wa aina hii wajitahidi kujiunga na elimu mbadala ili waweze kupata ajira zenye manufaa kwao.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi nikiri kwamba Micheweni ni Wilaya moja ambayo kuwa ina ajira za watoto. Pia napenda nikiri kwamba Wilaya ya Micheweni ni Wilaya ambayo ni kame kimaendeleo, kiuchumi na kimazingira.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri kama atakubaliana na mimi kwamba watoto wanaojiajiri yaani ajira za watoto, huwa hawafanyi kwa hiyari yao inakuwa ni lazima, kwa sababu wanajitafutia mlo na kwa sababu ni watoto

wanaosoma skuli, wanakwenda skuli wakirudi wanalazimika kwenda kubanja kokoto au kuchimba mawe kwa ajili ya kupata sare za skuli na mambo mengine, kwa sababu wazee wao ni wanyonge na hawatimizi hizo huduma.

Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi ili kuliondoa suala hili, kama sasa Serikali ya Awamu ya Saba ijidhatiti kikamilifu, ili kuwawekea vitega uchumi vya kila aina Wilaya ya Micheweni ili kulikomesha suala hili. Kwa hivyo, atakubaliana na mimi kuwa kuna haja ya kuweka viwanda vidogo vidogo na mambo mengine ili suala hili likome mara moja.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Mwenyekiti, mimi natokea Wilaya ya Micheweni, Jimbo langu liko katika Wilaya ya Micheweni. Kwa hivyo, hali ya Micheweni naijua sana. Wizara yangu imeipa kipaumbele wilaya hii kutokana na matatizo ambayo yapo.

Mhe. Mwenyekiti, namuhakikishia Mhe. Subeit Khamis kwamba hivi sasa serikali yetu ina mipango mingi ya kuwasaidia wazee wa watoto hawa. Kwa sababu chanzo hasa ni wazee sio watoto. Kwa sababu mtoto anapotoka kwenda kutafuta samaki na kupata chakula, ina maana kwamba nyumbani hali ndio mbaya. Kwa hivyo, serikali imeyaona haya na tutajitahidi kwa pamoja ili kuwasaidia wazee kwa kutoa miradi mbali mbali ambayo hivi sasa anajua Mhe. Mwakilishi kuwa miradi hiyo imeshaanza kupelekwa katika Wilaya ya Micheweni kuwasaidia wazee na hatimaye kuwaokoa vijana wetu au watoto wetu katika majanga haya ya uajiri wa mapema.

Nam. 46

Kero Katika Sekta ya Utalii

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Aliuliza:-

Utalii ni moja kati ya sekta zinazolileta taifa letu pato kwa maendeleo ya taifa, lakini kumekuwa na kero nyingi katika sekta hiyo.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa wale vijana wanaowakera watalii maarufu (Papasi) kiasi kwamba hata baadhi ya watalii wamekuwa wakilalamika juu ya kusumbuliwa na vijana hao.

(b) Je, wananchi wa maeneo ya pwani wanafaidika vipi na utalii.

(c) Je, kuna fidia yoyote inayotolewa kwa wananchi wanaoathirika kutokana na utalii huo katika maeneo yao.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 46 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, utalii ni moja kati ya sekta zinazoliletea taifa letu pato kwa maendeleo ya taifa, lakini kumekuwa na kero nyingi katika sekta hiyo.

(a) Serikali imechukua hatua ya kuunda kikosi maalum cha ulinzi kwa watalii (*Tourism Auxiliary Police)*, ambacho hufanya doria katika maeneo mbali mbali ya utalii ili kuongeza ulinzi wa watalii na mali zao. Hata hivyo, kikosi hicho kinakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo ukosefu wa vifaa vya kufanyia kazi, mfano gari za kufanyia doria katika maeneo ya utalii, motisha ya wafanyakazi hao na kusababisha ufanisi katika kikosi hicho kuwa mdogo.

(b) Wananchi wengi wa maeneo ya pwani wanafaidika na utalii ikiwemo kupata ajira, masoko kwa bidhaa zao katika baadhi ya mahoteli na kuimarika kwa hali za maisha kwa wananchi wa maeneo ya pwani.

(c) Wananchi hupata fidia za vipando vyao katika maeneo ambayo yamewekezwa miradi ya kitalii kama utaratibu wa serikali unavyoelekeza.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na dhana ya kutokueleweka kwa utalii hasa maeneo yale ya vijijini ya pwani kabisa. Je wizara yake ina mpango gani wa kuwaelimisha au kuwashajihisha watu wa kule kijijini wakaweza kuuelewa zaidi ule utalii, ahsante.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kwa kushirikiana na Shehia husika zilizomo kwenye uwekezaji, tunaelimisha jamii pamoja na wawekezaji ili kuondosha na kuepukana na maadili ya nchi za wenzetu. Vile vile kuweza kuondokana na kufuata mila potofu zilizokuwa sio za Kizanzibari.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza kama ifuatavyo. Kwa kuwa tatizo la mapapasi kukera watalii ni la muda mrefu.

(a) Je, serikali haioni kuna haja ya kuanzisha chuo cha kutoa mafunzo kwa mapapasi ili kujua wajibu wao.

(b) Wizara haioni kuna haja ya kuwapa sare wale mapapasi waliokubalika kwa serikali.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu imejipanga kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii kuweza kuwapatia sare mapapasi hao ili kuendeleza majukumu yao.

Nam. 193

Kupanda kwa Bei Bidhaa Muhimu

Mhe. Viwe Khamis Abdalla – Aliuliza:-

Wananchi wa Zanzibar wako taaban kwa kuuziwa bidhaa kwa bei ya juu hasa mchele, sukari, unga na mafuta ya kula.

(a) Kwa sababu serikali yetu ilibinafsisha baadhi ya mashirika na mengine kuyabakisha kama *ZSTC*. Kwa nini serikali hailitumii shirika hilo kuagizia bidhaa na kuwauzia wananchi.

(b) Zanzibar inacho chombo muhimu kinachosimamia mwenendo mzima wa biashara (Baraza la Biashara). Kwa nini chombo hicho hakiingilii kati dhiki hii na kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 193 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imeingia katika Mfumo wa Biashara Huria na kuiachia Sekta Binafsi kufanya biashara, kwa lengo la kupanua huduma za kibiashara na kiuchumi kwa wananchi wake, ili kupunguza umaskini. Hivyo, kutokana na mfumo huo inaona ni sijambo lenye manufaa kujingiza katika biashara na ni vyema wananchi wakaendelea kufanya biashara hiyo na Shirika la *ZSTC* kusimamia Biashara ya Karafuu peke yake.

(b) Serikali imeunda Baraza la Biashara kwa ajili ya kuimarisha mashirika kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Baraza hilo ambalo ni jukwaa maalum la majadiliano kwa pande hizo mbili,

linalengo ya kukabiliana na changamoto za sekta kuu za uchumi. Hivyo suala la kusimamia mwenendo wa biashara linasimamiwa na serikali chini ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kupitia Kitengo cha Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji.

Katika kusimamia bei, serikali imeandaa kanuni maalum zitakazosimamia mwenendo wa bei za bidhaa hasa za chakula. Kanuni hizo zinajumuisha utaratibu wa uletaji chakula, mwenendo wa bei na gharama zinazohusiana na chakula. Utaratibu huuu Mhe. Mwenyekiti, tutautangaza kwa wananchi hivi karibuni.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwa kweli wanaokupongeza sio wanawake tu hata na sisi wanaume pia tunakupongeza. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kilichotajwa hapa ni bei nzito ya chakula na moja katika madhumuni makubwa ya kuwekwa Ghala ya Akiba, vile vile ni kukadiria zile bei za vyakula wakati zikipanda basi Ghala ya Akiba inatumika kuweka sawa ile hali.

Je, wizara yako ina mpango gani kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili iliyoletewa msaada ule, ili hiyo Ghala ya Akiba ya Chakula iweze kutufika mapema na wananchi wetu waweze kuwa na uhakika na sio tu na chakula, lakini hata na bei za chakula.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, serikali imeliona tatizo la bei, upandaji kiholela wa bei za bidhaa na hasa chakula. Kwa kulifanyiakazi tatizo hilo tayari Wizara ya Kilimo na Maliasili imeshatuwasilishia hapa Barazani Mswada wa Kuanzishwa Ghala ya Uhakika wa Chakula.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, ndani ya mswada ule tayari si Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko peke yake, lakini wizara zote zimepewa majukumu kama Mhe. Mjumbe atakumbuka wakati unawasilishwa hapa na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ikiwa miongoni mwao.

Kwa kweli jukumu kubwa la Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ni kuhakikisha kwamba chakula kinakuwa na ubora kwa kumlinda mtumiaji. *(Makofi)*

Ghala hiyo kama ilivyosema sheria ile Mhe. Mwenyekiti pia itahusiana na kuiingiza chakula katika soko endapo kutakuwa na uhaba wa chakula. Kwa hivyo, tunategemea kwamba itasaidia kwa kiasi kikubwa ku-*control* bei za vyakula.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi sana ya wananchi juu ya upandaji wa bei za vyakula hasa mchele, sukari na unga. Je, Mhe. Waziri wizara yako ina mpango gani wa kuweza kufanya utaratibu wa wizara kuagiza chakula au kuunda shirika la kuagiza chakula, ili kuweza kusaidia wananchi kukidhi mahitaji ya wananchi kwa wakati wote.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, katika jibu langu nimesema kwamba wizara inaunda kanuni ambazo zitajumuisha pamoja na uletaji wa chakula, mwenendo wa bei na gharama zinazohusiana na bei za chakula. Katika kulifanyiakazi hilo tayari wizara tumeshakaa na wafanyabiashara na wala si mara moja au mbili.

Kwa hivyo, napenda kulihakikishia Baraza lako hili tukufu kwamba kimsingi tumeshakubaliana na utaratibu tuliouweka wizara katika suala zima la uagiziaji wa vyakula pamoja na bei za vyakula. Kwa maana hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe, wawe na subiri kwa sababu suala hili halifanyiki kwa siku mbili au tatu, kwani linajumuisha uandaaji wa kanuni na hivyo tutaomba watusaidie kuelimisha wananchi, ili tuipe nafasi serikali kulifanyiakazi suala hili.

Nam. 54

Wananchi wa Kichuani na Ziwani Kufaidika na Huduma ya Umeme

Mhe. Rashid Seif Suleiman – Aliuliza:-

Kuna baadhi ya vijiji ambavyo havijabahatika kupelekewa umeme wakati wa utekelezaji wa Mradi wa *NOREMCO* na sasa wananchi wanaoishi katika vijiji hivyo, wamekaribia kukata tamaa.

(a) Je, wizara ina mpango gani wa kuwafikishia huduma ya umeme wananchi hao?

(b) Je, iwapo huduma hiyo itawafikia wananchi wa vijiji hivyo, wizara inatoa ahadi gani ya huduma hiyo kuwafikia wananchi wa Kichuani na Ziwani?

(c) Je, wizara ina mpango gani wa kutoa mikopo ya muda mrefu ya uungaji wa umeme kwa wananchi wengi, ambao vipato vyao ni vya chini na hawamudu masharti yaliyomo sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 54 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Nia ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kuwafikishia huduma ya umeme wananchi wote ambao huduma hiyo haijawafikia. Hivyo wizara yangu itasimamia na kuhakikisha kuwa vijiji vilivyosalia vinapelekewa huduma hiyo.

(b) Kwa upande wa Ziwani umeme upo sehemu nyingi hivyo namuomba Mhe. Mwakilishi kutaja kitongoji halisi ambacho hakijafaidika na huduma hiyo. Kwa upande wa Kichuani wizara yangu itahakikisha kijiji hicho kinaingizwa katika bajeti ijayo.

(c) Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme limeweka utaratibu wa kuwapatia mkopo wana vijiji wanaohitaji huduma hiyo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa nilitaja kijiji cha Kichuani katika swali langu na Mhe. Naibu Waziri alipojibu alisema bajeti ijayo.

(a) Kwanza nataka nijue ni bajeti hii tuliyonayo au bajeti ya mwakani ya 2012 na 2013?

(b) Baadhi ya vijiji vilivyoungana na Ziwani yenyewe havina umeme ndio maana nikaitaja hiyo. Kwa hivyo, kama Mhe. Naibu Waziri anataka maelezo zaidi basi niko tayari kumpatia?

(c) Suala la ukopeshwaji wa umeme kwa wananchi naona Mhe. Naibu Waziri hakuligusa na ni muda mrefu sana wananchi hawamudu gharama kuu ya kuungiwa umeme. Je, serikali ina mpango gani wa kuwakopesha wananchi kwa muda mrefu umeme, kwa sababu upo uhakika wa kupata fedha zao kwani wanaunga mita za TUKUZA?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la mkopo Shirika la umeme Zanzibar linaendelea na suala hili la mkopo kwa mwananchi yeyote ambaye anayetaka mkopo huo.

Kwa hivyo, kwa yule ambaye hajaunganishiwa umeme kwa kupitia njia hiyo, basi mimi nathubutu kusema kwamba bado hajafika kwenye Shirika letu la Umeme. Lakini kwa yule yeyote anayefika pale na kutaka umeme wa mkopo, basi tunamkopesha na tunamuunganishia bila ya tatizo lolote. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo Mhe. Mjumbe swali lake la mwanzo arudie tena.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Niliuliza hivi kwa sababu kijiji cha Kichuani kama ulivyolijibu alisema linaingizwa katika bajeti ijayo. Sasa hii ijayo sikufahamu ni ipi, hii tuliyonayo ya mwaka 2011/2012 au 2012/2013 ndilo swali ambalo nimeuliza.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kwamba bajeti ya mwaka 2011/2012 kijiji hicho kimeingizwa katika upelekwaji wa umeme. *(Makofi)*

Nam. 127

Ucheleweshwaji wa Vyeti vya Kuzaliwa na Vifo

Mhe. Farida Amour Mohammed – Aliuliza:-

Kwa kuwa kila kizazi na kifo ni lazima kisajiliwe rasmi katika Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali.

Hivyo, wananchi wa Kisiwa cha Pemba wanajitahidi kupeleka maombi ya usajili wa watoto wao mara tu wanapojifungua.

Vile vile wahusika huwasilisha vielelezo vyote vinavyotakiwa kunakohusika.

(a) Je, Mhe. Waziri, ni sababu zipi zinazopelekea wananchi kutokupatiwa vyeti vyao kwa wakati na kuwasababishia usumbufu mkubwa?

(b) Kwa kuwa tatizo hilo limekidhiri, serikali imepokea malalamiko mangapi kutoka kwa wananchi tokea mwaka 2005 hadi leo hii?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 127 kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba kila kizazi na kifo kina ulazima wa kufanyiwa usajili kupitia Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali.

Wananchi wa Pemba na hata wa Unguja wamehamasika sana katika kufanya usajili wa vizazi.

(a) Kwa kawaida Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali inafanya jitihada kubwa ya kuwapatia wananchi vyeti kwa wakati, isipokuwa baadhi ya siku hutokea uchelewaji wa kupatiwa huduma hiyo hasa kwa Wilayani kwa sababu zifuatazo:-

(i) Upungufu wa wafanyakazi wa kuchapa vyeti kwa vile

wachapaji (*typist*) wa Wilayani wanatumika kwa kazi nyingi zinazofanywa Wilayani;

(ii) Baadhi ya wakati Ofisi ya Mrajis Mkuu inachelewa

kupata vyeti vilivyoagizwa kutoka Idara ya Upigaji Chapa;

(iii) Kutokuwa na udhibiti (*control*) ya wafanyakazi walioko

Wilayani na

(iv) Kutokuwajibika ipasavyo kwa baadhi ya Masheha kwa

kucheleweshа kupeleka "*returns*" na fedha walizopewa na wananchi wa maeneo yao kwa ajili hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya matatizo hayo wizara yangu hivi karibuni ilikutana na Wakuu wa Mkoa na Wilaya wote wa Unguja na Pemba, kwa ajili ya kuelezea udhaifu huu. Kwa hivyo, hivi sasa naamini ni afadhali kidogo, ingawa bado kuna maeneo ukorofi huo unaendelea. Kwa kweli tunajua kwamba ni jukumu la wizara yetu kuhakikisha kuwa tatizo hili linaondoka lote.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo tunawaahidi wananchi kwamba katika mpango wetu wa utekelezaji wa kipindi cha mwaka huu wa

2011/2012 suala hili tumelipa kipaumbele, ili kuhakikisha kuwa vyeti vya kuzaliwa vinapatikana mara moja bila ya pingamizi yoyote.

(b) Mhe. Mwenyekiti, malalamiko inayopata serikali kwa kupitia wizara yangu yanatokana na mambo mawili.

(i) Kwanza ni mtu mmoja mmoja kufika Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali au wizarani kwa ajili ya kulalamikia hayo. Kwa hivyo, wizara inapopata malalamiko hayo, huchukua hatua za kuyarekebisha mara moja.

(ii) Wizara hupata taarifa hizo pale ambapo tunatembelea maeneo yaliomo katika jimbo fulani. Kwa maana hiyo, Mhe. Mwenyekiti si rahisi kuweka malalamiko ya aina hii katika orodho kwani hayaletwi kila siku na pale yanapoletwa juhudi ya kuyatatua huzifanya haraka iwezekanavyo.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa suala la vyeti vya kuzaliwa limekuwa tatizo sugu katika Kisiwa cha Pemba na hasa ndani ya Wilaya yangu ya Wete.

Kwa kweli watu wengi baada ya kusajili huchukuwa muda mrefu kwenda na kurudi na kutokana na mfumko wa bei za nauli, yaani mtu anaweza kuchukua muda mrefu zaidi ya miaka mitatu bado hajapata cheti chake.

Je, wizara yako imepanga mikakati gani wa muda gani wa kuwaelekeza wananchi wetu kupatiwa vyeti hivyo bila ya kusumbuka kwenda na kurudi?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba hali hii ilikuwa ni matatizo hasa katika Wilaya zetu zote na wala si ya Wete, lakini ya Wilaya ya Micheweni, Wete, Chake-Chake, Mkoani, Kusini Unguja, Kaskazini Unguja na nyenginezo.

Sasa baada ya kuona hayo tulikutana na Wakuu wa Mikoa pamoja na Wilaya kwa ajili ya kuwaelezea matatizo haya, kwa sababu kama nilivyosema kwamba matatizo yanatokana na namna mbili.

Kwanza tumezoea sisi kumpa Sheha kila kikaratasi kwenda kukuchukulia cheti na hapa si lazima umpe Sheha ni vizuri wewe mwenyewe uende, kwa sababu unapompa Sheha shilingi 2,500/= akiwakuta pono atatumia kwanza, kwa hiyo anaweza kuchelewa.

Kwa hivyo, wananchi wenyewe wanashajihishwa na wanaombwa kwamba wanapopata vile vyeti basi waende wao bila ya kumtumia mtu mwengine na hiyo itapunguza hasara hizo.

Pili baada ya kukutana na Wakuu wa Mikoa na Wilaya tumekubaliana kwamba katika wizara yangu kwamba vyeti vya kuzaliwa lazima vipatikane katika wiki mbili baada ya kupeleka kikaratasi chako ulichopewa na hiyo tayari imeshaanza kutekelezwa. Kwa hivyo, tutajitahidi kuendeleza utataribu huu, ili kuwapunguzia matatizo wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona sana hivi sasa. Kwa kweli mimi ni shahidi tosha wa kwamba vyeti vinachelewa sana, siku tatu kabla ya kuja katika kikao hiki nilikwenda kuonana na Afisa Tawala na nikamuagiza mtu kupeleka vyeti vyake. Hivi namuuliza Mhe. Waziri kwa sababu kulikuwa na vyeti ambavyo tayari vimeshaandikwa kwamba mtu akachukue na baadaye akapigwa tarehe.

(a) Je, suala hili analielewa Mhe. Waziri, kwamba bado marekebisho hayo mliyozungumza watendaji hawajafaya?

(b) Akiwa analielewa atachukua hatua gani za ziada za kuona kwamba sasa kweli vyeti wanapewa watu kwa huo utaratibu aliousema wa wiki mbili?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, suala hili wizarani tunalielewa na ndio maana tutakutana na Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa ajili ya kujadiliana matatizo haya. Kwa hivyo, inaweza ikawa mtu huyo aliyekwenda katika wilaya na kukutana Afisa Tawala ama matatizo yatakuwa kwa wale typists niliosema pengine hawakuwepo au vyeti vyao vile vishina ambavyo wamewapa Masheha havijafika.

Sasa unapopata matatizo kama hayo si wizara wala si Afisi ya Mkuu wa Wilaya ndio inayocheleweshe, lakini ni yule mtu wa katikati ndiye anayecheleweshe ambaye ni Sheha. Kutokana na hali hiyo, ndio maana nikasema na kuwaomba wananchi wakati wanapopata vile vyeti vyao, basi wasimtumie mtu wa katikati isipokuwa waende wao wenyewe.

Kwa hivyo, wanapokwenda wao wenyewe na kupeleka kikaratasi kile ambacho wanapewa hospitali au pale mzazi amejifungua nje ya hospitali, basi akifika yeye mwenyewe na baada ya kulipa shilingi 3,500/- zinazotakiwa cheti chake hakichelewi. Mhe. Mwenyekiti, utaratibu huo tayari tumeshauanza na ndipo niliposema kuwa cheti kile kwa kuchelewa kitachukua wiki mbili na hivi sasa tayari.

Lakini najua kwamba matatizo bado yapo kwa baadhi ya maeneo na hayo tutayafuatilia, ili tuhakikishe kuwa utaratibu huu ambao tumeuanzisha unaendelezwa kwa wilaya zote. *(Makofi)*

Nam. 20

Kuzuia Magari Kupita katika Daraja la Kicha

(Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)

HOJA ZA SERIKALI

(Majadiliano Yanaendelea)

TAARIFA YA MWENYEKITI

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, taarifa ndogo. Mpaka hivi sasa wachangiaji wamefikia 16 *backbenchers*. Lakini naomba tukubaliane kwamba muda ambao tutakaoutumia katika kuchangia uwe dakika tano, ili kila mmoja wetu apate nafasi. Kwa hivyo, nakuombeni Waheshimiwa Wajumbe, tuziweke *points* zetu vizuri na wala tusirudie na twende kwa wakati, ili tuhakikishe mawaziri wetu wanapata fursa ya kuchangia. *(Makofi)*

Ahsanteni Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini muda ni mdogo sana. Kwa kweli nawapongeza wote waliopongezwa kwenye kitabu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze moja kwa moja kwa kumpa pole na wala sitaki nimpongeze kwanza, isipokuwa nataka nimpe pole Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kupewa kazi ngumu tena kubwa ya kuiongoza nchi yenye utajiri mkubwa ya Zanzibar, lakini iliyojaa umasikini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini nikampa pole, kwa sababu bajeti iliyoletwa na serikali ni nzuri sana tena ya kupigiwa mfano. Lakini Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia baadhi ya mambo ambayo yanaturejesha nyuma sana.

Tukiangalia kwenye bajeti yetu ya mwaka huu Waheshimiwa Wajumbe wengi wamezungumza kwamba bajeti yetu inakuwa tegemezi kiasi hichi. Mhe. Mwenyekiti, karibu bilioni 340/- tunapata kutoka nje, yaani tunasaidiwa sisi, lakini tukiangalia hali halisi tunavyo vianzio vingi vya ndani na kama hatujavifanyiakazi basi ndio maana tukafika kwenye utegemezi kama huu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze kwenye vianzio vya mapato na sana nije kwenye Katiba. Kwa mfano, tukiangalia Katiba yetu ya Jamhuri yetu ya Muungano ni Katiba nzuri sana napingana na wenzangu wanaosema Katiba mbaya, isipokuwa Katiba ni nzuri sana, lakini tatizo letu Katiba hatuitekelezi. *(Makofi)*

Kwa kweli tukiangalia katika mambo ya Muungano kuna maeneo mengine ambayo yametajwa ambayo hayo mapato yake kama yanakusanywa, basi yanakuwa ni mapato ya Muungano. Lakini tatizo letu Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kuipuuza Katiba na kwa bahati mbaya sana siku tuliyokuja hapa ya mwanzo tuliapa kwa Katiba mbili, yaani tuliaba kwa Katiba ya Zanzibar pamoja na ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, kutokuzitii Katiba hizi basi hii misukosuko ya kiuchumi ya Zanzibar itaendelea kutukumba. Kwa hivyo, kama tunataka tuwe wakweli bajeti ya Zanzibar inaweza kujitegemea karibu kwa asilimia 70 iwapo Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano itatekelezwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu suala la mafuta. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kweli namshukuru sana kwa sababu jana ile hotuba yangu aliichambua vizuri kama nilivyokosa mimi usingizi siku tatu kwa ajili ya kuandika hotuba ile, basi na yeye nimemkosesha usingizi siku moja na amenijibu vizuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, isipokuwa kuna jambo moja alinijibu kisiasa, lakini tutakapokutana basi tutalizungumza.

Mhe. Mwenyekiti, nije kweye hoja ya mafuta kwa kweli juzi aliwavunja moyo sana Wazanzibari kwa kusema kwamba hatuna sheria ya uchimbaji wa mafuta. Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikasema hebu tuifuate Katiba, kama tutaifuata Katiba basi hapa mafuta tutachimba, kwa nini nikasema hivyo.

Kwa kweli suala la bandari ni jambo la Muungano mbona tunalo Shirika la Bandari la Zanzibar, kwa nini tumeunda shirika hilo na tumeunga kwa sheria gani. Kwa hivyo, kutokana na muda wako najitahidi kusema kwa haraka, ili kuokowa muda.

Mhe. Mwenyekiti, kama tulivyounda Shirika la Bandari Zanzibar wakati bandari ni masuala ya Muungano. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, atuletee Sheria ya Kuunda Shirika la Mafuta Zanzibar na suala hili linawezekana. Sasa huyo atakayehoji kwa nini Zanzibar tumeunda Shirika la Mafuta, kwa nini

hakuhoji tumeunda Shirika la Bandari Zanzibar, Mhe. Mwenyekiti tusidanganyane katika Katiba tunadanganyana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu walizungumza na mimi nazungumza kwamba hivi sasa wenzetu wanatunyonya na mimi sikubali kunyonywa, kwa sababu kuna watu wanaoona raha kunyonywa na mimi sikubali kunyonywa kwa haki yangu. Kwa hivyo, kama hatuwezi kuunda Shirika la Mafuta na kuambiwa hatuna sheria labda tufuate sheria ya Muungano. Hivi Shirika la Bandari la Zanzibar tuliliunda kwa sheria gani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati wakati atakapokuwa kuwasilisha bajeti yake basi atueleze lini atatuletea Sheria ya Mafuta, ili tuanze kuchimba mafuta hapa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie kidogo kama ulivyosema dakika tano, lakini ninayo mambo mengine, lakini nataka nizungumzie kuhusu suala la *TRA*. Kwa kweli hivi sasa *TRA* wanataka kuzidisha hali ngumu ya maisha kwa Watanzania na sio Zanzibar tu, yaani sote.

Wenzetu kila siku *TRA* wanaangalia Zanzibar inanufaika kwa mtaji gani, Zanzibar hatuna viwanda na viwanda vyetu wafanyabiashara. Sasa leo wafanyabiashara wanaleta magari kwa wingi. Kwa mfano, katika bajeti hii tukiangalia *TRA* tunategemea katika bajeti hii tutakusanya karibu bilioni mia moja *point* nane na serikali tunategemea kukusanya bilioni mia mbili na 21 na bilioni mia moja inatoka *TRA*. Sasa leo wafanyabiashara wa magari wameshagoma na hiyo bilioni mia moja tutaipata wapi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti lazima tuuzungumze ukweli, mimi …

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma umebakiza dakika moja.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti mimi nasikitika sana lakini nitakuja kusubiri kwenye bajeti ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo nitakua kuzungumza kwa upeo mkubwa lakini lazima tukiri, kwamba wenzetu hawatutakii mema wanataka tunyanyasike katika Zanzibar tajiri yenye uchumi wa kujitegemea ambao tunaishi katika umasikini wa kutosha.

Mhe. Mwenyekiti nitapata nafasi katika hotuba nyengine najaribu kuzungumza maoni yangu na mimi kwa sababu naitwa mkorofi, ukorofi wangu ndio huu kuwa sikubali kunyanyaswa, wala sikubali kunyonywa wanaokubali kunyonywa na wanaofurahia waache waendelee kuwa wasamaria wema lakini mimi nitaendelea kuwa mkorofi, kwa maslahi ya Wazanzibari wote.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache nitakuja kuangalia baadae ninaweza kuzuia fungu la Idara ya Uratibu ili nipate muda wa kufafanua zaidi ya hiki ninachokisema, sikusudii kumzuia rafiki yangu mpezi wangu Balozi Seif Iddi lakini nitazuia kifungu cha Idara ya Uratibu ili nipate ufafanuzi, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti unganipa dakika ishirini nisingezuia fungu, lakini kwa kuwa umenipa dakika chache nitakuja kuzuia fungu au nasikiliza kiti chao, kikiniruhusu dakika nyengine kumi na tano nimalize maneno yangu nisizuie fungu sawa.

Mhe. Mwenyekiti naomba kukaa ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma tayari tumeshaweka utaratibu na tumekubaliana kwa hivyo haiwezekani.

UTARATIBU

Mhe. Omar Ali Shehe: Kwa mujibu wa kanuni ya 57 inasema kwamba mjumbe atatakiwa kuchangia zaidi ya dakika 30 kila mjumbe anayechangia hoja atatakiwa kusema kwa muda usiozidi dakika 20 wakati wa mikutano ya kawaida na dakika 30 katika mikutano bajeti. Kwa hivyo Mheshimiwa kwa kuwa hiyo ni kanuni na kwa kuwa hakuna hoja iliyotolewa ya kuitengua kanuni hiyo na kwa kuwa tunajadili mambo mazito ya kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti naomba tuzingatie kanuni hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kama ulivyoeleza kwamba kutokana na muda inabidi tuwape Waheshimiwa wawakilishi dakika tano za kuchangia, na kwa kuwa tunahitaji wawakilishi wengi zaidi wapate nafasi hiyo. Kwa hivyo napenda nitoe hoja ili Baraza lako liridhie kwa kazi hii maalum iliyo mbele yetu basi wawakilishi waridhie kuchangia dakika tano tano kama ulivyopendekeza.

Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa kutumia ibara hiyo hiyo ya 50 ni kwamba hoja iliyopo mbele yetu ni hoja muhimu sana ni Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ambaye ndio Mkuu wa shughuli za Serikali, kuendelea kuwapa wajumbe dakika tano ni kukosa michango iliyo mahiri na makini ya kusaidia nchi.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba muda wa kuchangia hoja hii uongezwe ili wajumbe waweze kuchangia kwa mujibu wa Kanuni. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba kwa mujibu wa kanuni hizi ni kama walivyosema wajumbe, lakini Mhe. Mwenyekiti kiti chako kina uwezo pale ambapo wawakilishi ni wengi na muda ni mdogo ukawapunguza wawakilishi ili muda uliobakia wakapata wale kwa mujibu wa utaratibu uliopo kwenye katiba.

Kwa hivyo ninachopendekeza Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba kama Wawakilishi ni 30 unaweza kuwapunguza 20 ukawakata unayo mamlaka hayo wakapata kumia ambao watapata dakika 15 ambazo tumekubaliana. Mhe. Mwenyekiti ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri hili ni suala la maamuzi yetu sote kama tutakubaliana kwamba tuengeze muda inaana kwamba kuna wengine hawatopata nafasi, sasa mimi nafikiri tukubaliane wengine ambao wanahisi kwamba wao si muhimu sana kuzungumza wanavyojihisi wao wenyewe, basi walete notice ili wapungue ili wengine waweze kuzungumza dakika kumi kumi. Au laa kila mtu anataka kuzungumza basi itabakia pale pale nafikiri na mimi naweza kuchukua maamuzi yangu kwamba tutakuwa tunazungumza kwa dakika tano tano kwa maamuzi ya kiti. Sasa nataka tukubaliane hivyo ili wapate wengine nafasi ya kuzungumza.

Katibu wa BLW: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Kanuni ziko wazi kabisa kwamba muda wa kuchangia katika siku za kawaida ni dakika 20 lakini wakati wa bajeti ni dakika 30, kwa hivyo maamuzi ni ya Baraza lenyewe. Hoja iliyokuwepo kuna wachangiaji wengi hawajapata nafasi ya kuchangia kwa hivyo tufanye maamuzi kama tufuate katika Kanuni dakika 30, hivi sasa ni saa nne na nusu maana yake mpaka saa sita tutapata wachangiaji watano mpaka saa sita.

Lakini kwa vyovyote kwa mujibu wa taratibu bajeti hii leo jioni imalizike tutakapokuja jioni hakuna uchangiaji, isipokuwa ni kumpisha Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais pamoja na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa ajili ya kufunga mjadala wa bajeti hii. Kwa hivyo ni jukumu la Baraza lenyewe kuamua lipi bora kuwapa watu watano wazungumze mpaka saa sita kamili, au kugawa muda wajumbe walio wengi wapate kuzungumza kwa kila mtu kuweza kutoa mawazo yake.

Kwa hivyo ni jukumu la baraza lenyewe kwa hivyo nafikiria Mhe. Mwenyekiti, unachotakiwa ni kuwahoji Waheshimiwa wajumbe ili wakubali katika hilo ni lipi, wakiamua katika kanunia yaani thalathini maana yake ni wajumbe watano watakaopata kuchangia.

Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe naomba tukubaliane, wajumbe wamekubali dakika kumi na tano, sawa tumekubaliana na wale ambao hawatapata bahati basi watachangia kwa maandishi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria hivi ndivyo inavyotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuokoa muda nataka niende nizungumzie ni jinsi gani TRA inavyotaka kuzidisha maisha magumu kwa Watanzania, sasa hivi kuna wafanyabiashara wa Zanzibar wameleta biashara zao miongoni mwao kuna magari yamekwama Dar es Salaam na wameshagoma wanasema hawataki kulipa, na ikiwa hawataki kulipa ndio mana nikasema yale makusanyo ambayo tuliyotegemea kuyapata ya bilioni mia moja kutoka TRA kwa bajeti hii tunayokwenda nayo ambayo kuna mambo mengi, kuna miradi kuna huduma za jamii hapa wafanya biashara wakigoma ina maana haya mapato hayatopatikana. Ndio pale itakapokuja hoja ya Mhe. Makame Mshimba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi unazungumza kumbe huna kitu.

Tukishindwa kuishughulikia TRA Mhe. Waziri atakuja mwakani hapa tutamsuta kwa sababu haya yote aliyoyapanga hayatotekelezeka, sasa hivi TRA wameleta hii *document* ambayo ninayo hapa wameleta utaratibu mpya wa ulipaji wa magari, wameweka 75% ya ile bei ya upya wa gari, wakaifanya *point 5 percent* ndio ilipiwe ushuru, huko duniani zinakouzwa gari kwa huu udhuru walioupanga TRA sasa hivi *balloon* ambayo inauzwa Japan kwa $ 500 ina maana TRA wameshaiwekea thamani yake iwe $ 1,500. Kwa hivyo ndio tukasema hawa TRA wanakusudia sasa hivi kuwadidimiza Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti kwa nini nikasema hivyo mara nyingi tumepeleleza TRA wakishaona Zanzibar pamato yake yanakuwa wanaangalia yanakua katika nyanja gani wameona mapato yetu yanakua kutokana na biashara, ndio maana sasa hivi wakaamua kupandisha kodi.

Lakini tuje katika suala zima la sheria sisi tuna Mawaziri wawili wa fedha kuna Waziri wa fedha wa Jamhuri ya Muungano kuna Waziri wa fedha wa Zanzibar bajeti zao tofauti wala hazitegemeani, hivi walipokaa wakapanga huu ushuru mpya wa magari walikaa pamoja.

Sasa hii mimi nasema sio haki na wala hatuikubali, naomba suala la mapato na suala la uchumi tulitoe katika katiba sasa hivi hatuwezi tena kustahamili kwenda huko, hili nalizungumza kwa sababu gani huu utaratibu wanaofanya TRA kuwabanda wanyabiashara wa Zanzibar ndio maana katika bajeti ya mwaka huu 2009/2010 Mhe. Waziri ameeleza yaani hapa uwekezaji umeondoka kutoka bilioni 270 umeshuka mpaka ukaja bilioni 110 uwekezaji

Zanzibar umeshuka, bajeti iliyopita na kwa mkwara huu wa TRA ina maana hapa tutakuja kukosa hata hicho cha kununulia dawa angalau ya kumpatia Dk. Sira Mamboya apate angalau kutibu watu.

Mhe. Mwenyekiti ukiangalia kibapasenteji uwekezaji Zanzibar umeshuka kwa asilimia 56.2 kwa mujibu wa kitabu cha Waziri wa Fedha, Uchumi Mipango ya Maendeleo sasa hapa tunakwenda wapi, ndio maana nikasema hapa lazima tukubaliane katika masuala ya kodi sasa hivi Zanzibar wawe na uhuru wa kupanga kodi zao na waangalie ni eneo gani wataweza kupunguza ili kuweza kuimarisha uchumi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika suala zima la katiba mpya tunazungumzia sasa hivi kariba mpya sisi tusiizungumzie katika masuala ya mafuta na gesi, suala la katiba mpya litakuja baada ya uchaguzi wa mwaka 2015 kwa hivyo tutaendelea kusubiri sheria hii ya mafuta mpaka ije mwaka 2015, hichi kitu hatuwezi kusubiri.

Katika bajeti ya Makamo wa Pili wa Rais imezungumzia mambo mengi kwa sababu inazungumzia sekta mtambuu, tumezungumza suala la nishati. Mhe. Mwenyekiti, suala la nishati tukichimba mafuta Zanzibar *automatic* gesu tutaipata, ukichimba shimo la mafuta umekosa mafuta gesi itapatikana, Sasa hivi wenzetu Tanzania Bara wameshapewa maelezo waimarishe bandari ya Mtwara kwa sababu gani, kwa sababu imeonekana kwamba sasa hivi Tanzania kila wanapochimba mafuta kama hayapatikani inapatikana gesi kwa wingi kwa hivyo baada ya miaka mitano mbele Tanzaiba Bara itakuwa na sehemu kubwa ambayo inazalisha gesi kwa wingi, kwa hivyo uwezekano huo na hapa Zanzibar upo kwa nini sisi tufungwe mikono wenzetu wanakwenda mbele.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikasema kwamba kuna makubaliano hapa wamekubaliana katika mambo ya muungano ndio maana nikasema ninaweza kuja kuzuia fungu, kuna suala bado la *deference* ya ushuru bado gari na bidhaa nyengine ambazo zimeshalipiwa kodi Zanzibar linapofika Tanzania Bara bado inaendelea kutolewa ushuru mwengine. Lakini humu katika kitabu Mhe. Makamo wa Pili wa Rais anatwambia limeshaamuliwa katika vikao, suala hili ukienda katika vikao wanakubali vizuri na hivi vikao tumeshakaa vingi, mimi siku moja nimebishana na Kamishna wa TRA anamdanganya Rais wa Zanzibar katika *business council* anamwambia suala hilo Mhe. limeshakwisha, nikamwambia hilo suala Mhe. Rais sio kweli.

Kwa hivyo inaonyesha bado watendaji wako wanaendelea kukudanganya kwamba suala hili limeshapatiwa ufumbuzi na ndio maana linakuja katika vikao.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma umebakiwa na dakika mbili tu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Nakubaliana na kusema kwamba nimalizie hizo dakika mbili lakini Mhe. Mwenyekiti umenibana sana, sasa mimi kitu ambacho nataka kukimalizia tu naondoka katika hoja za uchumi nakuja katika masuala mengine.

Mhe. Mwenyekiti nimekuja na *document* zangu hizi naomba maafisa waje wawape Mawaziri kwa sababu nilisema kwamba bajeti zote ambazo zitakuwa zinadaiwa na Kiwanda cha Upigaji Chapa, mimi na wajumbe wangu wa Kamati na nitawashawishi na wajumbe wengine ili wasiunge mkono. Kwa hivyo naomba muhudumu aje ili nimpe awape Mawaziri tusije tukasokotana katika bajeti zao.

Mhe. Mwenyekiti, sioni giza labda baada ya hayo machache niunge mkono hoja na mambo mengine nitakuja kuzungumza katika bajeti nyengine. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa fursa kuchangia maneno mawili matatu katika hotuba hii ya bajeti iliyopo mbele yetu ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti na mimi kwanza kabla sijasahau naomba nichangie hapa alipoacha mwenzangu kwenye masuala ya kuimarisha Muungano, ukweli tunamuomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ayaangalie sana masuala haya ya uimarishaji wa Muungano wetu, kwa kweli kama walivyozungumza wenzangu na mimi niseme kwamba sisi hatukatai Muungano lakini tunataka muungano ulioimarika ambao una maslahi kwa pande zote mbili haonewi mtu. Lakini kwa mujibu wa Muungano wetu sasa hivi sisi Wazanzibari unatubana.

Mhe. Mwenyekiti niseme Mhe. Makamo wa Pili wa Rais anatakiwa hili suala aliangalie kwa hadhari kubwa sana kwa sababu wenzetu hawafanyi kwa bahati mbaya wanafanya kwa ajili ya kuwa sisi twende chini wao wanyanyuke. Kwa hivyo ukiangalia masuala haya ya uimarishaji wa Muungano kuna mambo ambayo kuwa sisi Wazanzibari yanatubinywa kwa hatua kubwa sana, kama TRA hayo wanayoyafanya wanayafanya kwa makusudi, kwa sababu mimi nakumbuka Zanzibar wakati huo ni njema atakae na aje, kilikuwa ni kituo cha wageni wa kila aina kwa biashara, walikuwa wanakuja Waburundi, Waganda, Wakongo, Malawi, Comoro lakini sasa hivi ukiangalia huwezi kumuona Mkomoro yeyote wala Mburundi anayekuja kuchukua biashara.

Kwa sababu wenzetu wanatuuwa kidogo kidogo bila ya sisi kujua wanapandisha ushuru, wanawatoza kodi wafanya biashara mara mbili ili

wafanya biashara wahame kidogo kidogo na wahamie kwao. Sasa Mhe. Makamo wa pili wa Rais yamazungumzwa mengi kuhusu matatizo ya Muungano lakini sitosema kama ni kero za muungano nasema ni zogo la muungano.

Kwa sababu kuna mambo mengine ukiyafanya inakuwa kama zogo, sasa kila siku sisi tutakwenda na kero za muungano mpaka lini tunatatua hili halijaondoka linakuja jengine, tutakuwa tunazungumzia kero za muungano siku zinasogea mbele haya matatizo yetu hayapati ufumbuzi wao wanakwenda mbele sisi tunarudi nyumba. Mheshimiwa wakati umefika sasa hivi masuala haya ya kero za muungano yamalizike kila siku tusiwe na kero za muungano tu zifike hatua ya kuwa sasa basi.

Mhe, Mwenyekiti suala jengine ni suala la mafuta wale wenzetu wanatufanya kama kijiji kimoja, ukiwa na kitu wanakwambia ni chetu hicho, lakini akiwa nacho yeye anasema ni chake kwa hivyo ndio wanavyotufanya, kitu tukiwanacho sisi tunaambiwa cha Muungano lakini kile cha kule kwao ni chao peke yao. Mbona kama kama walivyouliza wenzangu gesi imeshachimbwa zaidi ya miaka kumi na tano serikali itwambie tumeshapata mapato gani ya gesi, lakini tukisubiri amri ya kuchimba mafuta tupewe na wenzetu siku zitasogea mbele kama alivyosema Mhe. Hamza tusubiri katiba ipitishwe bungeni halafu tuje tuchimbe zaidi ya miaka kumi na tano mbele huku sisi tunarudi nyuma.

Kwa hivyo kama walivyosema wenzangu Wazanzibari uchumi tunao tuutumieni, tusifuge rasilimali ambazo kuwa tunaziacha mapaka lini sisi tunafuga lakini wenzetu wanaendelea, hivi tunajua mwisho wa ulimwengu ni lini tutumieni kabla ya mwisho wa ulimwengu.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine nataka kuzungumzia hali ya siasa iliyopo katika nchi yetu, kwa kweli utulivu kama alivyosema Mheshimiwa sasa hivi utulivu upo wa kutosha, sasa fursa hiyo ya utulivu wa hali ya kisiasa iliyopo basi tuutumie kwa ajili ya kuimarisha kukuza uchumi wa nchi yetu, isiwe hali ya kisiasa imetulia na ilikuwa ikiturudisha nyuma sasa tumefika muda wa kuwa tukuze hali ya nchi yetu, maslahi ya uchumi wa nchi yetu ionekane kama sasa kweli hali ya kisiasa ilikuwa ikiturudisha nyuma. Na tuseme wananchi wetu katika utulivu huu uliopo wana matumaini makubwa ya maslahi ya uchumi wetu kukua na kila mwananchi kujua kwamba kweli sasa hivi hali ya nchi yetu imekua.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haraka haraka nakuja kwenye mfuko wa maafa, kwanza naishukuru serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuona kwamba sisi Wazanzibari ni moja kati ya watu tuliomo katika dunia, kwa hivyo wakati wowote ule

tunaweza kufikwa na maafa ndio ikaona kwamba tuweke mfuko huu. Lakini naomba mfuko huu wa maafa serikali iangalie maafa mimi nasema ni pamoja na majanga au matokeo yanayotokea katika nchi yaliyokuwa hayakutarajiwa.

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais namuomba aangalie yanapotokea masuala ambayo kuwa hayakutarajiwa majanga basi ionekane kwamba huu mfuko unafanya kazi zake, kwa maana hiyo mimi nasema Micheweni kama tunavyoizungumza naomba niguse kidogo katika jimbo langu Micheweni kama tunavyoizungumza kwamba ni sehemu mojawapo ya ukame kwa sababu tunatarajia upatikanaji wa mvua ndio unaotusababisha kama Micheweni iwe ni sehemu ya ukame. Mvua tunazopata sisi ni mvua za masika tu zikipita mvua za masika basi hatutarajii kupata mvua nyengine na ndio sababu ikawa ndio sehemu ya ukame katika sehemu za mashariki kule Pemba.

Kwa hivyo katika suala hili la mfuko huu wa maafa naomba sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais aone kwamba sasa hivi Micheweni kwanza nataka kusema tayari imefikwa na maafa kwa sababu gani niseme hivyo, wananchi wa Micheweni walijitahidi kulima katika kipindi hiki cha mvua za masika wakapanda mtama mwingi lakini kwa bahati mbaya ule mtama umengiwa na wadudu wote umeharibika, kwa hivyo hawatarajii kwamba watajikimu katika kipindi hiki kinachokuja na wakati mvua zao zishapita.

Kwa hivyo naomba Mhe. Makamo wa pili wa Rais aone kama linapotokea suala kama hili basi serikali ikimbilie haraka haraka wale wananchi wake kwenda kuwaafu, kwa nini niseme hivyo ulipoanza kuharibika ule mtama kwasababu tuna viongozi wa kila wilaya kila Mkoa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Subeit Khamis Faki umebakizadakika mbili tu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ishaalla Mhe. Mwenyekiti naomba nimalizie kwa hivyo ilikuwa kuna haja ya kupatiwa wale wananchi dawa za kuhami vile vipando vyao kabla, ule mfuko wa maafa ulikuwa utoe wanunuliwe dawa ili viwahiwe vile vipando vyao na waweze kujikimu. Kwa maana hiyo hawakufanya hivyo serikali labda kama watendaji hawakusema au sijui kwa nini, kwa hivyo namuomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais awaelekeze watendaji wake katika Mawilaya, katika Majimbo ili kutoa taarifa zinapotokea za haraka haraka.

Mafano kipindi kilichopita mimi nilikuja kumueleza Mhe. Waziri Kiongozi hapa kutokana na maafa yaliyotokea kule Micheweni, nashukuru yeye mwenyewe alipanga safari tukaondoka mimi na yeye na akenda kuona hali, watendaji wake kule kabla ya kumpa ripoti huku nimempa ripoti mimi. Kwa hivyo na hili namuomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alione kama mfuko

huu uwe ni faida kwa wananchi wetu wote walio katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba linapotokea tatizo mfuko huu haraka uwahami wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti kwa kuheshimu muda wako naomba sana niunge mkono hoja hii mia juu ya mia. *(Makofi)*

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambae amenijaalia kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu nikiwa mzima na afya njema, lakini pia nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kukupongeza wewe mwenyewe Mhe. Mwenyekiti, kwa namna ulivyokikalia kiti hiki, niungane na wenzangu kwa kusema kwamba wanawake tukiwezeshwa tunaweza.

Pia nichuku nafasi hii nimpongeze Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa hotuba yake ambayo kama itatekelezeka basi itawaletea maendeleo makubwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo basi nakuomba haya maelezo yangu ya shukurani yasiingie katika dakika zangu niende moja kwa moja katika kitabu hiki, niingie katika ukurasa wa 49 mfuko wa kukabiliana na maafa. Ukweli kabisa nichukue nafasi hii kuipongeza serikali kwa kuona upo umuhimu mkubwa wa kuelimisha idara hii, lakini pia niipongeze idara hii kwa namna ambavyo imetoa mafunzo kwa shehia mbali mbali kwa Unguja na Pemba jinsi ya kukabiliana na maafa, niipongeze kwa dhati kabisana nawaomba waendelee na moyo huu huo wa kuhakikisha kwamba tunatoa elimu kwa wananchi wetu katika kukabiliana na maafa.

Mhe. Mwenyekiti mimi nina wasi wasi kwamba katika Idara hii ya kukabiliana na maafa bado hatuna vifaa vya kisasa vya kukabiliana na maafa, pamoja na kuwa hotuba yako Mhe. Makamo wa Pili wa Rais umeeleza kwamba utashirikiana na taasisi mbali mbali kuhakikisha kwamba maafa haya yanatatuliwa. Nitoe mfano mwaka 2009 ilipozama meli ya MV. Fatihi kwa kweli serikali yetu ilitaharuki lakini sio hilo tu ikabidi tuagizie vifaa vya uokozi kwa wenzetu wa Tanzania Bara, kama nina kumbu kumbu vizuri ilituchukua siku tatu kuokoa wananchi wetu lakini pia kuokoa mali zao.

Mhe. Mwenyekiti ni kweli kabisa idara hii haina vifaa vya kuhakikisha kwamba tunakabiliana na maafa, lakini pia taasisi ambazo tunazitegemea hata kuzamia hawawezi. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri tujitahidi kuhakikisha kwamba tunawapa mafunzo zile taasisi ambazo tunaziona zitaweza kutusaidia katika kukabiliana na maafa.

Mhe. Mwenyekiti, kama tungekuwa tuna vifaa vya kutosha, vyombo vya kuinulia ile meli ilipozama kutoka chini kwenda juu, isingeweza kutuchukua siku tatu. Kutokana na upungufu, kutokana na serikali haijajiandaa kukabiliana na yale maafa ndio maana imetuchukua zaidi ya siku tatu.

Naomba niiombe serikali katika kukabiliana na maafa tuhakikishe tuna vyombo vya kisasa, tunatoa elimu kwa wananchi pamoja na kutegemea serikali lakini na mwananchi mwenyewe aweze kujisaidia kama atatokezewa na tatizo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea niingie kwenye ukurasa wa 66. Nije kwenye Baraza letu la Wawakilishi. Kiukweli kabisa kwa dhati yangu nichukue nafasi hii kuipongeza serikali, kwa namna ilivyojitahidi kujenga Baraza letu hili jipya la Wawakilishi. Baraza hili lina hadhi ya chombo chenyewe cha Sheria. Pamoja na pongezi hiyo kuna kasoro ndogo ndogo ambazo kama zitashuhulikiwa jengo hili litaendelea kuwa na hadhi ya chombo hichi.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni kuna matatizo ambayo yamejitokeza katika jengo hili. Kwa mfano vyoo. Vyoo vyetu inaonekana wale wajenzi walipojenga hawajatuwekea vyoo vya kisasa vyenye umadhubuti. Kama utakwenda katika kile choo lengo la choo kile kile kilichokuwemo ndani kiweze kutoweka. Lakini kama utakwenda utavuta bomba kama piya maji yanazunguka pale pale na kile ambacho kilichokusudiwa kiingie ndani ya choo hakiendi. Hii inatokana na kwamba vyoo vyetu havifai.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia serikali yetu nimuombe basi Mhe. Makamo wa Pili wa Rais suala hili tulishughulikie mara moja ili tuweze kulitatua tatizo hili. Waswahili wanasema usipoziba ufa utajenga ukuta. Si hilo tu, kama hatutolishughulikia mara moja basi itatupelekea serikali yetu kupata hasara zaidi.

Nikiendelea katika Baraza la Wawakilishi nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kuipongeza serikali kwa kujenga nyumba ya kisasa na ya kileo ya Mhe. Spika. Baraza letu lililopita mlitupeleka ofisi yetu tukakague yale maendeleo ya jengo lile na tulikagua.

Lakini sasa hivi tunapita nje tu tunaona jengo linang'ara lakini ndani hatulioni. Kupitia wizara hii naomba ofisi zetu za Baraza la Wawakilishi liandae utaratibu ili Waheshimiwa Wajumbe waende kuangalia jengo namna lilivyomalizika. Kwa kweli jengo linapendeza na linavutia. Niiombe serikali jengo zuri lakini ipo hija ya kuingiziwa fenicha Mhe. Spika, ili akiingia pale aingie na nguzo zake tu.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze serikali kwa kuwapatia mafunzo wafanyakazi wetu wa Baraza la Wawakilishi, kuanzia ngazi ya cheti, ngazi ya diploma mpaka shahada ya juu, inatia moyo sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa bado dakika 3, malizia.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 27 suala la madawa ya kulevya. Mhe. Waziri wa Fedha alipokuwa anazungumza bajeti yetu kuu ya taifa mimi nilitegemea kwamba suala hili atatupa mikakati yake kama serikali kuu ili kuhakikisha vijana wetu hawa tunasaidia kuondokana na madawa ya kulevya, pia tunakikisha tunazuia madawa ya kulevya. Maana usipomjua mgonjwa maradhi yake huwezi kumtibu, lakini hatukumsikia.

Mhe. Mwenyekiti, nasema bado serikali haijawa-*serous* katika kulishughulikia suala hili la madawa ya kulevya. Mhe. Waziri wa Fedha alitwambia Mikakati yake kwamba vijana atahakikisha kwamba wanajikwamua na umasikini. Lakini vijana hao hao ambao tunawategemea kwa taifa letu, kama hatujahakikisha kwamba wanaondokana na madawa ya kulevya pesa hizo watazitumiaje.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kama tutaondoka hapa tukianza ziara kuanzia Malindi, tukija Mlandege, Miembeni, Mikunguni, machozi yanaweza kukutoka, inasikitisha. Kila kijana unamkuta sasa hivi anasinzia. Kuna bibi mmoja sikuhiyo alikuwa anasema kwamba *alhamdulillahi* sasa hivi mwanangu hatoki anasinzia tu ukumbini. Haya mambo hayafurahishi yanasikitisha na hili suala sio la mtu mmoja ni suala letu sote. Ni suala la kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, nchi yoyote inategemea vijana, taifa lolote linategemea vijana. Bila ya vijana madhubuti nchi yetu itayumba. Vijana wamepotea, vijana wanakula kama mas-hara, kutwa wanakula mikate ya boflo tu na juice. Kweli hiyo ni halali, serikali tupo, hatuwezi kuzuia kwa ukweli kabisa. Bado hatujawa *serious* katika kuhakikisha kwamba tunazuia uagiziaji wa madawa ya kulevya. Tunawalaumu vijana, tumesema tutawajengea, tutawafungia lakini ikiwa bado unga unaingia nchini kwetu haitasaidia kitu.

Naomba kupitia kwa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, tuhakikishe awamu hii tunaonesha angalau kupungua suala hili la madawa ya kulevya. Kila siku linaingia tena kwa kasi mno.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa dakika zako za kutoa mchango zimemalizika naomba tuheshimu muda.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa vile nakuheshimu sana, naheshimu muda wako, hasa kwa vile mwanamke mwenzangu naomba kusema kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia juu ya mia.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, lazima nikiri kidogo kwamba leo nimevurugika. Kadiri wenzangu wakichangia suala la Muungano nakuwa sipo katika hali nzuri. Kwa hivyo niweze kuchangia muda mfupi sana.

Mhe. Hamza leo amenimaliza ilikuwa na dakika zangu 15 apewe yeye. Mimi nataka niseme tu kwamba Mhe. Balozi kwangu mimi na kwa Wazanzibari ni mtu muhimu sana. kwa sababu sio tu kwa uzee lakini kwa umaarufu wa uongozi Tanzania na nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasikitika sana kuona hadi leo hii watendaji wanaendelea kuwadanganya mawaziri wetu. Nasema hivi kwa sababu kama leo hii tutamwambia watupatie makubaliano ya hizi kero za muungano nina hakika hakuna makubaliano.

Kwa msingi huo inaonesha watu wanaandika haya mambo kwa sababu ya kudanganya Baraza. Bila shaka itakuwa kuna maslahi yao. Haiwezekani zaidi ya miaka 20 watu wazungumzie jambo moja, wanaambiwa na Waswahili wenzao, nchi moja, taifa moja sera moja haiwezekani. Kwa vyovyote itakuwa kuna watu wanamaslahi yao. Na hili mimi binafsi sitakuwa radhi kulikubali.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Balozi amezungumza humu kati ya kero za muungano zilizokuwa hazijapatiwa ufumbuzi ni

- Tume ya Binadamu,
- TRA
- Mgawanyo wa mapato ya GBS.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Sheria na Haki za Binaadamu naomba nikubali limekubalika na tume inafanya kazi. Lakini hakuna ukweli kwenye suala zima la mapato ya TRA. Na hakuna ukweli kwenye mgawanyo wa mapato ya GBS. Hata Mhe. Waziri wa Fedha juzi amethibitisha kwamba zaidi ya bilioni 116 haziingii kwenye mfuko Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Mimi kwa mtazamo wangu madhani tukubaliane kwamba tatizo sio Tanganyika tatizo ni sisi wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, pale ninavyoangalia na kuona kwamba wapi tunakwama, mimi naona sisi Wazanzibari ndio tatizo. Kwa sababu inawezekana kwamba

kuna watu wanapendelea mgongano huu kwa maslahi yao binafsi. Nataka nisome katiba ya Zanzibar kifungu cha 23 (1).

Kifungu cha 23 (1) "Kila mtu ana wajibu wa kufuata na kutii Katiba hii na sheria za Zanzibar kuchukua hatua kisheria kama inavyowekwa, kuhakikisha hifadhi ya Katiba na sheria za nchi zinalindwa.

(2) Kila mtu ana wajibu wa kulinda maslahi ya Zanzibar mali ya nchi na mali inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi na pia kuiheshimu mali ya mtu mwengine.

(3) Watu wote watatakiwa na sheria kulinda vizuri mali ya Zanzibar na kwa pamoja kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhilifu na kuendesha uchumi wa Zanzibar kwa makini kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadaye ya taifa lao."

Kwa mnasaba wa Katiba hii na kwa sababu kila siku tunasikia kuna kero hazifikii kikomo ni dhahiri kwamba serikali imeshindwa. Kwa sababu hatuoni msingi, ikiwa katiba inaeleza hivyo kwa nini hatufikii maamuzi. Zanzibar kama Tanzania Bara itaendelea kuvunja muungano na kwa hivyo suala la TRA, GBS na mapato ya mafuta ni matakwa yetu wenyewe Wazanzibari, tukiamua leo inawezekana wala si kesho.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafanya utafiti kujua kwa nini hadi hii leo hatujafika maamuzi ya masuala ya mafuta. Ishallah tukika uhai siku ya Wizara ya Maji nitasema hadharani. Si Tanzania Bara ni sisi wenyewe. Mwaka jana tulikubaliana kwamba Wazanzibari 10 waende wakasome nje fani ya mafuta. Kwa taarifa yako hadi hii leo hakuna hata mmoja. Nimefatilia wapo Wazanzibari wanne, watatu wanasoma afya, mmoja. anasoma *solar energy*. Sivyo tulivyokubaliana. Ni sisi wenyewe hatujakuwa tayari kwa kumuonea haya mke ndugu.

Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari wametuchagua, tumeapa kwa kutumia msahafu, Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Muungano, tunawasaliti. Imani yangu Mhe. Balozi atusaidie. Mimi sipo tayari kuidhinisha fedha ya uratibu kwa ajili ya watu kwenda kuzungumza tu na kunywa soda. Sipo tayari, kwa sababu hakuna faida yoyote inayopatikana, watu wanaoneana haya.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba suala la muungano si tatizo, tatizo ni sisi wenyewe. Kuna watu unawasaidia mgogoro wa muungano. Mimi nasema mafuta, TRA tukiamua leo kesho Jumamosi haifiki na Wazanzibari ndio wenye

kupanga uchumi wao. Basi tuamue kuanzia leo TRA iondoke, mapato yote yakusanywe na ZRB chini ya usimamizi wa Wazanzibari wenyewe. Hatuwezi kuchukua mtu akatuadhibu halafu tukaambiwa sisi ndio maslahi yetu. Ikiwa maamuzi ni kwamba tunakiri sisi ndio tutakaodhalilika basi TRA kwa umoja wetu tuamueni kuondoka Zanzibar, tuwaachie ZRB wakusanye mapato yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze *point* nyengine ambayo Mhe. Balozi amesema hapa kwamba moja kati ya changamoto ambayo inatukabili nidhamu na maadili ya Uongozi katika serikali. Mimi nakubaliana na wewe moja kwa moja Mhe. Balozi kwamba nidhamu na maadili ya Uongozi yanatushinda. Kwenye hotuba hii ya Mhe. Rais aliyozindua Baraza hili alisema kwamba kila kiongozi aliyechaguliwa na aliyeteuliwa lazima azingatie maadili na nidhamu ya uongozi.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba nilipongeze Baraza la Manispaa ya Zanzibar kwa kuipiku Baraza la Wawakilishi. Kazi hii yakuundwa Tume ilikuwa ni kazi yetu lakini tulishindwa. Nashukuru sana kwamba wenzetu madiwani walimudu kuunda tume na kuweza kugundua uovu unaofanywa Baraza la Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni gazeti la Zanzibar leo, gazeti la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, limesema kwamba Kamati maalum yaibua madudu lukuki. Inapendekeza Serikali imng'oe Mkurugenzi. Mikataba ya matatizo mabovu yaanikwa, huu ni ukweli.

Mhe. Mwenyekiti, juzi tulikuwa na semina *Ocean View* nikabahatika gari yangu ilikuwa ipo kule chini. Nikakutana na Wakurugenzi wawili wanaambiana, mmoja anamwambia mwenziwe. Eti Madiwani wanataka kukitumia wakuone, hawajui kama wewe ni mtaalamu, alah! Mtaalamu kuliko ibilisi. Suala la utaalamu na uwajibikaji ni tofauti, kwa hivyo uwe mtaalamu kuliko bilisi lakini ni lazima ufuate sheria na kanuni za nchi hii. Ikiwa kuna wizi ni lazima utafutwe.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwamba serikali ndiyo inayokaribisha waharibifu hawa wa mali ya serikali. Kwa nini tukizungumza hapa tuunde tume, Mawaziri wote wanabadilika rangi, kama jambo kubwa, kama tusi. Mimi nasikitika sana.

Juzi ilivyotokezea sunami Japani Waziri Mkuu amechelewa tu, kujenga miundo mbinu akaambiwa ajiuzulu, amechelewa sio kwamba hakuna fedha. Kwaambiwa Ijumaa, kafa Jumamosi, kaambiwa ajiuzulu. Hapa mtu anaiba anaachiwa, *Inalillahi waina illahim Rajy-un.* Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi na mimi niseme chochote kuhusiana na hotuba ya Bajeti iliyokuwepo mbele yetu. Kwa kuwa ni mjumbe wa Kamati nitazungumza mambo mawili madogo sana ili niwape wenzangu na wao wachangie kwa sababu sisi tumechangia vizuri katika Kamati yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa hotuba nzuri ya bajeti katika wizara yake. Pili nianze moja kwa moja kuchangia hotuba hii kwa kuangalia Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Idara hii ni idara moja muhimu sana katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. Bado ina matatizo mengi sana ambayo yanasababishwa na vitu mbali mbali kama uchakavu wa vifaa vya kutendea kazi na mambo mengine.

Lakini la kusikitisha zaidi katika idara hii kuna idara nyingi sana za serikali ambazo zinadaiwa na idara hii sijui kwa muda wa miaka mingapi, lakini pia ikiwemo Afisi ya Makapo wa Pili wa Rais, inadaiwa na Idara hiyo ya Upigaji Chapa.

Katika malengo yake idara hii imepanga malengo mengi sana yakiwemo kuanzisha Bohari Kuu ya vifaa. Nataka serikali kupitia idara zake ikanunue vifaa hivyo katika Bohari hiyo.

Jengine ni kuhama kutoka eneo lao la sasa na kwenda katika eneo jipya la kiwanda cha Sigara. Lakini kutokana na haya madeni yaliyokuwepo katika Idara mbali mbali za serikali hatuoni kwamba hapa tunazidi kuwarejesha nyuma watu wetu hawa ambao ni muhimu sana katika serikali yetu hii.

Mimi nasisitiza tena kwamba idara zote au wizara zote ambazo zinadaiwa na afisi hii au Idara hii ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, vifungu vyao vya bajeti hapa hatutovipitisha mpaka watwambie lini watawalipa hawa watu wetu ili waweze kujiendeleza na shughuli zao kama walivyopangiwa.

Mhe. Mwenyekiti, idara hii imepangiwa kukusanya pesa nyingi sana, lakini pesa zenyewe kumbe taasisi za serikali zinapokwenda kule wanakopa, hakuna kurejesha pesa hizo. Kwa hivyo msisitizo wangu kwamba idara zote ambazo zinadaiwa zirejeshe fedha hizo haraka sana, ama vifungu vya bajeti zao hatutovipitisha.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili ni suala la mwisho ni suala la uchimbaji wa mafuta. Mgogoro kila siku Zanzibar tunagombana kuhusiana na mafuta, mafuta yenyewe yako ardhini wala hatujui kama hapo au hayapo. Serikali kuna ugumu gani kuamua kuchimbwa haya mafuta yakaonekana kama yapo, pengine

hata kama yapo mafuta hayo hayatoshi hata kujipaka watu wawili. Lakini sisi huku tunagombana tunataka kuuwana, migogoro ya kila siku, ina maana gani.

Mimi nahisi kwa mawazo yangu mafuta haya kama yapo kwanza yachimbwe halafu baadae mpango wa kutaka kuyatoa mafuta sijui katika mambo ya muungano yatafuata baadaye. Tukisubiri sisi kwamba tutoe suala hili katika suala la muungano, tusubiri Katiba mpya miaka mitano nadhani ijayo huko. Sisi tunasubiri tuunde sheria. Tuangalie kwanza, yachimbwe mafuta yaangaliwe kama yapo. Badala yake huo mlolongo wa kutaka kuyatoa utafuata baadaye lakini tutakuwa tumeshapata uhakika. Lakini tukisuribi miaka mitano halafu tukae miaka mengine tena mafuta yachimbwe pengine kwa muda wa miaka 15 sisi tuna tamaa ya mafuta tu.

Mhe. Mwenyekiti baada ya hayo mimi naomba nimalizie hapo. Ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nikachangia mawili matatu katika bajeti hii ya Mhe. Makamo wa pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kukupongeza wewe na kukutakia Ijumaa Karim mbele ya kiti chako hichi. Lakini nichukue fursa kwa Mhe. Makamo wa pili wa Rais kwa hotuba ya bajeti yake aliyotuletea mbele ya Baraza hili, nasema namshukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, niingie kwenye mada ya ukurasa wa 23 katika sehemu ya maji safi na salama. Katika kikao kilichopita tuliletewa Mwaswada unaohusiana na Wizara ya Biashara na Masoko kwa upatikanaji wa kupata kutumia wananchi wa Zanzibar viwango vilivyobora kwa kuepusha matatizo kadhaa ya maradhi.

Sisi katika kijiji chetu cha Tumbe tuna kisima kikubwa ambacho kuwa kina maji mengi, lakini nataka nimthibitishie Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kuwa kisima chetu bado tuna tatizo ya kupata maji yalikuwa bora na salama. Kutokana na sababu hizo maji yetu tunayotumia kwa kunywa ni maji ya mashimo. Maji yetu ya kisimo kilichokuwepo Tumbe kwanza yana harufu mbaya halafu baadhi ya vyakula unavyopitia huwa zinaleta rangi mbaya. Tunaomba Mhe. Makamo wa Pili wa Raisi ulione tatizo letu hili tufanyiwe uchunguzi kile kisima yale maji ni safi na salama?

Halafu katika ukurasa wa 28 kuna changamoto ya tatizo kubwa katika uwajibikaji ndani ya taasisi zetu za serikali. Mheshimiwa mimi hili nitoke katika maofisi mengine, kero langu hasa katika Mahospitali ambalo kuwa juzi

Mhe. Waziri wa Fedha anauliza anakwenda pale anakwenda kwa ajili ya matatizo. Ikiwa hana matatizo pale haendi. Lakini la kunisikitisha katika kituo chetu cha Wila ya Micheweni unaweza kutoka na mgonjwa Makangale na hali yake mbaya, ukenda nae pale katika kituo kile ambacho kuwa tunaambiwa ni kituo cha Wilaya hukuti daktari.

Mhe. Spika, nataka nimwambie Mhe. Makamo wa Raisi wa Pili ni kuwa tunayoyasema kwamba tunayaona, si mambo ya utashi au kusikia. Ni juzi tu alipelekwa mgonjwa hali yake taabani, basi watu walikwenda mpaka kituo cha polisi akajakatafuta daktari ndio akapata huduma. Mimi nasema hilo ni kero sana hasa katika kitengo hichi cha afya.

Halafu la tatu niende katika hili suala la Ukimwi. Mimi niliposikia katika Wilaya ya Micheweni kuwa ni Wilaya ambayo inaongoza katika asilimia hizi zilizotajwa hapa katiak suala la Ukimwi, Wallahi nilishtukwa na roho kidogo. Kwa sababu ukiitizama Wilaya yetu ya Micheweni ni Wilaya ambayo kuwa tunaambiwa inaongoza kwa umasikini, inaongoza kwa ukame halafu na letu tunasikia kuwa inaongozwa kwa suala zima la Ukimwi. Tunaomba serikali itufanyie linalowezekana kidogo ili angalau mengine tupunguzike.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni sehemu ya utalii, bado tunachukuliwa wanetu wanapelekwa katika Mahoteli ya Kitalii. Kwa hiyo tunakiomba kitengo kile cha utalii watakaoingia pale kama ni wari hawajaolewa basi wafukuzwe.

Halafu jengine ambalo kuwa naiyomba serikali itusaidie ni katika hichi kitabu chako hapa, hawa akina mama wanaotengeneza sabuni kwa kutumia mwani. Nakuomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais utusaidie hili katika Wilaya yetu ya Micheweni. Katika Wilaya ya Micheweni wakulima wa mwani ni wengi na kazi kubwa wanayoipata ya ukulima ule wa mwani na pia hawana soko na hizo soko walizonazo hauna bei, wanahangaika. Kwa hivyo tunaomba kupitia kikundi hichi cha utengenezaji wa mwani serikali itusaidie angalau mradi na sisi upelekwe kule ili wananchi wetu badala ya kuuza na mwengine wakipata katika matumizi mengine utatusaidia.

Kwa hayo machache Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja, Mimi kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Micheweni mia juu ya mia. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii adhimu na mimi nikatoa mchangio wangu kidogo kuhusu hotuba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha mchana huu kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango utaingia sana katika kifungu cha 42 ukurasa wa 22 kinachozungumzia kuimarisha huduma za afya kwa jamii. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makamo hapa ametaja Hospitali kuu ya Mnazi Mmoja na hospitali za Kivunge, Micheweni, Vitongoji, Wete pamoja na Mkoani.

Mhe. Mwenyekiti, ni faraja kubwa kwa Wazanzibari kwani muda mrefu wananchi wetu wanapata tabu ya kuhamia Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili. Kwa hivyo, serikali imefanya jambo la msingi na la maana kuanzisha Hospitali ya Rufaa hapa Zanzibar. Lakini kinachonishangaza mimi sana na kuniumiza kichwa ni hali halisi ya Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, hospitali hii imeanzishwa tokea mwaka 1920 ni karibu miaka mia tena na walioanzisha jengo hili hasa vile vyumba vya wodini vilikuwa vina uwezo wa kulaza wagonjwa watano. Na kila mgonjwa alikuwa anaangaliwa bila ya matatizo yoyote. Kwa hivyo, watu 25 walikuwa wanaingia katika chumba kimoja kumuangalia mgonjwa wao, lakini sasa hivi hospitali hiyo kila chumba kinalazwa watu 15.

Mhe. Mwenyekiti, hebu chukulia hao wagonjwa 15 na kila mgonjwa mmoja anaangaliwa na watu 15 hivyo inakuwa ni watu 75 wanaoingia chumba kimoja kumuangalia mgonjwa. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hospitali hii uwezo wake ni mdogo sana, na kutokana na hali halisi ya majengo yenyewe yamekuwa ni ya muda mrefu na yanaweza kuja kuhatarisha maisha wagonjwa na wale watu wanaokwenda kutazama wagonjwa.

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mnazi Mmoja pale utafikiri pana matanga jinsi palivyokuwa na watu wengi. Kwa hivyo, ningeliishauri sana serikali kutokana na suala hili ili waweze kuliangalia kwa kina na kuangalia eneo mahsusi ambalo litakuwa ni la kisasa ili kujenga hospitali ya rufaa itakayoleta tija kwa wananchi wetu na wagonjwa wanaokwenda katika hospitali hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nichangie kuhusu suala zima la changamoto za taifa katika kifungu cha 51 ukurasa wa 29 kuhusu kupambana na rushwa. Mhe. Mwenyekiti, serikali ina jukumu kubwa sana kwani rushwa hapa Zanzibar imekuwa kama maji ya kunywa tu. Kwa kweli miaka mingi Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar tokea kuanzishwa hakuna kufuatiliwa suala zima la rushwa. Mhe. Mwenyekiti, rushwa imeenea katika sekta zote, ukija kwenye mawizara, maidara, taasisi mbali mbali, vikosi vya ulinzi.

Mhe. Mwenyekiti, juzi katika safari yangu moja nilikuwa nipo maeneo ya Mnazi Mmoja kama saa 11 za jioni basi niliwakuta hawa askari wa usalama barabarani karibuni watu 9, lakini mkubwa ndiye mtu wa mwanzo aliyeanza kuvua kofia yake. Mhe. Mwenyekiti, waliofuatia kila mmoja alikuwa anavua

kofia lakini ndani ya ile kofia anaingiza anatoa pesa zinakusanywa kwa yule mkubwa. Kwa hivyo, walipomaliza askari hao nafikiri pesa zile hazifiki katika kitengo hiki cha Usalama Barabarani zinamalizia kwao wao wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nahisi kwamba pesa ile imepatikana humu kwa ndugu zetu madereva kwa kujisalimisha na kesi isiende Mahakamani. Kwa hivyo, hii rushwa imekuwa na inazidi kuendelea katika nchi yetu hivyo, ningelimuomba sana Mhe. Balozi apambane na suala hili mwisho wa nguvu yake. Mhe. Mwenyekiti, kinyume na hivyo basi Zanzibar tutazidi kurudi chini kiuchumi, tutazidi kudidimia na wale ndugu zetu waliokuwa wanyonge watazidi kupoteza maisha yao hali ya kuwa nchi hii ina uwezo wa kupata maendeleo na kuweza kuizuia rushwa.

Mhe. Mwenyekiti, rushwa ni adui wa haki, rushwa imekemewa katika dini zote, hivyo ningeliomba sana Makamo wa Pili wa Rais ajitahidi kulisimamia suala hili ili kuwafanya Wazanzibari waweze kuishi vizuri. Mhe. Mwenyekiti, katika misingi ya maendeleo ili tupige hatua na tuondoke hapa tulipo, hatuna budi kuwa na maadili yenye kufuata sheria. Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo ni lazima kila wizara, idara na sekta yoyote ya umma wahakikishe tumefuata maadili ili kuifanya sheria yetu inakwenda kama vile tulivyojipangia.

Mhe. Mwenyekiti, pia tunatakiwa tuwe waaminifu kwani kama hatukuwa waaminifu basi hatuwezi kuleta maendeleo mazuri hapa Zanzibar. Kwa hivyo, ni lazima tuwajibike wale wafanyakazi wahakikishe wanafanya wajibu wao, kama serikali ilivyopanga muda wa kazi basi masaa manane tuhakikishe wafanyakazi wetu wamebaki katika maeneo ya kazi na kazi zimekwenda kama vile serikali ilivyojipangia.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine la msingi ni kwamba tuheshimu haki za wote, kwani hapa Zanzibar ubaguzi umekuwa mwingi sana, hatujali wa Donge, hatumjali Mpemba wala hatumjali wa popote pale. Kwa hivyo, ili tuende vizuri basi haki za kila mtu tuzipe wajibu wake.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ni kujituma kwa bidii mimi naomba sana Mhe. Makamo ahakikishe katika wizara zake wafanyakazi wetu wamejituma kwa bidii zaidi. Lakini mimi nataka niseme kuwa ni lazima tuwe na dhamira ya kutenda mambo makubwa, dhamira hii tukenda jambo kubwa kabisa la mafuta ni kuhakikisha mafuta ya Wazanzibari yamechimbwa. Kwa hivyo, tutakapochimba mafuta haya basi matatizo haya yote tuliyonayo basi yataondoka.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana pia na mimi naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii yakuweza kutia baraka kwenye hotuba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Mhe. Mwenyekiti, mimi naanza kwa kusema naunga mkono hoja. Pili, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha Ijumaa ya leo na inshaallah atufikishe tusali kwa jamaa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile namshukuru Mhe. Makamo kwa hotuba yake iliyogusa suala la viwanda na biashara. Kwa haraka haraka suala hili ni suluhisho ambalo tunakubali kabisa kwa nafasi ya Zanzibar kijiografia ndio utamaduni wa visiwa vingi duniani. Mhe. Mwenyekiti, sijui ni shetani gani alitusibu tukaviachia viwanda vyetu kwamba leo tunakuja kuanza kufufua.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema hatujachelewa kama dhamira ni njema na tukayaondoa yale yaliyotusibu mpaka kufika sasa tunakuja kufufua huko mbele ya maelezo yangu labda nitapata jibu la suala hili. Mhe. Mwenyekiti, wajumbe wako mengi wameshayazungumza na yote yana maana na uhimu na uzito wake, lakini kuna jengine ambalo pia na mimi nataka niliguse kwenye kitabu cha hotuba hii kuna changamoto za kitaifa juu ya mikakati ya utekelezaji. Hii ndio *challenge* ambayo sasa hivi inatukabili kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kitabu kinakidhi kwamba tuna matatizo makubwa katika uwajibikaji, utii na nidhamu ndani ya taasisi zetu. Mhe. Mwenyekiti, tuna wimbi kubwa lililotukabili sasa hivi la watendaji kwenye taasisi mbali mbali ingawa sio zote. Tuna watendaji waliojifanya taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba ni mali zao ama ni mirathi kutoka kwa wazazi wao.

Kwa hivyo, wapo wanaotia mikataba mibovu ndani ya taasisi hizi kwa maslahi yao wenyewe pamoja na familia zao. Kuhusu ubadhirifu wa fedha za umma sasa hivi imekuwa ni jambo la kawaida kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupanga watumishi wanaowataka wao maeneo ambayo hawana uwezo nayo. Mhe. Mwenyekiti, jambo hili jana lilisemwa lakini yanafanywa haya kwa sababu yale yale maslahi binafsi, lakini kuna ubaguzi wanabaguliwa watu wale ambao wana uwezo waonekana ni maadui kwa baadhi ya watendaji wa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili tunakuomba Mhe. Makamo uturuhusu wala usitutizame vyenginevyo ili tuwaambie wenzetu Waheshimiwa Mawaziri wanaosimamia taasisi zao wale ambao wanajihisi hawajaweza ama kuwa tayari kusimamia utendaji wao kimaadili ya utendaji, basi waripoti mara moja kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kama kazi imewashinda watoe nafasi kwa wenzao. Mhe. Mwenyekiti, sisi tunataka kuijenga Zanzibar mpya kiuchumi, kinidhamu na Zanzibar mpya kwa kila lilo jema kwa faida na maslahi ya nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, Muungano umetajwa lakini sitowatendea haki Wazanzibari kama sijasema. Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari wanaoupenda Muungano tena kwa mapenzi ya hali ya juu, kama kuna Watanzania waliohangaika na mali zoa ni Wazanzibari kwenye Muungano. Lakini tulikubaliana uwe na maslahi ya pande zote, maslahi ya Zanzibar Mhe. Mwenyekiti yamezungumzwa sana kwamba hayapo na kwa makusudi hayapo kwani wenzetu hawataki kuiona Zanzibar inafaidika ndani ya Muungano huu.

Mhe. Mwenyekiti, Katiba ya Zanzibar ukurasa wa 7 kifungu cha 9(2a) kwa ruhusa yako naomba ninukuu. "Mamlaka yakuendesha nchi ni ya wananchi wenyewe ambapo nguvu katiba utatoka kwa wananchi wenyewe".

Mhe. Mwenyekiti, nimeomba kuinukuu sentensi hii kwa kuiambia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba Wazanzibari sasa walijenga matumaini makubwa na bado wana imani kubwa kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Vile vile Mhe. Rais alimteua Mhe. Makamo wa Kwanza (Maalim Seif Sharif Hamad) na bila ya kukosea akamteua Makamo wa Pili Balozi wetu (Mhe. Seif Ali Iddi).

Mhe. Mwenyekiti, viongozi hawa wakubwa Wazanzibari tumejenga matumaini makubwa sana ya hatma ya nchi hii, na kwa mnasaba huo basi ndugu yangu mwenye dhamana ya fedha alitueleza lakini sitaki kumjibu. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kusema kwamba Wazanzibari sasa wanazihitaji, wanazitaka haki zao ndani ya Muungano zilizokwama kwa miaka 47 sasa tuzikamate wenyewe ili tufaidike wenyewe, tuwezeshe wenyewe kwa faida ya Wazanzibari na maslahi ya nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, hatupigi kelele wala wenzetu wasituelewe vibaya, lakini tunataka haki sawa tumesema kwa maslahi ya nchi mbili, tumesema maslahi ya pande mbili, hivyo kama ni za pande mbili basi Zanzibar ni upande mmoja na Bara ni upande wa pili. Kwa hivyo, haiwezekani, haikubaliki na hata hatukubali tunasema sasa hatukubali Wazanzibari wa majimbo 50 wako pamoja na wawakilishi ndio sisi waliotuleta hapa kudai haki, kusimamia haki zao na tunaiambia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba Wazanzibari wanataka haki zao zilizo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, *message* imefika lakini pamoja na hizo uwiano wa haki ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuwa hapana kwani Wazanzibari wanakosa nafasi hizi kwa visingizio mbali mbali ikitajwa elimu. Mhe. Mwenyekiti, sijui wenzetu wamesoma wapi ambapo Wazanzibari kabla ya mwaka 1964 madaktari wa mwanzo Afrika Mashariki ni Wazanzibari, hivyo hii dharau ya kwamba Wazanzibari hawana elimu inatoka wapi.

Mhe. Mwenyekiti, BoT ni ya Muungano ipo pale kuratibu uchumi wa pande zote mbili. Mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi tunakwenda pale wanatwambia kwa Zanzibar minazi sasa isipasuliwe mbao eti wanaishauri kamati hii ya Baraza lako tukufu. Mhe. Mwenyekiti, sasa wakati umefika tunaiambia serikali kwamba Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ya Mhe. Ali Juma Shamuhuna tunamuomba kwa heshima taadhima katika bajeti yake inayokuja kauli ya mwisho aiambie Baraza hili sheria iliyokwisha tunga, sera tuliyoiipitisha kwenye Baraza hili kuhusu uchimbaji wa mafuta utaratibu utaanza vipi na lini.

Mhe. Mwenyekiti, hili ndilo Wazanzibari wanalolisubiri walisikie kutoka kwa serikali yao vyenginevyo vyovyote wametutuma kuwa hii wizara kwanza tutaiweka upande mpaka itoe jibu. Mhe. Mwenyekiti, sisi wajumbe hatuna nia ya kuizuia lakini tunataka tunayoyasema yawe yanatekelezwa hatukuja hapa kupiga kelele, ila tumekuja kuwawakisha watu kwa faida zao na maslahi ya nchi yao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuheshimu sana muda wako mengine nitayabakisha mpaka tufike inshaallah hiyo siku.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo kwa niaba ya Mawaziri na Manaibu wao kuweza kuchangia hoja ya Makamo wa Pili wa Rais. Kwanza naomba nikupongeze wewe Mhe. Mwenyekiti, na sio tu kwa sababu watu wanasema wanawake wakiwezeshwa wanaweza, mimi naamini Mhe. Mwenyekiti, hujawezeshwa isipokuwa umepewa fursa na unaonesha uwezo wake. Kwa hivyo, naomba nikupongeze kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nimshukuru Mhe. Rais kwa kumchagua Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ili kusimamia ofisi hii na kuweza kutuletea hotuba ambayo hata sisi wanagezi tunaweza kuipitia na kuweza kuichangia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niende moja kwa moja kwenye *point* ya uwezeshaji, nia njema ya serikali ni kuhakikisha kwamba wananchi wake wanatoka kwenye umasikini. Lakini ninachokiona mimi katika sehemu mbili ambazo tunazifanyia kazi tunahitaji kidogo tujisukume hasa kwa upande wa kuwezesha vikundi na miradi ya *TASAF*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa uzoefu niliouone huko nyuma miradi inakuwa midogo midogo mno watu wanaopewa hawana uelewa matokeo yake inakuwa haina tija, kama tulivyoona kwenye *TASAF* zilizopita au kwenye mifuko ambayo imetolewa.

Kwa hivyo, mimi ushauri wangu kwa serikali naomba kwamba kuwe na wataalamu katika kila Wilaya ambao wataweza kuwakusanya wale wahusika ili waweze kuwahamasisha, kuwashirikisha na kuweza kuvumbua miradi ambayo wao wenyewe wataipendekeza, lakini ikiwa na tija wakijua kwamba kweli hii itawasaidia. Pia na kuandika hiyo miradi na baadae ndipo miradi hiyo itekelezwe.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwezekana isiwe miradi midogo midogo tena kama hiyo ya nyuma iliyokwishakupita ya vikundi vya watu wawili watatu, isipokuwa miradi iende kwenye angalau Wadi au Jimbo wanapoweza kufanya jambo kubwa likaonekana. Kwa mfano, hai nimeuona kwetu Muyuni kulikuwa na miradi ya Shehia tatu midogo midogo kila mmoja ana kipesa chake, lakini tumejaribu kuwaelimisha na mwisho wake tukafikia kujenga sekondari ambayo iliwasaidia wananchi wote badala ya ile miradi midogo midogo ambayo Shehia ilipendekeza.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la pili nilikuwa nataka nizungumzie suala la kuwezesha wananchi kiuchumi. Kwenye hili ninaloliona mimi naomba serikali tuwasaidie watu wetu na serikali wenyewe tujisaidie pale ambapo tunapowakaribisha wawekezaji. Mhe. Mwenyekiti, tunapenda wawekezaji waje na watusaidie, lakini linapokuja suala la ardhi au labda rasimali ya serikali badala ya kuwa tunawapa kwa muda mrefu au wananchi wanauza, bora tushirikishwe kama ubia.

Kwa hivyo, mwananchi awe mbia labda kwenye ardhi yake kwa yule mwekezaji au serikali iwe mbia kwa kile ambacho kinawekezwa ili tuweze kupata tija endelevu, badala ya kumpa mtu au kumuuzia mtu halafu yeye akaendelea kupata kadri siku zinavyokwenda na yule mtu akabakia masikini kwa sababu alichopewa kimeshatumika.

Vile vile ningependa nizungumze kuhusu suala la kilimo kwani juhudi zimeoneshwa na serikali kwa mbegu nzuri, matrekta, mbolea. Pia tunalizungumzia suala la umwagiliaji maji kwani wataalamu wa umwagiliaji bado tunao kidogo naomba niongeze nguvu ya kuwasomesha ili haja iweze kukidhiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la elimu na teknolojia kilichonifurahisha zaidi ni elimu ya awali ya msingi maana hapa ndio ninapouona mwanzo wa kupata wanafunzi ambao wataingia kwenye hizi skuli za Wilaya 19 ambazo zinajengwa wakiwa na msingi bora zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nizungumzie suala la afya kama sijasikia basi sisikii tena maana kila anayesimama, kila linalozungumzwa sisi tunaonekana zaidi

kwa sababu tuko katika maisha ya binadamu, wengine wote wakifanya hawaonekani sana. Lakini nasema kuwa nimesikia na tutajitahidi, tutarekebisha, tutasimamia maana ndio kazi tuliyopewa.

Mhe. Mwenyekiti, nikija kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja kweli tunataka iwe ya rufaa, hivyo tutayafuatilia yaliyotamkwa kwenye hotuba, tutashirikiana na kikosi cha wataalamu wa SMZ kufuatilia makubaliano kuhusu Hospitali ya Rufaa hasa katika yale makubaliano pamoja na Serikali ya Iran.

Hata hivyo, hapa ninaloliona ni suala la nishati mbadala. Mhe. Mwenyekiti, nishati mbadala ninaiona ina uhimu kwa sisi wanawake na hasa kwa mazingira. Nataka nizungumzie kuhusu kikundi kimoja tu ambacho nimekikuta wakati wa maonesho ya *May Day* na juzi kwenye kikundi cha mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kikundi pale kinatoka Mwanyanya ambacho kinajihusisha na kuzungusha taka taka na kuzifanya kuwa makaa ule ni mradi mpya nasikia mwengine uko lakini nataka ufuatilie niujue, lakini huu kwa vile nimeuona ni taka taka tu ambazo watu hatuzithamini ni makaratasi ndicho kinachotumika. Miradi hii inafanyika Tanzania Bara tena inafanyika kwa wingi Rwanda, Burundi, Congo na Uganda. Mhe. Mwenyekiti, ni miradi mikombozi kwa hawa wanaoitenda na pia imefanya kazi kubwa ya kusafisha mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningependa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ahakikishe kwa sababu aliwapa na *certificate* wale wa Mhe. Waziri wa Uwezeshaji awasaidie kwa sababu wanachokihitaji ni kidogo tu kuweza kuwasukuma kutoka pale walipo na watakuwa ni mfano na ni walimu kwa watu wengine. Hivyo, nitahakikisha kwamba mji wetu unasafika na wakati huo huo tunapata nishati mbadala.

Mhe. Mwenyekiti, pia ningependa nizungumze kuhusu suala la utafiti. Hapa kulizungumzwa kuhusu Tume ya Mionzi, tume hii kwa nchi yetu ni muhimu kwa sababu mimi nakumbuka wakati nimeanza kazi kitengo cha *x-ray* kilikuwa ni kimoja tu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, sasa hivi hospitali zote zina vitengo vya *x-ray*. Mhe. Mwenyekiti, tuna ma *ultrasound*, tuna *CT Scan* na mengine mengi yanakuja. Mhe. Mwenyekiti, bila ya kuwa na hiyo tume hapa nchini kwetu kwa kutegemea tume iliyoko Arusha kuja kutufanyia kazi hapa kwa kweli huwa inachukua muda mpaka kufika, na mambo mengi huwa yanasimama kwa sababu inabidi tusubiri tume hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo labda lingekuwa la mwisho ni kuhusu mifugo cya CDF kwa kweli nafikiri hili litakuwa ni jambo la maana kama litatiliwa mkazo, lakini bado usimamizi uje uwe kama huu ambao wa miradi ambao ulianzishwa vyenginevyo tutakuwa tunafanya kazi lakini mwisho wake

hatutapata tija inayotakiwa. Kwa nafasi hii iilyonipa Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru na ninapenda kuunga hoja hii iliyotolewa katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi nikachangia hotuba hii ya Makamo wa Pili wa Rais. Kwanza nianze kumpongeza Mhe. Makamo wa Pili wa Rais pamoja na watendaji wake wote. Pia nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kumteua Makamo wa Pili wa Rais kuweza kutekeleza wajibu wake kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu muda ni mdogo mimi nichangie kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kuhusu utalii. Kwa kweli waheshimiwa wenzangu wanawake wamegusia kwenye utalii, mimi nawaomba waheshimiwa musiogope kuwapeleka watoto wetu wanawake kwenye kufanya kazi katika maeneo ya utalii na wala msiwe na wasi wasi na serikali iko pamoja na wao.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije kwenye habari nampongeza Mhe. Makamo kwa kuweza kutekeleza wajibu wake kwenye serikali kwa kuweka miundombinu thabiti iliyokuwa ni ya kubadilisha mfumo mpya wa kuondoka kwenye *analogue* na kwenda *digital*. Mimi naipongeza serikali, nampongeza Makamo wa Pili wa Rais kwa kuliona hilo. Pia nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi mnaotoka Pemba msiwe na wasi wasi na mitambo yenu imeshafika Pemba na Mwenyezi Mungu akitujaalia itafungwa na mufurahi zaidi kuona mambo mbali mbali yanayotoka kwenye televisheni ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niende kwenye utamaduni kwa kweli utamaduni nao umeguswa sana na unatugusa sisi Wazanzibari sote, hili nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi muwe watu wa mwanzo kuweza kuielimisha jamii kuhusu mila la desturi na utamaduni wetu wa Kizanzibari usipotee uimarike zaidi. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, nafasi ni ndogo sana kwani tulikuwa tuna mengi sana yakuchangia kwa kuisaidia serikali lakini nakoma hapo na nakushukuru kwaniaba ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo pamoja na Mhe. Waziri wangu na kwa niaba ya Mkoa wa Kaskazini Pemba naiopengeza hotuba hii ya bajeti mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nishukuru kwa kunipa fursa hii yakuchangia hotuba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais (Mhe. Balozi Seif Ali Iddi). Mhe. Mwenyekiti, kama mnavyoelewa kuhusu sekta ya utalii duniani ni sekta moja ambayo ni muhimu sana katika kujenga uchumi na nchi nyingi leo zinaitegemea sekta hii zimetoka

kwenye sekta nyengine au kupanua wigo ili kuingia katika sekta ya utalii baada ya kuona umuhimu wake wa kujenga uchumi kwa haraka sana.

Mhe. Mwenyekiti, kama unavyokumbuka kwamba Zanzibar tumeingia katika sekta hii ya utalii ni baada ya kuanguka kwa zao letu muhimu sana la karafuu katika soko la dunia na serikali ikaamua kwa makusudi kupanua wigo ili kusaidia na sekta ya kilimo na zaidi kusaidiana na zao la karafuu, ili kujenga uchumi imara kwa kuongeza mapato na wananchi wetu waweze kuishi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, sekta ya utalii imeanza kukua mara tu baada ya serikali kuamua kujiingiza katika sekta hii na hasa pale baada ya hali ya uchumi wa dunia kurudi katika hali yake ya kawaida mwaka 2004-2005. Pia katika mwaka 2007 hali ya idadi ya watalii walioingia ndani ya nchi kwa kweli iliongezeka maradufu, lakini katika mwaka 2008 kidogo idadi ya watalii ilishuka na hasa baada ya lile tukio la Septemba, 11 2001 kidogo idadi ya watalii walioingia nchini ilipungua. Mhe. Mwenyekiti, lakini katika mwaka 2009 hali ya uchumi duniani ilirudi katika hali ya kawaida na idadi ya watalii ikarudi kama mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, takriban kadri unavyokuwa huwa unakuwa na mahitaji mengine, utalii ulivyokuwa na ukuwaji wa idadi ya mahoteli nayo vile vile imekuwa, ongezeko la mikahawa, ongezeko la *tour operators* nalo lilikuwa. Mhe. Mwenyekiti, sambamba na huduma ambazo zinaambatana na sekta hii ya utalii kama vile mawasiliano, viwanja vya ndege, bandari pamoja na huduma za benki nazo huwa zinakwenda sambamba na ukuaji wa sekta hii ya utalii.

Mhe. Mwenyekiti, mtalii anapokuja hapa maana yake huwa anakuja kupumzika, anakuja kuona namna gani tunavyoishi, utamaduni wetu, anakuja kuangalia vivutio vilivyoko ndani ya nchi yetu. Kwa hivyo, kwa kweli hali ya usalama inahitajika kwa sababu kadri utalii unavyokuwa na hali ya usalama nayo vile vile huwa inahitajika. Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuishukuru wizara yangu kushirikiana na Kamisheni ya Utalii na kulishukuru Jeshi la Polisi kwa juhudi zao za ulinzi na usalama kwa wageni wetu pamoja na mali zao.

Mhe. Mwenyekiti, mtalii kabla ya kufanya maamuzi ya kuja hapa huwa anaangalia kitu usalama, kwa hiyo usalama ni kitu muhimu sana kwa sekta hii kwa sababu bila ya usalama basi mtalii haji hapa. Leo mtalii hawezi kwenda Somalia, mtalii leo hawezi kwenda Libya, hawezi Syria kwa sababu humo hamna usalama na yeye. Kwa hivyo, naomba wajumbe hili suala la kulinda sekta hii liwe ni jukumu lao sote, tulinde kama ipasavyo na tutekeleze kama ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, mtalii anapopata huduma nzuri anapokuja hapa kwa kweli anabakia ni balozi mzuri wa kuitangaza Zanzibar kwa hiyo huwa anatusaidia na atakapopata huduma mbovu vile vile huwa anatutelekeza. Kwa hivyo, bado jukumu la kuilinda sekta hii liko pale pale na umuhimu wake.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile wizara ikishirikiana na Kamisheni ya Utalii haikusita hapo tu katika kuimarisha uchumi na kujenga uchumi kila unapoingia msimu wa utalii kwa kweli tuna utamaduni wa kukaa na wahusika wote wanaohusiana na sekta hii ya utalii ili kufanya tathmini ya msimu ulopita na kujenga mwelekeo mpya wa namna gani tuendeshe utalii wetu. Mhe. Mwenyekiti, jambo hilo tumelishalifanya kwa hivyo kwa vile muda haupo mimi nichukue fursa hii tu kuishukuru hotuba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na kuiunga mkono mia kwa mia na kuwapongeza wale wajumbe wote ambao wameipongeza na kuiunga mkono hotuba hii, namtakia kila la kheri. Ahsante sana.

(Saa 6:00 Mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)
(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea, nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyekiti, Mhe. Mgeni Hassan Juma kwa kazi nzuri ambayo ameifanya na amenipa taarifa kwamba wajumbe karibu wote wamemaliza wamebakia Waheshimiwa Mawaziri ambao watamsaidia Mhe. Makamo wa Pili wa Rais.

Kwa hivyo, muda wetu si mkubwa sana, nitaomba Waheshimiwa Mawaziri wale ambao wameomba kumsaidia Mhe. Makamo wa Pili wa Rais tujaribu kutumia muda usiokuwa mkubwa ilimradi tu Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na hatimaye Mhe. Makamo wa Pili mwenyewe waweze kumalizia majumuisho na hatimaye tupitishe vifungu mbali mbali vya ofisi hii vikiwemo vya Baraza la Wawakilishi ili tuweze kufanya kazi kwa msimu huu tunaoanza nao wa Julai mosi. Kwa hivyo, nitangulie kumkaribisha Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa jioni hii ya leo kunipa nafasi ya mwanzo. Kwa kweli sitochukua muda wako mwingi isipokuwa nataka nitumie nafasi hii kutoa wasi wasi kwa baadhiya Waheshimiwa Wajumbe katika suala zima walilozungumzia hasa suala zima la kuondosha umasikini na kuwawezesha wananchi.

Lakini kabla sijasema hayo, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Kwa kweli amewasilisha bajeti kwa ufasaha, umakini na sekta zote ambazo zimehusika kwa hapa Zanzibar basi amezungumzia kwenye kitabu chake hata kama kwa ufupi, lakini amezizungumzia na nadhani mawaziri tunaohusika sote tumefahamu. Kwa hivyo, nichukue nafasi hii kumpongeza sana yeye na waziri wake Mhe. Moh'd Aboud pamoja na watendaji wote kwa kuiandaa bajeti ile ambayo inaeleweka kwa urahisi sana.

Mhe. Spika, katika mjadala wetu huu wa kuchangia hoja hii waheshimiwa wengi walizungumzia suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi. Hili ni jukumu letu sote, lakini wizara hii nimekabidhiwa mimi. Sasa nataka niwatoe wasi wasi kwa sababu hiyo wizara yangu nikiielezea sasa hivi tena bajeti yangu itakuwa ndio nimeshaisoma hapo, isipokuwa wavute subira wangojee bajeti yangu nitakapoiwasilisha hapa nina hakika kabisa wataridhika kama ilivyowasilishwa Hotuba ya Bajeti ya Serikali watu wakaifurahia basi na bajeti hii wakae mkao wa kusikiliza na bajeti ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika na wataifurahia sana. Kwa sababu itamgusa kila mheshimiwa aliyemo humu ndani na itawapa faraja kubwa kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka 2015 tukijaaliwa.

Limezungumzwa suala la kuwawezesha wananchi. Mhe. Abdalla Juma Abdalla alizungumza kabla hatujawawezesha tukawapatia fedha ingelikuwa vizuri basi watu hawa tukawapatia mafunzo. Mhe. Spika kwa taarifa ya wajumbe haya mafunzo tayari yameshaanza sasa hivi yanaendelea na tunaendelea kufanya ziara katika wilaya zote sasa hivi. Lakini pale ambapo waheshimiwa wenyewe, na ninashukuru kuna baadhi ya waheshimiwa wamekuja pale ofisini wakatuomba kwamba, tayari wanavyo vikundi vyao vya ushirika, vikundi vya *SACCOS* na vikundi vyengine ambavyo wameandaa katika majimbo yao wangehitajia labda kupatiwa mafunzo juu ya uwezeshaji. Tumefanya hivyo na tumekwenda.

Natoa wito kwamba bado waheshimiwa wale ambao wangehitajia pengine tuwahi kabla hatujachelewa kwa sababu maombi ni mengi, basi walete wataalamu wako tayari na ninakuhakikishia Mhe. Spika, kwamba tutayafanya hayo kwa sababu Mhe. Rais wa Zanzibar ameanzisha wizara hii kwa madhumuni hasa ya kutupunguzia umasikini na pengine kuuondosha kabisa katika miaka mitano na mingine ijayo.

Jengine ambalo nataka nilizungumzie kidogo kuhusu hii mikopo ambayo imezungumzwa ya JK na AK kwa upande mmoja. Mhe. Spika, namshukuru sana Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ametoa ufafanuzi. Tayari nataka niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wajumbe

Benki Kuu ya Tanzania kwa kushirikiana na PBZ pamoja na wizara yetu, tumefanya mitano miwili, mmoja tumefanya hapa Unguja na mwengine umefanyika Pemba. Namshukuru sana Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba ambaye alifungua mkutano ule kwa niaba yangu.

Madhumuni pia ilikuwa kuwaalika na wale ambao tumewapa mikopo na zile taasisi ambazo kwa njia moja au nyengine zinahusika katika utoaji wa mikopo. Mhe. Spika, tumefika pahala pazuri na hivi sasa kwa taarifa mikopo ile imeshaanza kutolewa tena na tunatarajia itaendelea. Kwa sababu kama nilivyosema kulikuwa na hakiba ambayo bado ipo karibu shilingi bilioni 2.2 ambayo inahitajiwa kutolewa. Kwa hivyo, itaendelea kutolewa na nina hakika kadiri siku zinavyokwenda na wenzetu, marafiki zetu na washirika wengine wa maendeleo wataendelea kutusaidia kwa lengo la kuondosha umasikini.

Wizara hii inagusa kila wizara, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maliasili tupo, uvuvi tupo, biashara tupo, yaani kila utapoangalia basi utamkuta Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kakaa pale anakusubiri. Mimi malengo ambayo tumejipangia sitoyakalia kitako, nitayasimamia barabara. Kwa sababu ndio yanayohitajika ukisema unayakalia ndio yale tena hayaji juu.

Tulikwenda Pemba na Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi na Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo tukiwa pamoja kuna mwananchi mmoja alitwambia pale kwamba, alikuja mheshimiwa mmoja akatupa maelezo kuwa matatizo haya anayachukua na wanakwenda kuyakalia kitako na akasema kweli maana yake hayakuja juu mpaka leo Mheshimiwa.

Sasa sisi nadhani Waheshimiwa tuliokuwemo humu ndani na mawaziri wa awamu hii ya serikali ya Umoja wa Kitaifa hatutoyakalia kitako tutayasimamia na tutashirikiana. Kwa sababu kila mmoja ana wajibu wa kumsaidia mwenzake na kushirikiana na mwenzake.

Nadhani Mhe. Spika, mimi nisiendelee kuchukua muda wako wasubiri bajeti yangu Inshaallah inakuja tarehe 17 na 18 Julai. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Makunduchi tunaunga mkono hoja ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais aliyewasilisha hotuba hii. Inallaha maanswabirina. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia na mimi machache katika Hotuba ya Makamo wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi.

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa hotuba yake nzuri ambayo imepangika na

maneno yote ambayo yamo katika hotuba hii ni masuala yanayotekelezeka. Mimi kwa upande wangu nataka kuchangia machache tu.

Kwanza nianze na ukurasa wa 14 ambao umeelezea habari ya uimarishaji wa sekta binafsi. Kupitia Wizara yetu ya Biashara, Viwanda na Masoko tuna jukumu la kuratibu na kuongoza Baraza la Biashara. Nataka niuhakikishie ukumbi huu kwamba, wizara yetu imejidhatiti kwa sababu kama mlivyoona katika hotuba hiyo kwamba serikali imeweka mkakati huu wa kuimarisha sekta binafsi na wafanyabiashara wote wa sekta binafsi wamefarijika sana na masuala ya Baraza la Biashara. Hotuba ya jana kwa kweli imewapa faraja kubwa sana kuona kwamba Mhe. Balozi Seif Ali Iddi anawajali sana sekta binafsi.

Jumuiya ya Wafanyabiashara nayo vile vile imeleta salamu zake kufurahishwa na hotuba hii na kwamba ilitarajia kwamba Mhe. Makamo wakati atakwenda safari zake za nje awachukue na baadhi ya wafanyabiashara katika ziara zake ili waweze kuimarisha masuala ya kibiashara baina ya Zanzibar na nchi za nje.

Baada ya hapo kulikuwa na masuala ya *TRA*. Wafanyabiashara vile vile wamenilalamikia kwamba ni kweli kabisa kuwa bado masuala ya *TRA* ni kiini macho, kwamba bado wanahangaishwa na utaona kuwa ni masuala ya kiutendaji. Mimi nina hakika kwamba chini ya uongozi wa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais tutasimamia ipasavyo kuona kwamba *TRA* inawajibika kuhusiana na masuala haya ya kutoza ushuru mara mbili mpaka tatu.

Mhe. Spika, ukiangalia hasa umuhimu wa kuunganisha nchi zetu ni masuala ya kisiasa na kiuchumi. Tumo katika mkakati wa Soko la Afrika Mashariki, Soko la *SADC* na Soko la *COMESA*. Soko la Afrika Mashariki la watu 97 milioni kufikia Soko la *SADC* la watu 300 milioni mpaka kufikia katika *COMESA* la watu 700 milioni. Sasa ikiwa leo Solo la Tanzania Bara hatupewi fursa itawezaje kuweza kuchukua soko la watu 700 milioni la *East Africa*, *SADC* na *COMESA*.

Mhe. Spika, urari wa biashara baina ya Watanzania Bara na Tanzania Visiwani hauko mzuri. Katika mwaka 2009 Tanzania Bara kutoka Zanzibar tumeingiza bidhaa zenye thamani ya shilingi 19.65 bilioni, na kutoka Visiwani kupeleka Tanzania Bara tumesafirisha mizigo yenye thamani ya shilingi 4.26 bilioni. Katika mwaka 2009 kuna nakisi ya 15.39 bilioni.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010 tumeagiza bidhaa kutoka Tanzania Bara zenye thamani ya shilingi 23.26 bilioni na kutoka Zanzibar tumesafirisha bidhaa zenye thamani ya shilingi 3.3 bilioni. Kwa hivyo, katika mwaka 2010 kuna nakisi ya shilingi 19.96 bilioni, hakuna sababu zozote za kimsingi za wenzetu

wa Tanzania Bara kuanza kuchacharika kwani urari wa biashara baina yetu na wao una tofauti kubwa sana. Nina imani kwamba chini ya uongozi wa Mhe. Rais wa Zanzibar, Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, (SSS) nina imani suala hili litapatiwa ufumbuzi kwa haraka kwa sababu ni suala ambalo kidogo linaleta maudhi katika masuala ya *export*.

Mhe. Spika, katika masuala ya *export* hatuwezi kuendelea kama hatukuongeza idadi ya usafirishaji. Kwa taarifa ya ukumbi huu Zanzibar ni nchi ya mwisho kabisa katika Afrika Mashariki kwenye *export as percentage of GTB.* Nchi ya kwanza ni Uganda yenye *export as percentage of GTB ya 17.16,* Kenya 14.78, Tanzania Bara 10.95, Burundi 4.68, Rwanda 3.79, lakini Zanzibar ni 3.38. Kwa hivyo, chini kabisa, tuna kazi ngumu na kubwa ya kuchupa kutoka hapo tulipo hata tukawafika wenzetu wa Uganda.

Kwa hivyo, ili tuweze kuchupa hapo tuwe na mtaji mkubwa sana, mtaji ambao haupungui shilingi 15 bilioni US$. Kwa hali hiyo basi, jambo pekee litakaloweza kutuokoa ni kuweza kuchimba mafuta yetu wenyewe, tukiweza kufanya hivyo tutapata mchupo wa kuruka kutoka hapa tulipo sasa hivi na kuweza kuwafikia wenzetu ambao wako mbali sana na sisi. Kwa hivyo, imani yangu iko pale pale kama Waziri wa Biashara kwamba tutafanya kazi ya ziada kuona kwamba tunachupa kutoka 3.38 na kufikia katika *double digit.*

Mhe. Spika, la mwisho ni suala la viwanda. Katika hotuba hii imeelezwa kwa urefu kabisa kwamba tunayo azma ya kujenga na kuimarisha na kufufua viwanda. Nataka niwahakikishie kwamba Wizara yetu ya Biashara imejidhatiti kwa kila njia kuona suala hili linatimizwa na viwanda vitavyopewa kipaumbele kwa sasa hivi ni viwanda ambavyo vitatumia *raw materials* ambazo ziko *available* visiwani kwetu. Kama vile karafuu na makonyo ya karafuu kwa ajili ya kutengeneza *perfume,* madawa, *beauty product, tooth paste, creams, bums na cigarettes*. *Sea weed* vile vile viwanda vya *seller dressing*, *sauces* na vitu vya *conservative* vitafanyiwa kutoka katika *sea weed* kutokana na samaki, minofu ya kusindika pamoja na samaki wa kukausha, viwanda vya vifaa vinavyotokana na mpira, viwanda vinavyotokana na ndizi mpaka mafuta yanatoka katika ndizi, vile vile kutokana na mihogo na kutokana na ngozi, mbao, nguo pamoja na vifaa vyengine vya *candies* na *bakeries*.

Viwanda hivi vitaweza kusaidia sana kuamsha ari ya ukuaji wa viwanda na kuweza kuongeza usafirishaji. Kwa hivyo, mimi nataka niwahakikishie kabisa kwamba Wizara ya Biashara imejidhatiti chini ya uongozi wa viongozi wetu hawa watatu na tunaamini kwamba yote haya yaliyozungumzwa hapa tutayakabili kwa njia zote na *Inshaallah* tutafanikiwa. Baada ya kusema hayo nasema ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana, nafikiri kati ya mawaziri ambao waliomba tumewamaliza bado Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na hatimaye Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Lakini kabla ya kumuomba Mhe. Waziri naye achangie hoja hii, naelewa kwamba wajumbe wengi walikuwa na hamu ya kuichangia hoja hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, lakini kufuatana na ufinyu wa muda sio wote ambao tumepata hiyo nafasi. Kuna wengine tangu jana nilipokuwepo walionesha hamu kubwa sana na masuala ya hamu matatizo yake tunayaelewa sote. *(Makofi)*

Sasa nataka niwaombe radhi wale wote ambao waliomba nafasi lakini ikawa hawakupata kuchangia, mmoja wapo ambaye amenikumbusha hayo ni Mhe. Salim Abdalla Hamad wengine inaonekana wamechangia changia japo kidogo, lakini kama kuna wengine ambao waliomba na wakakosa nafasi kwa ujumla wao naomba radhi sana kwa kukosa hiyo nafasi.

Najua nia ilikuwa ni kumsaidia Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ili kuweza kufanya vizuri katika mwaka ujao wa fedha wa 2011/2012. Waheshimiwa Wajumbe naomba radhi sana, ufinyu wa muda umetufanya tusimudu kuwaita wote.

Baada ya hayo basi sasa namuomba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Mapamo wa Pili wa Rais kumsaidia Mhe. Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa jioni hii. Aidha, kwa kutuwezesha kuendelea na mchakato wetu huu wa bajeti. Namuomba Mola atusaidie tuimalize bajeti hii ya Hotuba ya Makamo wa Pili wa Rais kwa salama na zinazokuja zote zimalize kwa salama ili tuweze kufanikisha malengo ya wananchi.

Mhe. Spika, nataka nikushukuru wewe binafsi kwa namna ambavyo unaliongoza Baraza letu hili tukufu, kwa kweli ni Spika wa mfano nakushukuru sana.

Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza sana rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuongoza nchi yetu. Lakini vile vile nimpongeze kwa umahiri mkubwa aliyoonesha katika uongozi wake. Napenda nichukue fursa hii kumshukuru sana yeye Mhe. Rais kwa kuniteuwa mimi kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, namshukuru sana.

Aidha, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais kwa kuteuliwa nafasi hiyo na kwa namna anavyofanya kazi zake vizuri. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa

kuteuliwa kuwa Makamo wa Pili wa Rais. Lakini pia kwa namna anavyoiongoza vizuri sana ofisi hii na mashirikiano makubwa anayotupa sisi watendaji katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Mheshimiwa tunakushukuru sana.

Nataka pia nichukue fursa hii kuwashukuru mawaziri wenzangu wote na manaibu waziri kwa namna tunavyoshirikiana katika shughuli zetu za kila siku. Nataka niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu wote kwa namna ambavyo mnatupa mashirikiano makubwa. Na shukurani za kipekee niishukuru sana sana familia yangu kwa ustahamilivu wao na uvumilivu mkubwa wanaoonesha juu yangu. Kwa sababu Mhe. Spika, kazi hizi huwa mara mbili, licha ya ofisini na nyumbani pia unarudi na makabrasha yanayochukua muda mrefu. Kwa hivyo, nawashukuru sana kwa namna wanavyonistahamilia.

Mhe. Spika, nimshukuru sana Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Afisa Mdhamini na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa mashirikiano yao makubwa juu yangu, nawatakia heri na mafanikio makubwa.

Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo kwana nataka niseme naunga mkono hoja hii iliyo mbele yetu. Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wameonesha ujasiri na umahiri mkubwa katika michango yao wakati wa kuchangia Ofisi hii ya Makamo wa Pili wa Rais. Kwa kweli michango yao ni ya kina na ambayo imetupa mwanga mzuri sana kwa kutusaidia kufanya shughuli zake.

Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu na wananchi wote wa Zanzibar kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar siku zote itakuwa tayari kushirikiana na wananchi wake katika kujenga Zanzibar mpya yenye maendeleo, umoja na maelewano.

Mhe. Spika, serikali yetu itachukua kila hatua kuhakikisha kwamba maslahi ya Zanzibar yanalindwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nataka niwahakikishie hilo wajumbe wote wa Baraza hili tukufu. Na serikali yetu chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohammed Shein imejipanga kuzitumia rasilimali zake zote kwa ukamilifu ili zisaidie maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, katika hoja mbali mbali zilizotolewa hapa imeonekana wazi kwamba wajumbe wote watakubaliana nami kwamba Muungano wetu ni jambo muhimu kuwa nalo. Lakini vile vile zile kasoro ambazo zinajitokeza basi tuchukue jitihada za kuziondoa, cha msingi hapa ni kulinda maslahi ya Zanzibar ndani ya Muungano huu.

Mhe. Spika, unapoumwa na kidole hukati mkono mzima unakitibu kidole, kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakubaliane kwamba tushughulikie kutatua matatizo yaliyopo na tuimarishe Muungano wetu.

Katika suala la Muungano Waheshimiwa Wajumbe wako wa Baraza hili tukufu…

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwaombe radhi tena, huo umerudi umeme. Niwaombe radhi sana Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, karibuni hivi tatizo hili la kukatika kwa umeme litamalizika. Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu walielezea kwa masikitiko makubwa kwenye masuala ya Muungano na sana walizungumzia yafuatayo:-

Walizungumzia suala la Kero za Muungano kwamba hazipati ufumbuzi, wakazungumzia kwamba Muungano unaikosesha fursa Zanzibar za kukua kiuchumi, na kuna wengine walihoji uhalali wa Kamati ya Pamoja ya Kushughulikia Kero za Muungano. Nasema wapo waliohoji hata mfumo wenyewe wa Muungano.

Mhe. Spika, hii yote inaonekana inatokana kwa suala la muda mrefu la kuchelewa kuyapatia ufumbuzi sahihi matatizo yaliyomo ndani ya Muungano wetu.

Mhe. Spika, kuhusu mfumo wa Muungano. Mhe. Spika, lazima tuelewe kwamba mfumo wa Muungano kwanza unatokana na matakwa ya Kikatiba. Lakini isitoshe mfumo huu unagusa maslahi ya wengi, maana mfumo huu umo pia katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ambayo ndio tunayoitekeleza na ina ridhaa ya wananchi wengi.

Kwa hiyo Mhe. Spika, kwa mazingira yetu ni vizuri sana tuwe wavumilivu sana katika suala zima la kuimarisha Muungano wetu. Pale penye kasoro basi ni vizuri tukazizungumza lakini kwa kuamini kwamba nia ni kuimarisha Muungano wetu.

Mhe. Spika, vile vile tumezungumzia sana suala la muundo huu wa Muungano lakini ningependa kutoa ushauri. Si muda mrefu tutakuwa na mchakato wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, tutoe nafasi kwa wananchi wetu kutoa maoni yao na huo utakuwa ndio muelekeo mzuri.

Mhe. Spika, pia nataka nimkumbushe sana ndugu yangu Mhe. Saleh Nassor Juma alifikiri kwamba mchakato unaokuja ni kufanya marekebisho, si kufanya marekebisho ni kufanya mabadiliko ya kuwa na Katiba mpya. Vile vile katika mchakato huo kutakuwa pia na utaratibu wa kuwepo na Bunge la Katiba. Bunge hilo la Katiba mara hii Mhe. Spika, ninahakika hata Wajumbe wako wa Baraza tukufu hili watakuwa miongoni mwa Bunge hilo la Katiba. Hatokuwemo tena Mzee Pasiganda. Mhe. Spika, Mzee Pasiganda yupo Mchangamdogo kapumzika tumuombee dua aendelee kupumzika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika mchakato huu kutakuwa pia na kura ya maoni itakayopigwa na pande zote mbili za Muungano wetu. Kwa hiyo, mchakato mzima wa Katiba utaridhiwa na pande mbili za Muungano wetu kwa utaratibu mzuri kabisa. Hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu tuvute subira sana ili tuone hatma njema ya nchi yetu inavyokwenda.

Mhe. Spika, kuhusu uhalali wa Kamati ya Pamoja ya Kero za Muungano, jambo hili lilizungumzwa sana na Mhe. Rashid Seif Suleiman. Mhe. Spika, nataka nikuhakikishie kwamba Kamati ya Pamoja ya Kushughulikia Kero za Muungano ipo kihalali. Maana kamati ile ni uamuzi wa Marais wetu wawili Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa niaba ya wananchi wao. Wameamua hili ili kushughulikia matatizo ya wananchi wao na kuondoa kero zilizopo katika Muungano wetu. Kwa hiyo, walivyofanya vile walifanya kwa nia njema na mimi naamini kabisa kwamba kamati hii imeanza kufanya kazi nzuri ijapokuwa inayo changamoto.

Mhe. Spika, nataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba hatua zitachukuliwa katika kuondosha kero hizo. Marais wetu wana haki kamili ya kufanya hivi ili kuondoa matatizo yetu. Sio kila jambo linahitaji kwenda kwenye Mahakama ya Katiba, kuna mambo tunaweza kuyafanya wenyewe vizuri kwa nia njema ya kuondosha matatizo yaliyopo na tuimarishe Muungano wetu. Nia ya kushughulikia kero ipo, uwezo wa kuondoa kero upo na dhamira ya kutekeleza maamuzi ipo. Nataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwamba yale yaliyokuwa ni matatizo tutafanya kila jitihada yasiwe tena matatizo.

Mhe. Spika, changamoto kubwa inayotukabili ni mambo mawili. Moja ni kuchelewa kwa muda mrefu kuzipatia ufumbuzi Kero za Muungano. Lakini la pili baada ya kujadiliana na kukubaliana namna ya utekelezaji kwa yale ambayo tuliyoamua. Sasa hatua gani tunachukua.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais tumeanza kuandaa mfumo maalum kwa utekelezaji wa maamuzi tuliyokubaliana. Hiyo ndio itakuwa agenda kuu tutakayokwenda kuizungumza katika kikao chetu kinachofuata cha

pamoja, ili tuweke utaratibu wa namna ambavyo tutatekeleza yale yote tuliyoamua ili kuondosha matatizo yaliyo mbele yetu. Nawaombeni sana Waheshimiwa Wajumbe tushirikiane ili mambo haya tuyatekeleze vizuri.

Mhe. Spika, kwenye upande wa Msemaji Mkuu wa Serikali. Mhe. Spika, kwa mambo makubwa yanayogusa nchi yetu Msemaji Mkuu wa Serikali ni Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Lakini Waheshimiwa Mawaziri wanasemea katika sekta zao, Mawaziri wote wanakuwa wasemaji wakuu kwenye wizara zao wakishirikiana na Makatibu Wakuu. Kwa maana hiyo hiyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais anasemea yanayohusu wizara yake na yale mambo mengine ya kawaida ambayo Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ataelekeza tuyasemee basi tunayasemea pia.

Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu, milango yetu iko wazi kwa waandishi wa habari wote, wakati wowote na sio Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Lakini hii inatakiwa kwa wizara zote za serikali milango inakuwa wazi na hivyo ndivyo ilivyo ili wananchi wetu wapate taarifa kamili ya yale tunayoyafanya. Kwa kuwa tumeanza utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ni vizuri kila wizara ikawa inatoa taarifa hizo kwa msingi wa wananchi wetu kujua yale ambayo tumeanza kuyatekeleza.

Mhe. Spika, kuhusu Ushirikiano wa Afrika Mashariki, jambo hili limezungumziwa sana na Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Subeit Khamis Faki na baadhi ya waheshimiwa wengine.

Mhe. Spika, kwa kweli ndugu yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu amenipa mtihani mkubwa wa kulizungumzia jambo hili kwa sababu kubwa nne. Sababu ya kwanza suala la ushirikiano wa Afrika Mashariki halisimamiwi katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, liko chini ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ndio maana hukuliona katika hotuba yetu.

Sababu ya pili kwamba suala lenyewe ni jambo ambalo lina matakwa ya Kikatiba. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nyongeza ya kwanza ya ibara ya 4 (2) inasema mambo ya nchi za nje ni mambo ya Muungano.

Jambo la tatu ni uzoefu ambao tumeanza nao kwa hivi sasa tunavyoshirikiana kati ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye ushiriki wa vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mpaka sasa hatujapata matatizo makubwa katika ushiriki huu ambao tunakwenda nao.

Lakini jambo la nne ni kubwa linahitaji kutafakariwa kwa kina, linahitaji maamuzi ya wengi, siwezi tu mimi mmoja hapa kufanya uamuzi wa kujitoa katika ushirikiano huu ambao tunakwenda nao sasa. Kwa hiyo, suala lake

lilikuwa zito kwangu kumjibu moja kwa moja kwa sasa. Hasa Mhe. Spika, ukiangalia kwamba kabla ya kuanzishwa mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wananchi wetu walipewa nafasi ya kutoa maoni yao kwenye suala hili.

Hivyo Mhe. Spika, ushauri wangu tuendelee na mfumo wetu wa sasa tulionao wa ushiriki katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kama kutakuwa na maoni yoyote basi kwa sababu mchakato wa Katiba unakuja tuwaachie wananchi watuongoze katika kutoa maoni yao.

Mhe. Spika, utaratibu wa sasa ambao upo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania namna inavyoshiriki katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Zanzibar inashirikishwa kikamilifu kuanzia ngazi ya wataalam, ngazi ya Makatibu Wakuu, ngazi ya Mawaziri na ngazi ya Marais wetu.

Kabla ya kwenda kwenye vikao hivi vya jumuiya kama nchi tunakutana pamoja kuweka msimamo wa nchi, tunashauriana pande mbili Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuweka msimamo wa nchi wa pamoja. Wakati wa mazungumzo waziri yeyote kutoka Zanzibar huwa hakatazwi kuchangia jambo lolote likiwa la Muungano ama lisilo la Muungano na ana haki ile ile ya kutetea maslahi ya Zanzibar kwa msingi wowote utakaojitokeza katika kikao hicho.

Kwa hiyo, mpaka sasa ukitazama utaratibu huu haujatupa matatizo. Lakini kama Waheshimiwa Wajumbe watakuwa na ushauri mwengine wowote basi mimi ushauri wangu tunasimama tungojee mchakato wa Katiba na maoni ya wananchi watuelekeze kuhusu utaratibu huu ambao tunauona baadae.

Lakini kubwa zaidi Mhe. Spika, ni kwamba kila nchi mwanachama inatakiwa ichangie kwa mwaka katika Jumuiya ya Afrika Mashariki karibu dola milioni 8 kwa mwaka. Maana yake tunazungumzia zaidi ya bilioni 10 kwa mwaka za pesa ya Kitanzania. Kwa hiyo, ukitazama ni gharama kubwa kwa wakati huu hasa kwa hali yetu ya kiuchumi tuliyonayo kwa sasa.

Hapa Mhe. Spika, kwetu sisi jambo kubwa Zanzibar ni kujitayarisha namna ya kulichangamkia soko liliopo katika Afrika Mashariki. Kwetu sisi ni kuchukua hatua namna ya kulichangamkia soko hili.

Mhe. Spika, kuhusu Mfuko wa Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, suala hili lilizungumzwa sana na Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Alitaka tuchukue hatua za haraka kuhakikisha kwamba Mfuko wa Baraza la Wawakilishi unakuwepo. Mhe. Spika, hivi sasa wizara yangu kwa kushirikiana na Baraza la Wawakilishi tumo katika

mchakato wa matayarisho wa Sheria ya Utawala ya Baraza la Wawakilishi na mchakato huo unakwenda vizuri.

Mhe. Spika, nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba Baraza lijalo la mwezi wa 10 basi tutahakikisha kwamba tumewasilisha rasimu inayohusiana na Utawala wa Baraza la Wawakilishi. Katika rasimu hiyo tabaan mambo yanayohusiana na mfuko na mambo mengine yatajitokeza kutokana na ushauri utakaotokea katika hatua ya ngazi mbali mbali za mashauriano ndani ya serikali.

Mhe. Spika, kuhusu kuvuja kwa jingo la Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, pia Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imelizungumzia sana jambo hili. Mhe. Spika, hatua zimeanza kuchukuliwa zikiwa ni pamoja kuwasiliana mjenzi wa jengo hili na mjenzi kwa bahati nzuri amechukua hatua ya kuleta wataalam kuja kukagua hali halisi ilivyo na tayari ripoti ya wataalam na mapendekezo yao yamewasilishwa katika Afisi ya Baraza la Wawakilishi. Aidha, tayari wameletwa mafundi kwenye zile sehemu za madirisha ambazo zilikuwa zikivuja wameweka raba ili kuzuia uvujaji kwenye madirisha.

Lakini hata hivyo Mhe. Spika, kama itatokea kwa mjenzi huyu hakuweza kukamilisha mapema inavyotakiwa basi serikali itaingiza mkono wake kuhakikisha kwamba jengo letu hili zuri linakuwa katika hali nzuri na kurekebisha matatizo yaliyojitokeza.

Mhe. Spika, kuhusu jenereta serikali kupitia Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo tayari imeshatoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa jenereta mpya. Tunanunua jenereta yenye *KVA 725,* tatizo hili la kukatika kwa umeme hapa ndani litamalizika.

Tayari asilimia 90 ya fedha zimelipwa ambazo ni sawa na shilingi milioni 302 na fedha zilizobakia ni shilingi milioni 35 ambapo zitalipwa wakati wowote baada ya kuwasili jenereta hili hapa Baraza la Wawakilishi. Mafundi wanaoshughulikia suala hili la jenereta kutoka Kampuni ya *Mantrax?* tayari wamekuja kujenga sehemu ya kuwekea jenereta. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu napenda kuwahakikishia kwamba tatizo la jenereta tuko katika hatua za mwisho kupata ufumbuzi wake.

Kuhusu suala la *hostel* hili lilizungumziwa sana na Mhe. Omar Ali Shehe. Mhe. Spika, kwenye *hostel* tuna mambo mawili, moja ni suala la kiwanja, tunataka kiwanja *hostel* hii isiwe mbali na eneo hili la Baraza la Wawakilishi na wenye kiwanja ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Spika, nataka nichukue fursa hii kumshukuru sana Mhe. Haroun Ali Suleiman wakati

alipokuwa Waziri wa Elimu alitoa *concession* hii ya kutupa kiwanja hichi. Hivi sasa tumemuelekea tena Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban kumuomba sehemu nyengine. Kwa hiyo, mazungumzo yanaendelea kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ili kuongeza nafasi zaidi tuweze kujenga *hostel* yetu.

Pia nataka nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Spika, katika jitihada zake za kutaka kuona *hostel* inajengwa. Alichukua jitihada maalum za kwenda Libya kutuombea msaada wa ujenzi wa *hostel* hii. Lakini ndugu zangu nyote ni mashahidi matokeo ya Libya sasa si rahisi tena kupata msaada huu.

Lakini serikali yetu inaona umuhimu wa kuwa na *hostel*. Kwa hiyo, nia yetu katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais katika mwaka ujao wa 2012/2013 *inshaallah* Mwenyezi Mungu atuweke hai, basi tunaomba kwamba tutaingiza katika miradi yetu ya wizara ili *hostel* hiyo ijengwe katika eneo hili.

Mhe. Spika, vile vile kuna suala ambalo lilizungumziwa kuhusu kazi za kamati kwamba muda hautoshi kwa kamati kufanya kazi zao kwa ufanisi. Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe, sote tunapenda kamati zetu hizi zifanye kazi kwa ufanisi na tija kwa sababu sote ni mashahidi zinatusaidia katika kutekeleza majukumu yetu. Lakini tatizo kubwa ni udogo wa bajeti ambayo tunayo kwenye Afisi yetu hii ya Baraza la Wawakilishi. Lakini naamini katika muundo mpya tunaokuja nao ambapo Baraza litakuwa na uhuru zaidi na litakuwa na mfuko wake ndio litakuwa na uwezo mzuri zaidi wa kujipangia vizuri zaidi kwenye suala hili. Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi tuvute muda wakati tunashughulikia mambo haya ili tuje tufikie hatua iliyo nzuri zaidi huko mbele ya safari.

Mhe. Spika, Mhe. Shawana Bukheti Hassan alizungumzia kuhusu Kitengo cha *Hansard*, akazungumzia kuhusiana na kupatiwa maslahi wafanyakazi wa kitengo hichi kutokana na majukumu yao mengi wanayoyatekeleza hasa katika vipindi hivi vya Baraza.

Mhe. Spika, nataka nikwambie wewe Mhe. Kiongozi wa Baraza letu tukufu na Wajumbe wa Baraza hili kwamba ushauri huu tunaupokea, tuufanyie kazi ili vijana wetu hawa wawe na maslahi mazuri zaidi kuliko yalivyo sasa.

Aidha, Mhe. Abdulla Juma Abdulla alizungumzia kuhusu *CDF*. Mhe. Spika, nia ya kuanzisha *CDF* ipo, mchakato unaendelea, nayo rasimu ya sheria itawasilishwa katika kikao kinachokuja cha Baraza hili tukufu la mwezi wa 10. Kwa sasa serikali imetoa milioni 510 kwa ajili ya kusaidia shughuli za maendeleo katika majimbo yetu.

Mhe. Spika, kuhusu *TASAF* Mhe. Ali Salum Haji kwa niaba ya kamati, Mhe. Raya Suleiman Hamad, Mhe. Abdulla Juma Abdulla na Mhe. Shawana Bukheti Hassan walizungumzia kwa kina suala la *TASAF* na walitaka sana kwamba vikundi vipatiwe utaalam ili viweze kufanya faida katika shughuli zao wanazozianzisha za kiuchumi.

Mhe. Spika, ushauri tunaupokea tutaendelea kushirikiana na vikundi hivi ili tuwapatie wataalam wapate mafunzo hayo waweze kufanya vizuri katika shughuli zao za maendeleo ili kuunga mkono nia ya serikali ya kunyanyua hali za wananchi wake.

Mhe. Spika, katika *TASAF III* malengo makubwa ni kuimarisha kipato cha mwananchi. Kwa hiyo, hapa hatuna shaka yoyote zile shughuli za kiuchumi ambazo wananchi watakuwa wamezielekeza kwenye *TASAF III* tutachukua nafasi kubwa na hata uwezo wa kuwawezesha kimtaji kama walivyotaka Waheshimiwa Wawakilishi, basi naamini hilo litafanyika hapo wakati tutakapofanikiwa kumaliza mazungumzo kuhusiana na mradi wa *TASAF III*.

Kuhusiana na mambo ya maafa. Mhe. Spika, kamati yetu imetutaka kutoa elimu zaidi hasa hasa kwa kuangalia makundi maalum ya wanawake na watoto kwenye suala zima la elimu ya kukabiliana na maafa. Mhe. Spika, sisi tunaamini kabisa kwamba elimu kwa umma itasaidia sana kupunguza matatizo haya ya maafa na kwa msingi huo tunakubali kupokea ushauri huu ili twende tujipange vizuri zaidi tutoe elimu, hasa kwa hawa ambao wanakuwa waathirika wakubwa watoto, wanawake, wazee wasiojiweza na walemavu. Hatua zitachukuliwa ili kuhakikisha kwamba tunazidisha kasi yetu ya kutoa elimu katika shehia ili elimu hiyo iweze kumfikia kila mwananchi aweze kuelewa vizuri suala hili.

Kuhusu kuanzishwa Mfuko wa Maafa. Mhe. Spika, tayari tunayo Sheria ya Kukabiliana na Maafa Nam. 2 iliyotungwa mwaka 2003. Lakini kwa sasa tumo katika mchakato wa kuanzisha Sera ya Maafa. Mara baada ya sera Mhe. Spika, tutaanza matayarisho ya kuanzisha Mfuko wa Maafa. Mfuko huu utakuwa katika ngazi zote kuanzia Shehia, Wilaya na Taifa.

Nia ni kwamba mfuko huu hautochangiwa tu na Serikali Kuu, lakini tutajaribu kufanya kila jitihada kuhamasisha Sekta Binafsi, Jumuiya za Kimataifa, jamii na wafadhili wengine mbali mbali kuchangia mfuko huu kwa sababu una umuhimu sana kwa wananchi wetu hasa pale ambapo wamepata maafa na matatizo makubwa yanawakuta.

Mhe. Spika, ipo mifano mingi kwa hiyo ni jambo la muhimu sana kuwa na mfuko wa maafa ili tusaidie wananchi wetu. Kwa sababu wananchi maskini wanakuwa maskini zaidi baada ya maafa.

Mhe. Spika, kuhusu kupunguza gharama za sherehe, hili lilizungumziwa sana na kamati yetu na baadhi ya wajumbe. Mhe. Spika, kwanza niseme kwamba ushauri tumeupokea. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha Idara Maalum kusimamia suala la Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa. Kazi yake ya kwanza idara hii ni kuandaa muundo utakaosaidia kupunguza hizi gharama wakati wa sherehe.

Hivi sasa tunaandaa muundo ili kwanza kamati yenyewe ya Sherehe na Mapambo iwe ndogo isiwe kama ilivyo sasa ambapo kamati yenyewe inakuwa ni gharama kwa upande mmoja. Kwa hiyo, tutafanya kila njia tuwe na kamati ndogo sekretarieti hii ifanye kazi yake vizuri. Lakini tumo katika kufanya tathmini ya kina kuona namna gani tutapunguza gharama hizi za sherehe na baada ya tathmini hii tutaiwasilisha serikalini ili tupate maoni ya serikali na hapo basi maamuzi ya serikali yatafanyika ili kuona namna gani tutachukua hatua za kupunguza gharama katika sherehe zetu.

Lakini kubwa zaidi hapa ni suala zima la vifaa tunavyonunua kila mwaka wakati wa sherehe. Kwa sasa idara hii itakuwa na dhamana ya kuvisimamia vifaa hivi ili visipotee na wala visiharibiwe na viweze kutumika kwa muda mrefu zaidi. Pale vitakapotumika vitatumika tu kwa ajili ya shughuli maalum au kwa kukodishwa iwe kwa kibiashara ili viweze kuingiza kipato serikalini.

Kuhusu Idara ya Mpiga Chapa Mkuu. Mhe. Spika, jambo hili nalo lilizungumziwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi wa Baraza lako tukufu. Lakini nataka nichukue nafasi hii kuishukuru sana Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa ushauri wao waliotaka zile taasisi zote za serikali zilipe madeni yake kwa Idara ya Mpiga Chapa Mkuu. Kwa upande wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ambayo inadaiwa shilingi 139,000 kuanzia kesho tutafanya jitihada deni hili tulilipe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala jengine lililozungumziwa ni kuimarisha Idara ya Upigaji Chapa. Mhe. Spika, ili kuimarisha Idara ya Upigaji Chapa yapo mambo matatu makuu. Kwanza eneo ambalo hivi sasa Kiwanda cha Upigaji Chapa kipo, sio eneo zuri kwa mazingira ya kazi ile. Kwa hivyo, hatua zinachukuliwa na serikali za kuhamisha kiwanda katika eneo lile na sasa kiwanda tutakipeleka katika majengo yaliyokuwa Kiwanda cha Sigara Maruhubi, pale ndio sasa itakuwa Afisi na shughuli zote za Upigaji Chapa katika jengo lililokuwa Kiwanda cha Sigara Maruhubi. Kwa hivyo, hiyo ni kazi ya kwanza ambayo serikali imeanza kuchukua hatua.

Kazi ya pili, mashine zenyewe yaani vifaa vile vimechakaa sana ni vya zamani haviwezi kufanya wajibu wake vizuri. Serikali inaanza kuchukua hatua hizi, hivi sasa tumo katika mazungumzo na serikali ya Oman ili itusaidie katika kupata mashine na vifaa vipya vya uchapishaji. Mazungumzo yanakwenda vizuri, tumuombe Mwenyezi Mungu tufanikiwe katika hili.

Eneo la tatu ni taaluma kwa wafanyakazi wetu katika kiwanda kile. Uwezo wa wafanyakazi wetu ni mdogo mno. Hatua zinaanza kuchukuliwa kuwasomesha baadhi ya wafanyakazi katika kiwanda kile. Pia tumeshirikiana na Kiwanda cha Uchapishaji cha Tanzania Bara, kutokana na utaalamu wao wasaidie kuwafunza wataalamu wetu wa hapa Zanzibar. Kwa hivyo, hatua zinachukuliwa katika kuleta mabadiliko katika kiwanda kile.

Mhe. Spika, kuhusu matangazo ya TVZ kutosikilikana Pemba. Mhe Raya Suleiman Hamad, alililalamikia sana suala hili. Mhe. Raya Suleiman nataka nikutaarifu kwamba tayari mitambo imenunuliwa na serikali chini ya usimamizi ya wizara inayohusika, na hivi sasa mafundi wanafunga mitambo hiyo. Tuna taarifa kwamba mwishoni mwa mwezi wa Julai tuna tamaa kubwa kuwa TVZ Pemba itafanyakazi na wananchi wa Pemba wataisikia TV yao.

Kuhusu vitendo vya unyanyaswaji, jambo hili amelichangia sana Mhe. Saleh Nassor Juma. Mhe. Spika, kuhusu unyanyasaji wa watoto ambapo hivi karibuni serikali kwa kupitia wizara husika, imepitisha sheria ya haki za watoto nia yake kubwa ni kuwalinda watoto wetu. Tunaamini sheria hii inakidhi haja lakini kubwa hapa ni mashirikiano ili tupambane na wanyanyasaji wa watoto wetu. Jambo hili ni baya na linazungumziwa sana, sasa hatua kali zitachukuliwa ili kupambana na watu wote wenye vitendo hivi vibaya.

Mhe. Spika, Mhe. Rashid Seif alizungumzia sana suala la uratibu katika shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ni kweli tatizo tunalo Mhe. Spika, hivi sasa Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais katika mwaka huu wa fedha wa 2011/2012 tumeandaa mipango maalum ya kutathmini uwezo wa watendaji wetu wa serikali na kujua mapungufu yaliopo na kupanga mikakati ya kuweza kujenga uwezo kwa ajili ya watendaji wetu, ili suala la uratibu liweze kufanya kazi zake vizuri na mashirikiano yawepo mazuri.

Napenda nitoe wito Mhe. Spika, kwa kuptia Baraza lako hili tukufu kwamba mashirikiano ni kitu muhimu, mashirikiano ya wizara kwa wizara, mashirikiano ya idara kwa idara na mashirikiano ya wafanyakazi, bila ya mashirikiano Mhe. Spika, hakuna maendeleo.

Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan Hija alielezea kuhusu utekelezaji wa maamuzi ya vikao, na Mhe. Hija Hassan alieleza kwamba hata baadhi ya maelezo yetu

ya taarifa katika hotuba yetu yamedanganya. Nataka nimuhakikishie Mhe. Hija Hassan kwamba maelezo yaliyotolewa ni sahihi, vitabu vyetu, vikao vilikaa, kumbukumbu ziko na maamuzi yakafanyika. *TRA* wenyewe walitangaza rasmi kwa kupitia kwa Kamishna Mkuu, kwamba suala la kulipa kodi mara mbili halipo.

Kama ikitokea mfanyakazi yeyote wa *TRA* atamlipisha kodi mfanyabiashara mara mbili, basi hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya mfanyakazi yule, ikiwemo kufukuzwa kazi. Kwa hivyo, ninachokuomba Mhe. Hija Hassan na waheshimiwa wengine wote, wenye vielelezo vya kwamba watu wetu wanatozwa kodi mara mbili, basi naomba mnipe vielelezo hivyo tutashirikiana na waziri anayesimamia mambo ya fedha ili tuhakikishe kwamba watu wetu hawatozwi kodi mara mbili. Kama yuko aliyelipa kodi kihalali basi Mhe. Spika, tupeni vielelezo ili tulishughulikie tatizo hili ili tuweze kulikomesha.

Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan alisema kwamba ni bora tuwache kabisa kuzungumza, maana mazungumzo yenyewe hayana faida. Mhe. Spika, mazungumzo yana faida, yako mambo mengi yaliyopatiwa ufumbuzi, yakiwemo kwanza tumeweza kupata fedha zinazotokana kwenye msamaha wa madeni, tumepata zaidi ya dola 155 ambazo zimetumika katika kununulia zana za kilimo, zimetumika kununulia vifaa vya Hospitali ya Mnazi Mmoja na vile vile zimetumika katika kununulia magari ya serikali.

Vile vile Mhe. Spika, katika mazungumzo haya tumefanikiwa kuweza kupata asilimia 4.5 kwenye mikopo na misaada kutoka nje. Pia tumeweza kupata asilimia 4.5 kwenye bajeti za kodi, tumepata pia mapato yanayotokana na mgao wa uvuvi wa bahari kuu. Vile vile tunapata fursa ya masomo ya elimu ya juu zinazogharimiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, mazungumzo yana faida, cha msingi hapa yale tunayoamua utekelezaji wake ufanyike. Nataka nikuhakikishie Mhe. Hija Hassan kwamba tutachukua kila hatua ili kuhakikisha kwamba utekelezaji unafanikiwa.

Mhe. Spika, mwisho nimalizie suala la uwajibikaji. Kwa ulimwengu ulivyo leo wimbi la mabadiliko liliopo ulimwenguni ni kubwa, hivyo hatusubiri hata kidogo kungojea kukumbwa na wimbi kama hili, maana ‘usipoyaongoza mabadiliko basi mabadiliko yatakuongoza wewe’. Kwa hivyo, ni lazima tubadilike kwa kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na nidhamu ili tuweze kuwatumikia wananchi wetu vizuri zaidi.

Mfano mzuri ni wa Rais wetu, ni mchapa kazi hodari, muadilifu na ana nidhamu ya hali ya juu. Naweza kusema ni mfano wa Marais sio wa Afrika tu

ni ulimwengu mzima. Kwa hivyo, Mhe. Spika, suala la uwajibikaji serikali yetu italichukulia kila jitihada ili kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda vizuri.

Mhe. Spika, naomba niseme la mwisho kabisa, kwamba ushauri wote walioutoa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu tunaupokea, maelezo yenu tutakwenda kuyafanyia kazi. Tunalowaomba Waheshimiwa Wajumbe mtuunge mkono, bila ya buti, hii ni bajeti yetu ya mwanzo. Baada ya kusema hayo naunga mkono hoja Mhe. Spika, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema amani, utulivu katika nchi yetu. Pili natoa shukrani zangu za dhati kwako Mhe. Spika, kwa kuiongoza mijadala ya wajumbe wa Baraza lako tukufu katika kuichangia hotuba yangu ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, pia sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa michango yao waliyoitoa kwa njia ya kuuliza maswali, kutoa maoni au kuhoji. Naamini wajumbe wote hawa lengo lao ni moja tu, nalo ni kuitakia afisi yangu mafanikio makubwa wakati wa utekelezaji wa bajeti yake. *(Makofi).*

Waswahili wanasema Mhe. Spika, “kinga na kinga moto huwaka”. Kutokana na michango yenu mbali mbali Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu, mlioitoa kwetu basi tutahakikisha moto unawaka kweli lakini bila ya kuungaza chakula wakati wa utekelezaji wa bajeti yetu utakapowadia. Vile vile napenda kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, kwa kutoa ufafanuzi wa mambo mbali mbali yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe.

Pia niwashukuru watendaji wangu wote wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, akiwemo Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Afisi Mdhamini na watumishi wote kwa kunisaidia katika shughuli zangu za kila siku, nawaambia nawashukuru sana.

Mhe. Spika, naomba kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kwa kuiunga mkono hotuba yangu na kwa kupitia kwake nawashukuru wajumbe wote wa kamati hii. Vile vile nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri waliochangia kwa kuzungumza na waliochangia kwa maandishi. Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza, waliopata wasaa wa kuchangia bajeti yetu ambao wamefikia 36 na hata wale waliokuwa hawakupata fursa ya kuchangia, lakini waliochangia miongoni mwao wote nawashukuru kwa kuunga mkono hotuba hii.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wawakilishi wengi wamechangia hotuba hii kwa lengo lile lile la kutuonesha njia ili tufanye kazi zetu kwa umakini zaidi. Kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba niwatambue waliochangia kwa kutoa maelezo, kuuliza maswali na waliochangia kwa maandishi kama hawa wafuatao. Kwanza kabisa ni:

1. Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa)
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu.
4. Mhe. Asha Bakar Makame.
5. Mhe. Shawana Bukheti Hassan.
6. Mhe. Omar Ali Shehe.
7. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
8. Mhe. Rashid Seif Hamad
9. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
10. Mhe. Ashura Sharif Ali
11. Mhe. Saleh Nassor Juma
12. Mhe. Kazija Khamis Kona
13. Mhe. Raya Suleiman Hamad
14. Mhe. Subeit Khamis Faki
15. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
16. Mhe. Hija Hassan Hija
17. Mhe. Ussi Jecha Simai
18. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
19. Mhe. Rufai Said Rufai
20. Mhe. Assa Othman Hamad
21. Mhe. Naibu Waziri wa Afya.
22. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.
23. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.
24. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika
25. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na
26. Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, waliochangia kwa maandishi ni:

1. Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.
2. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman.
3. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak.
4. Mhe. Mussa Khamis Silima.
5. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.
6. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma.

7. Mhe. Suleiman Hemed Khamis.
8. Mhe. Mohammed Said Mohammed.
9. Mhe Mohammed Mbwana Hamad na
10. Mhe. Mgeni Hassan Juma.

Mhe. Spika, wote waliochangia nawashukuru sana.

Mhe. Spika, Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, ametoa ufafanuzi wa kina wa hoja mbali mbali kwa hoja za wajumbe wa Baraza lako tukufu. Kwa upande wangu nitatoa ufafanuzi wa jumla kwa baadhi ya hoja zilizotolewa na wajumbe ambao nimehisi zinahitaji maelezo zaidi kutokana na uzito wake.

Mhe. Spika, kwanza rushwa. Kuhusu suala la rushwa bado ni tatizo katika nchi yetu, kama Waheshimiwa Wawakilishi walivyosema. Suala la rushwa limekaa katika nchi yetu kwa muda mrefu na sasa limeota mizizi. Mhe. Spika, sote ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba suala la rushwa tunalitokomeza nchini kwetu, kwa sababu suala la rushwa litatuathiri sote. Katika nchi yetu sasa hakuna mwahala tutakapokwenda kupata huduma bila ya kuambiwa kitu kidogo.

Sisi sote hapa tuna wajibu kama viongozi wa kuhakikisha kwamba tunalipiga vita suala la rushwa. Kuanzia mawaziri hadi watendaji wote serikalini. Kwa sababu watoa rushwa na wapokeaji rushwa wamo miongoni mwetu. *(Makofi).*

Sasa tunaambiwa tusitoe wala tusipokee rushwa, wote hawa ni wakosa. Kwa hivyo, mimi nawasihi sana mawaziri na watendaji wakuu waangalie maofisini kwao vitendo hivi havifanyiki vya rushwa. Nikipata taarifa mtendaji yeyote anajaribu kupokea rushwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa mtu ambaye anastahiki ampe huduma, basi tutamchukulia hatua ikiwa ni pamoja na kumfukuza kazi. *(Makofi).*

Kwa sababu naamini kama hatukufanya hivi, basi rushwa haiondoki na itabidi tutoe mafunzo ya kufukuzwa watu kazi kwa suala la kupokea rushwa katika sehemu zozote zile, maana suala hili limeenea sana. Limezungumzwa humu kuwa hakuna pahala utakapokwenda ukapata haki yako ya huduma ile bila ya kutoa kitu chochote haiwezekani. Kwa hivyo, nawasihi sana, kila mmoja wetu aiangalie afisi yake vizuri na awaangalie watendaji wake wasijiingize katika upokeaji wa rushwa. Kila Mzanzibari ana haki ya kupata huduma bure, hakuna Mzanzibari yeyote atakayetakiwa kulipia huduma ambayo anastahiki aipate bure. Hivyo, hili ni jukumu letu sote na lazima tulivalie njuga ili kuhakikisha kwamba tunalitokomeza nchini mwetu. *(Makofi).*

Mhe. Spika, sekta ya utalii nayo imezungumzwa kama ilivyoelezwa. Sekta ya utalii ni moja ya sekta muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wetu. Sekta ya utalii tumeiingiza kwa sababu ya kuporomoka kwa bei ya karafuu, zao ambalo tulikuwa tunalitumia sana kwa ajili ya kukuza uchumi wetu. Sekta ya utalii ni muhimu na lazima tuifanyie kila hali ili iweze kukua.

Namshukuru sana Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Mhe. Abdillah Jihad Hassan pamoja na Naibu Waziri wake juu ya maelezo ya kina juu ya namna serikali yetu ilivyojiandaa katika kukuza utalii nchini.

Mhe. Spika, katika kulishughulikia tatizo la ajira kwa vijana wetu, kwa sababu moja ya mambo ambayo tunayapigania kuleta vitega uchumi hapa, ni kwa sababu vijana wetu waweze kuajiriwa katika vitega uchumi hivi ambavyo tunavialika kutoka nje. Moja kati ya sekta muhimu ni hii ya utalii ambayo tunaamini inaweza kuwaajiri vijana wetu wengi zaidi. Nafikiri tuna vikwazo kwa sheria yetu ya uwekezaji.

Sasa Mhe. Spika, katika kulishughulikia tatizo hili la ajira kwa vijana wetu wa Kizanzibari kupitia sekta ya utalii naziagiza Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, *ZIPA*, Wizara ya Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika na Idara ya Uhamiaji wakutane chini ya afisi yangu, kuona ni jinsi gani tunaweza kuzifanyia mapitio sheria zetu za uwekezaji ili kukuza fursa za ajira kwa vijana wetu.

Sheria kama zilivyo hivi sasa hazitusaidii. Mimi nimeshakwenda kwenye baadhi ya mahoteli, utakuta zaidi ya asilimia 90 ya wafanyakazi mule ndani ni kutoka nje ya Zanzibar. Jana nilimdokeza kitu pale Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, hoteli fulani ambayo kazi yake kila wakati inakwenda kwa wenzetu kule kwenda kufanya uajiri wakati hapa Zanzibar wapo vijana wetu, tumewasomesha, tunacho Chuo cha Utalii lakini hawaonekani, wanaonekana wenzetu wa kutoka Tanzania Bara.

Hatukatai wenzetu wa Tanzania Bara wasiajiriwe lakini basi pawe na uwiano, ‘sadaka huanzia nyumbani’. Kwa hivyo, na sisi tunasema ni lazima tuziangalie sheria zetu kwa wawekezaji wetu ili kuhakikisha kwamba wanapoanzisha miradi yao hapa Zanzibar, basi ni lazima ajira kwa vijana wetu iwepo.

Kwa hivyo, naomba sana Waheshimiwa Mawaziri niliowataja tukutane ili kuangalia sheria zetu namna gani tunaweza kuzifanyia mapitio na kuzibadilisha, ili kuwanufaisha vijana wetu kuweza kupata ajira katika hivi vitega uchumi vinavyokuja Tanzania Zanzibar.

Mhe. Spika, katika sekta ya kilimo, serikali ya awamu ya saba inatilia mkazo kilimo na hasa kilimo cha umwagiliaji maji. Hii itasaidia kupunguza tatizo la upungufu wa chakula kwa wananchi wetu na kupunguza mfumko wa bei hapa nchini. Serikali kwa kushirikiana na nchi marafiki na washirika wa maendeleo, tumepanga kulifanyia kazi kwa kiwango kikubwa suala hili kwa kuimarisha miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji maji, kuzalisha mbegu bora na kuongeza vifaa hasa matrekta yatakayotumika katika kilimo cha umwagiliaji maji hasa kwa kilimo cha mpunga.

Aidha, serikali inakusudia kuimarisha kituo cha utafiti na mafunzo ya kilimo Kizimbani na Matangatuani kule Pemba, kwa lengo la kutoa mbegu bora na teknolojia bora za uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Vile vile serikali itahakikisha wataalamu wa kilimo wanawekwa vijijini ili kuwasaidia wakulima na wafugaji wetu kwa kuwapatia taaluma ya kisasa ya uzalishaji. Hatuwezi kuwaachia wataalamu wetu wa kilimo wakae maofisini, kazi zao wale sio ofisini. Kazi zao ni mashambani kutoa taaluma kwa wakulima wetu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili atusaidie katika kazi hiyo ili wataalamu wake waende mashambani kwenda kuwaelimisha wakulima wetu.

Mhe. Spika, mkazo pia utawekwa katika uimarishaji wa zao la karafuu, zao la nazi, mazao ya viungo na zao la mwani. Bei ya zao la karafuu itaimarishwa ili kutoa kivutio kwa wakulima kutunza mashamba yao na kupanda miche mipya. Nimelitaja zao la mwani kumbe sikujua kama ni zao muhimu sana, mpaka juzi nilipofanya ziara ya Paje.

Paje kuna kikundi cha akinamama kule wamejikusanya wanapata msaada wa mafunzo kutoka kwa washirika fulani wa nje, Sweden nafikiri. Pale mwani huu wanatengeneza sabuni, mwani huu unatengenezwa vileja, mwani huu unatengenezwa *juice*. Sasa naambiwa bei ya mwani kwa kule Paje imepanda. Wanashindana wanunuzi wa mwani kwa sababu tunacho kiwanda cha kusarifu mwani.

Namshukuru Mhe. Mwakilishi kutoka nafikiri Micheweni Viti Maalum, alisema kule Micheweni nako tupeleke taaluma hiyo. Sasa mimi nafikiri Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika yupo na anasikia, tuipeleke taaluma hiyo Micheweni ili wananchi wetu kule waweze nao kupata matumizi bora ya mwani na kujizidisha fedha kwa ajili ya kuendeleza maisha yao.

Mhe. Spika, nidhamu na uwajibikaji. Hili nalo limekuwa ni gumzo ndani ya Baraza lako Mhe. Spika, wengi wamezungumza sana juu ya uwajibikaji wa

watendaji wetu katika maofisi yetu. Ni kweli, hali ya nidhamu katika maofisi yetu imeshuka sana. Watendaji wanaingia maofisini saa wanayotaka, wanatoka saa wanayotaka na siku nyengine hawaji kabisa. Lakini hili ni jukumu la Waheshimiwa Mawaziri kusimamia ofisi zao. Mawaziri ni lazima wasimamie ofisi zao kuhakikisha kwamba nidhamu ndani ya afisi yake inaimarika.

Kwa hivyo, nawaagiza mawaziri wote kuifanya hiyo kazi. Tunayo sheria ya Utumishi wa Umma, mtendaji yeyote ambaye hataki kufuata sheria za utumishi, ikiwa ni pamoja na kuingia afisini mapema kama saa ilivyowekwa, kukaa afisini kwa muda wote ambao anatakiwa awepo afisini. Sasa tutatumia sheria ya Utumishi wa Umma kumuadhibu na sheria imeweka wazi atapewa onyo, ataandikiwa barua mara ya kwanza, mara ya pili na mara ya tatu au sio waheshimiwa. Sasa kama kashindwa, basi tutakuwa hatuna budi, itabidi tumsamehe.

Mhe. Rais ameshatuambia kama kuna mtu anaona hawezi kufanya kazi, kama ni uteuzi wa Rais aende tu akamwambie Mhe. Rais umeniweka hapa lakini aah! Naona sipawezi, naomba nipumzike, atakupumzisha tu, usingoje upumzishwe kwa sasabu hiyo itakuwa ni aibu. Kwa hivyo, tunawaomba Mawaziri wasimamie ofisi zao, pamoja na Waziri wangu wa Nchi Afisi ya Mamamo wa Pili wa Rais hakikisha kwamba ofisi yetu nidhamu inaimarika, tukishirikiana na Makatibu Wakuu wetu.

Lakini hatuwezi kuimarisha nidhamu kama sisi wenyewe mawaziri hatukuifuata hiyo nidhamu. Kwa sababu hao watendaji wetu wanaiga, anajua waziri haingii afisini mpaka saa 3:00 na yeye anakuja saa 2:00 au saa 2:30. Kwa hivyo, sisi wenyewe mawaziri tujihimu kwenda maofisini mapema, isipokuwa kama unadharura maalum. Kama na wewe Waziri unazoea kuingia afisini saa 3:00 au saa 4:00 unajua mimi ni waziri au mimi Katibu Mkuu, basi na wafanyakazi wa chini nao wanafanya hivyo hivyo, wanasema aah! Waziri mwenyewe anaingia saa 4:00 au saa 3:00, kwa hivyo wanaiga. Kwa hivyo, mawaziri na sisi tujihimu.

Mimi nimechelewa sana basi naingia afisini kwangu saa 2:00. Kuna utaratibu ni lazima uanzishwe afisini kwangu wa kuweka kumbukumbu, kwamba afisa yeyote anaingia katika wizara anaandika jina lake na saa aliyoingia. Ingawa haitosaidia sana lakini kama usimamizi mzuri utakuwepo basi utasaidia.

Maana yake tutajua nani kaingia saa 2:00 na nani kaingia saa 3:00 na nani kaingia saa 4:00 au nani hakuja kabisa. Afisa muhusika ndani ya afisi ile ataweza kuchukua hatua zinazostahiki. Kwa hivyo, mimi nafikiri ni vyema Waheshimiwa Mawaziri tukachukua hatua hizo ili kuhakikisha kwamba nidhamu zinarudi serikalini.

Lakini Mhe. Spika, na wewe pia nakuomba utusimamie. Hapa tumezungumza sana na wewe mwenyewe juzi ulisema kwamba kama ni uimarishaji wa nidhamu basi ianze na humu ndani ya Baraza pia. Humu tunaanza Baraza saa 3:00 basi Mhe. Spika, na wewe utusimamie tuingie humu Barazani saa 3:00 na tusitoke toke. Tunapata *sitting allowance* kwa sababu ya kazi hii ya kukaa humu ndani.

Sasa kama tunapata *sitting allowance* kwa kukaa humu ndani ya Baraza basi tukae. Kuanzia saa 3:00 mpaka saa 7:00 na saa 11:00 mpaka saa 1:45. Kwa hivyo, tuianzie humu ndani Mhe. Spika, isiwe wenzetu wanatusema serikalini, lakini sisi humu hatufuati. Mimi nahisi na sisi humu ndani ya Baraza tujirekebishe. Najua Mhe. Spika, hilo utaliweza la kuturekebisha.

Mhe. Spika, tatizo la Baraza la Manispaa. Ni kweli katika kikao kilichopita, niliahidi kuunda tume ya serikali kuchunguza mambo yaliotokea katika Baraza la Manispaa. Lakini kabla sijaunda tume hiyo, Baraza la Madiwani nalo likaunda tume, likafanya uchunguzi wa kina na ripoti mimi ninayo.

Mhe. Spika, unajua mgonjwa akienda kwa daktari akipata mawazo ya daktari mmoja basi anatafuta na mawazo ya daktari mwengine, tukasema na sisi serikali tuunde tume. Tumeunda tume na inafanya kazi hivi sasa. Ilikuwa wamalize kazi hii tarehe 20, bahati mbaya kwa sababu ya haya mambo ya bajeti imekuwa haikuwezekana wameomba wapatiwe wiki moja zaidi.

Baada ya wiki moja ripoti yao itatoka, tutalinganisha na ile ya Baraza la Madiwani na baada ya hapo taarifa zote hizi zitafikishwa Barazani, yale yanayotuhusu serikalini basi tutachukua hatua za kiserikali na kama yanawahusu Manispaa huko basi Meya atachukua hatua zinazomuhusu. Kwa hivyo, bado hili zoezi linaendelea na hatukulipuuza. Ningemsihi sana Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kitope astahamili hili jambo tunalishughulikia.

Mhe. Spika, suala la muungano. Tumezisikia hoja za Waheshimiwa Wajumbe kuhusu kero za muungano na muundo wa muungano wetu uliopo hivi sasa. Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais amelielezea hili kwa kina. Ninachosema, muungano huu ni wetu ni muungano wa Zanzibar pamoja na Tanganyika. Muundo gani tunautaka kwa muungano huu ni sisi ndio wa kuamua. Hivi sasa muundo wa muungano wetu ni wa serikali mbili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Sasa kama tunafikiria muundo huu unatuletea matatizo, Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais ametuambia kwamba tungojee Katiba mpya inayokuja ili tutoe maoni yetu, wala sio baada ya muda mrefu. Hivi sasa mswada wa kuunda tume hii ya kukusanya maoni karibu itakamilika. Tukiitwa kwenye maoni tutoe

maoni yetu, muundo wa serikali ya muungano wetu uweje. Hapo na wenzetu kule vile vile nao watatoa maoni yao, baada ya hapo sote tutapata kitu kizuri ambacho kitaweza kutupeleka mbele na muungano wetu utaweza kutufaidisha kwa pande zote mbili za muungano. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe mimi ningefikiri tungojee ili tuweze kutoa maoni yetu kwenye Katiba inayokuja kwa uhuru, kwa uwazi na kwa mujibu wa maoni yako unavyoona kuwa muungano huu vile vile unazo kero zake. Kwa kweli kero hizi nakuhakikishia Mhe. Spika, pamoja na Baraza lako tukufu kwa jumla, kwamba tunazishughulikia kwa dhati. *(Makofi)*

Mhe. Spika, haya yote waliyoyazungumza Waheshimiwa Wajumbe ni kweli yapo, lakini tunayashughulikia na wala hatukukaa na kunyamaza bure, hapana. Kwa kweli tunayashughulikia na tutaendelea kuyashughulikia na kuhakikisha yale tunayoyaamua hayarudiwe, kwa sababu hatuwezi kufuta kero hii na kesho inarudiwa tena na tunaanza kuizungumza upya hivyo hatuwezi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Spika napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba suala la kero zote za Muungano tunazishughulikia pamoja na hili la wafanyabiashara wetu kutozwa kodi au ushuru mara mbili. *(Makofi)*

Kwa kweli suala hili limeelezwa kwa kina na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na tunaendelea kulifuatilia kama kweli hili linafanyika, basi tutazidi kuongea na *TRA* kuhakikisha kwamba hili halifanyiki, kwa sababu ndivyo tulivyokubaliana. Mhe. Spika, tayari tumeshakubaliana na tutahakikishi kwamba tumekubaliana ina maana halirudiwi tena suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala la kujiunga na *OIC*. Kweli nakumbuka nafikiri ilikuwa ni miaka ya 1990 Zanzibar ilijiunga na *OIC*, lakini iliambiwa ijitoe kwa sababu ilikuwa inakwenda kinyume na Katiba. Sasa katika mazungumzo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikasema ni vyema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ijiunge, ili Zanzibar iweze kunufaika. Kwa bahati mbaya mpaka leo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bado haijajiunga na *OIC*.

Wakati nilipokuwa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje nilikuwa nalifuatilia sana hili na tukafikia wakati suala hili kulizungumza Bungeni, kwamba sasa Tanzania lazima ijiunge na *OIC*. Mhe. Spika, kwa sababu wenzetu Uganda ni wanachama wa *OIC* nafikiri na hata Rwanda, Msumbiji nchi zote hizi ni wanachama wa *OIC*. *(Makofi)*

Sasa nafikiri wenzetu Tanzania Bara hili jina linawaogopesha *Organization of Islamic Conference* ndilo linalowaogopesha, mpaka bajeti ya juzi mwaka

2010/2011 tulilizungumza tena kwamba Tanzania lazima ijiunge na OIC, ili kutoa nafasi kwa Zanzibar na wao kunufaika. Lakini taarifa tulizonazo ni kwamba kumbe waombaji wa uwanachama wa *OIC* wako wengi pamoja na mataifa makubwa.

Sasa uongozi wa *OIC* umeshtuka na umesitisha na kupokea wanachama wapya na hivi sasa wanaifanyia *review* Katiba yao, ili kuona sasa utaratibu wa kuingiza wanachama uwe vipi *qualification* zao ziwe vipi na utaratibu huu wa *reform* hii naambiwa utamalizika mwaka 2012. Mhe. Spika, jambo la msingi nadhani ni vyema kusubiri mpaka mwaka 2012 tuone hiyo *reform* na *qualification* za nchi zipi zinaweza kuwa mwanachama wa *OIC* tutakapozijua pamoja na masharti yao.

Mhe. Spika, suala hili bado tunalo kama nilivyosema na wala hatukukaa bure tumekuwa tukilizungumza na tumelifikisha mpaka Bungeni kwamba Zanzibar ijiunge na *OIC*. Lakini hali tuliyonayo hivi sasa ni hiyo kwamba *OIC* imesitisha kupokea wanachama wapya na tusubiri mpaka hapo watakapomaliza *reform* yao, ili tujue hizo *conditions* mpya ziko vipi na baada ya hapo tutaendeleza mchakato. Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe kwamba tusubiri suala hili mpaka hapo mwaka 2012 tutakapojua hasa *reform* hiyo iko vipi ya *OIC*. *(Makofi)*

Kuhusu suala la uchimbaji wa mafuta. Mhe. Spika, suala hili kwa kweli limejadiliwa sana katika serikali za awamu mbali mbali zilizopita. Kwa hiyo, kama Waheshimiwa Wajumbe mnavyoelewa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekubaliana na matakwa ya Waheshimiwa Wawakilishi mwaka 2009 ya kuliondoa suala la mafuta katika orodha ya mambo ya Muungano. *(Makofi)*

Mhe. Spika, uamuzi huo tayari umekwishapitishwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini lazima tufuate taratibu, yaani uamuzi tayari tokea mwaka 2009 na mpaka leo tunayazungumza haya kwenye Baraza la Mapinduzi, lakini kulitoa suala la mafuta kwenye Orodha ya Mambo ya Muungano lazima tufuate taratibu. Kwa hivyo, hivi sasa tunazungumza na wenzetu Tanzania Bara na wala hili sio sehemu ya kero za Muungano, yaani halimo kwenye kero za Muungano na hili linazungumzwa na Viongozi Wakuu, mimi naongea na Waziri Mkuu na baada ya hapo nafikiri Waheshimiwa Marais wetu watalizungumza hili kwa ajili ya kulipatia ufumbuzi.

Suala hili tunalishughulikia na vyema tuwe na subira tukifanya vyengine vyovyote tutaonekana sisi wababe na wala sio jambo zuri kwa serikali hii ambayo inao Uongozi wa Utawala Bora na Sheria tukaanza mambo ambayo wenzetu wasituelewe. Kwa kuwa tunalishughulikia basi tusubiri hatima ya

kulishughulikia suala hili. Lakini taarifa ya kina anaweza kuja kuitoa Mhe. Mhe. Wazira wa Ardhi, Maakizi, Maji na Nishati ambaye atalieleza vizuri zaidi.

Mhe. Spika, kuhusu migogoro ya ardhi. Kwa kweli kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu, kwamba chanzo kikubwa cha migogoro ya ardhi ni kutokuwa na usimamizi mzuri wa matumizi ya ardhi pamoja na baadhi ya viongozi kujiingia kwenye matatizo hayo. Katika kulidhibiti tatizo hili serikali imo katika hatua za kuweka mikakati madhubuti, itakayoziba mianya yote ya watu porora ardhi na kujikatia maeneo ya ardhi bila ya kufuata taratibu za kisheria. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nawaomba viongozi wote katika ngazi zote watendaji na wananchi kwa ujumla kuacha kujiingia kwenye matatizo ya ardhi. Mhe. Spika, narudia kusema kwamba serikali haitasita kuchukua hatua zozote zile ambazo itaona inafaa kwa wale wanaojiingiza kwenye migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakusudia kumshauri Mhe. Rais wa Zanzibar aunde Tume ya Kuchunguza Viini hivi vya Migogoro ya Ardhi, kwa sababu limekuwa tatizo kubwa ambalo linahatarisha hata maisha wa watu wetu wenyewe. Kwa mfano, kuna Mhe. Mjumbe mmoja hapa aliniambia kwamba sehemu za Matemwe, Pwanimchangani, Mtende na hata kule kwangu Kiwengwa ndio balaa tupu, yaani sehemu zote hizi kuna matatizo ya ardhi. Kwa hivyo, haya ni vyema kuyatafutia ufumbuzi.

Kwa kweli nilipoanza kushughulikia mambo ya ardhi kuna watu walianza kusema siku hizi nimekuwa poa nguvu ya soda. Lakini nawahakikishia kwamba sijapoa isipokuwa tumebadilisha *style* tu. Mhe. Spika, kama Mhe. Rais wa Zanzibar alivyoelekeza kuwa mambo ya ardhi, yaani wanaoanzisha migogoro ya ardhi ndio hao waimalize migogoro hii. Kutokana na hali hiyo, hivi sasa kwanza tunawaangalia Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuona kwamba wanaimaliza migogoro hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, watakaposhindwa tutawauliza wameshindwa vipi na wala huwezi kushindwa kutatua mgogoro wa ardhi kama wewe mwenyewe huhusiki. Kwa kweli ukihusika na mgogoro wa ardhi huwezi kuutatua mgogoro huo, kwa hiyo tutamuuliza mwenzetu vipi kwa nini umeshindwa na tukimgundua kuwa na yeye anahusika na mgogoro huo basi na yeye tutamchukulia hatua. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kama alivyosema Mhe. Rais wa Zanzibar huwezi kuanzisha mgogoro huo na baadaye ukuupandisha kwa viongozi wa juu, isipokuwa ni vyema kuumaliza mwenyewe. Kwa maana hiyo, ni sawa na mtoto wako ameanza ugonvi nje na baadaye anakimbilia ndani, basi wewe umwambie urudi nje na kama umeanza ugonvi wa kupigana nenda kapigane tu, sasa unakimbilia

ndani tukufanye nini sisi. Kwa hiyo, wanaoanzisha migogoro hii ni wao wenyewe ndio watakaoimaliza na akishindwa kuimaliza, basi tutamuuliza wapi na kwa nini. Hivyo tukigundua ikiwa anahusika na migogoro hiyo, basi na sisi tutamshughulikia ipasavyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kumalizia nachukua fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, naamini majibu yake yameridhisha na hivyo Waheshimiwa Wajumbe wataendelea kutuunga mkono kwa mpango wa utekelezaji wa mwaka ujao wa fedha 2011/2012. *(Makofi)*

Kwa mara nyengine nakushukuru wewe Mhe. Spika, kwa jinsi ulivyosimamia mijadala ya Waheshimiwa Wajumbe katika hotuba yetu. Vile vile namshukuru pamoja na kumpongeza Mhe. Mgeni Hassan Juma (Mwenyekiti wa Baraza la Wawawakilishi) kwa kuendesha vizuri kikao chetu wakati wa leo asubuhi, ambapo alifanyakazi nzuri ambayo inastahili kupongezwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa michango yao ambayo yote tunaithamini sana na tutaifanyiakazi bila ya kuchelewa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba watuunge mkono katika bajeti yetu hii, ili tuweze kuipitisha vizuri kwa ajili ya kuanza kufanyakazi vizuri. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nategemea Mhe.Ismail Jussa Ladhu ambaye ni rafiki yangu hatoitoa shilingi na kuwaacha ndugu zake kule nyumba wakafa na njaa. Kwa maana hiyo, namshukuru sana kwa kutuelewa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa heshima na taadhima sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, pia nakushukuruni Waheshimiwa Wajumbe pamoja na Mawaziri wote. Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa. Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha mwaka 2011/2012 wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi, ili kupitisha vifungu vya matumizi vya wizara yetu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 05 – OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Kifungu 03 – Afisi Kuu Pemba

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba muongozo kabla ya kuingia kwenye vifungu kwamba kwa kawaida tumezoea kwa mtiririko wa vitabu vya matumizi vinakuwa na mtiririko maalum unaowezesha kuhoji kwa mfano kama jambo la sera pale mwanzo kabisa. Sasa kwa mtiririko wa vitabu wa mara hii ulivyopangwa ni tofauti.

Kwa hivyo, nahitaji muongozo wake pale ambapo tunahitaji maelekezo au ufafanuzi wa sera tuzuie fungu gani baina ya Idara ya Utawala na Uendeshaji na Idara ya Mipango Sera na Utafiti. Mhe. Mwenyekiti, naomba muongozo wako.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri kama tulivyokuwa tumeelekezana mapema kwamba kitabu hiki mara hii kimebadilika kidogo na wala haliko kwenye ule utaratibu wa kawaida. Lakini kwa kuwa eneo hilo la Idara ya Mipango, Sera na Utafiti lipo, basi tutakapofikia eneo hilo kama unalo jambo linalohusu hapo basi utasimama na utaelekeza hiyo hoja yako hapo. Kwa hivyo, tuendelee.

Kifungu 03 – Afisi Kuu Pemba 267, 980,000/=
Kifungu 04 – Idara ya Mipango Sera na Utafiti

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia mjadala huu nilieleza nia yangu ya kutaka kupatiwa maelezo zaidi kuhusu suala hili. Kwa kweli nimeyasikiliza kwa kina majibu yaliyotolewa hapa na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kuna maeneo ambayo nimeridhika nayo, isipokuwa kuna maeneo mawili nahitaji ufafanuzi. Kwanza ni suala zima linalohusu uwanachama au ushiriki wa Zanzibar katika Jumuia ya Afrika ya Mashariki.

Katika maeleo ya Mhe. Waziri alitoa hoja kadhaa kuhusiana na suala hili, lakini nimeliibua katika suala hili na wala sio katika Ofisi ya Rais, kwa sababu kwenye kipindi cha Maswali na Majibu tarehe 20 Juni, 2011, yaani kikao hiki kinachoendelea, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alitutajia maeneo yanashughulikia ambayo aliyataja kama ni matatizo au kero za Muungano na moja alilitaja ni ushiriki wa Zanzibar katika Jumuia ya Afrika Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, nimeyasikia majibu, isipokuwa naomba maelezo zaidi, kwa sababu hoja zake alizozitoa ni kwamba suala hili lina maeneo mengi na moja wapo linahusu mambo ya Muungano.

Sasa kwenye hoja yangu nilisema Mhe. Mwenyekiti, kwamba unapouangalia mkataba wa Jumuia ya Afrika ya Mashariki unazungumzia maeneo kumi na saba ya ushirikiano ya ushirikiano, ambapo kimsingi wake ndio maeneo ya Afrika Mashariki. Kwa hivyo, kwenye maeneo yale kumi na saba manne tu ndio mambo ya Muungano, tunapoangalia Orodha ya Mambo ya Muungano iliomo ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, nyongeza ya kwanza iliomo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano ukurasa wa 128 na mambo mengine 13 sio ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, ninapoitizama Katiba ya Zanzibar katika kifungu cha 23(4) cha Katiba ya Zanzibar naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 23(4) cha Katiba ya Zanzibar kinasema hivi:-

Marginal note. Wajibu wa kutii sheria za nchi za nchi, kulinda mali ya umma na ulinzi wa taifa.

(4) “Kila Mzanzibari ana wajibu wa kulinda, kuhifadhi, kudumisha uhuru, mamlaka, ardhi na umoja wa Zanzibar”.

Sehemu ya mamlaka ndio ninayoitaka.

Vile vile tukiangali kifungu cha 43(5) cha Katiba ya Zanzibar Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu.

Kifungu cha 43(5) cha Katiba ya Zanzibar kinasema hivi:-

“Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Mamlaka ya Rais ndio itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya Sera za Serikali kwa ujumla na Mawaziri chini ya Uongozi wa Makamu wa Pili wa Rais watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar”.

Sasa hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba kwa haya maeneo kumi na tatu kati ya kumi na saba inayowajibika na ni maeneo ya mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambapo sote kama Wazanzibari tunapaswa kuyalinda kwa mujibu wa kifungu cha 23(4) cha Katiba ya Zanzibar.

Vile vile serikali kwa ujumla wake chini ya Makamu wa Pili wa Rais kama ilivyotajwa inawajibika katika Baraza hili kuhusu masuala haya. Ndio maana nikasema kwamba tunahitaji kuchukua maamuzi ya msingi kabisa kupitia katika Baraza hili.

Maamuzi hayo ni kuitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itupe kauli hapa, kwamba itachukua hatua angalau za kuwasilisha maombi katika *Secretariat* ya Jumuia ya Afrika ya Mashariki, kusema kuwa Zanzibar inataka suala hili liamuliwe na Zanzibar kupewa uwanachama ikiwa wa *Associate Membership* au ni *full membership*, kadri maelezo tutakavyopewa kwa yale mambo ambayo si ya Muungano, ni mamlaka ya Zanzibar kama ilivyo kwenye *Article of Union* tunayo *exclusive jurisdiction* na pia kama ambavyo imo kwenye Katiba ya Muungano kifungu cha 102 Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu.

> Kifungu cha 102 (1) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano kinasema hivi:-
>
> > "Kutakuwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakayojulikana kama "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar" ambayo itakuwa na mamlaka katika Zanzibar juu ya mambo yote yasiyo mambo ya Muungano kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii".

Mhe. Mwenyekiti, ninachokiomba ni kauli ya serikali kuhusu suala hili kwamba pamoja na maelezo ya jumla ambayo aliyoniba Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na haya aliwahi kunipa hata Bungeni mwaka jana wakati nilipouliza kuhusiana na suala hili.

Kwa hivyo, nadhani sasa wakati umefika Baraza hili lipewe nafasi yake Mhe. Mwenyekiti, atuambie lini serikali itachukua hatua ya kuwasilisha katika *Secretariat* ya Jumuia ya Afrika ya Mashariki, ombi la Zanzibar kujiunga ikiwa ni *Associate Membership* au *full membership*.

Vile vile ikiwa mkataba wa Jumuia unazuia basi pia kuna haja ya kupeleka maombi kulingana na hali halisi, yaani *special situation* ambayo ipo Tanzania kwa upande wa Zanzibar kwa mambo yasiyokuwa ya Muungano. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba sisi Zanzibar tuumeungana na Tanganyika na tutaunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jambo lolote linaekewa taratibu zake na taratibu kuu ni Katiba yetu. Katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano nyongeza ya kwanza ibara ya 4(2) inaeleza kuwa mambo ya nchi za nje ni mambo ya Muungano.

Kwa hivyo, ndio maana na wala sio Afrika ya Mashariki tu, lakini tukienda *SADC* tunakwenda kwa sura hii, pia tukienda *UN* tunakwenda kwa sura hiyo hiyo. Mhe. Mwenyekiti, kwa wakati huu hata yale mambo yasiyo ya Muungano tunawakilishwa kwa sura hiyo, kwa sababu kuna matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, halafu kuna matakwa ya mkataba.

Kwa maana hiyo, kwa sasa hatuwezi kufanya hayo maombi anayoyazungumza Mhe. Mjumbe. Mhe. Mwenyekiti, ndio maana tukasema ushauri mzuri tumeupata, kwa hiyo njia sahihi na safi ni muongozo unaotokana na wananchi wetu. Sasa kwenye utaratibu wa Katiba ambao tunakwenda kuufanya huo mchakato wa Katiba, basi maoni haya kama Zanzibar tumeshaamua tujitoe kwa utaratibu huu.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo maoni haya hata kabla ya kusainiwa mkataba huo wa kuanzishwa Jumuia ya Afrika ya Mashariki, wananchi wetu walitoa maoni yao na wakatuelekeza namna ya kwenda. Sasa kama tunayo maamuzi mengine, basi njia pekee na sahihi ni kurudi kwa wananchi, kwamba tukiweza kubadilisha Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano ikatupa mwangaza, kwa sababu leo ukienda hata huko kwenye mkataba Katiba yako mwenyewe ndio imekufunga.

Kwa kweli najua Mhe. Mjumbe anacho kitabu kinachomuelezea kwa kina, kwa sababu yako maelezo haya ambacho alikisoma. Mhe. Mwenyekiti, sasa tukimaliza kwenye Katiba yetu, basi lazima twende kwenye *special treatment* na kuomba huo utaratibu wa nchi yetu kuingia peke yake.

Mhe. Mwenyekiti, ninachomuomba Mhe. Mjumbe ni kwamba tukubaliane kwa sasa kwanza twende tukawasikilize wananchi wetu wanakubaliana na hili, kwa sababu ni jambo kubwa tena ni zito ambalo linahusu maslahi ya nchi yetu pamoja na mtikisiko wa taifa letu na lazima tufahamu. Kwa hivyo, ushauri wa mtu mmoja unaweza kutuletea matatizo katika utekelezaji wake.

Hivyo, ninachokiomba ni kuwa tuyafikirie kwa kina mambo haya na tuwe na subira. Mhe. Mwenyekiti, nafikiri jambo zuri katika hali hiyo tuliyonayo Mhe. Mjumbe ni vizuri akatuandikia *proposal* yake kama serikali, basi tukalitafakari

ndani ya serikali na kulijua vizuri suala hili na baadaye tukaweza kuliangalia kwa upana wake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa njia ni mbili. Kwanza tupeleke kwenye maoni ya wananchi. Pili kuitaarifu serikali kwa kuiandikia na kueleza kwa kina hasa ule muono wake anaouona katika suala hili na kuonesha athari tulizonazo kwa sasa na faida ambazo tutazipata kwa baadaye.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba nieleweke isiwe kama nafanya haya kwa ukaidi au kutokutaka kumsikiliza Mhe. Waziri na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais namheshimu sana. Lakini hapa tunazungumzia maslahi ya Zanzibar na watu wake ambayo ndiyo yaliyotuleta kwenye Baraza hili Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hoja kubwa ya Mhe. Waziri ni kwamba hata kwenye maelezo yake ya jumla alisema kuwa suala hili lilifikishwa kwa wananchi na wananchi walishauriwa. Lakini tunajua wenyewe utaratibu ambao tuliokuwa tukishirikisha wananchi. Kwa kweli suala kubwa ambalo liliwashirikisha wananchi kwa njia ya moja kwa moja lilikuwa ni suala la muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na ndio maana hakuna mwenye kubisha, kwa sababu lilipigiwa Kura ya Maoni na wananchi wakaliridhia.

Mhe. Mwenyekiti, tusidogoshe nafasi ya Baraza hili na kama sisi hatuliheshimu Baraza hili na wala hatutambui nafasi yake kwa Zanzibar pamoja na kusimamia mambo ambayo si ya Muungano kwa upande wa Zanzibar, basi hakuna mtu mwengine ambaye atakiheshimu chombo kama hiki. Kwa mfano, hata kwenye suala la mafuta Mhe. Mwenyekiti, tunaonekana tunapiga kelele tu, yaani tumeamua na wala halitekelezwi. *(Makofi)*

Kwa nini nasema hivyo Mhe. Mwenyekiti, Katiba hii ya Zanzibar kifungu cha 21(1) naomba kunukuu.

Kifungu cha 21(1) cha Katiba ya Zanzibar kinasema hivi:-

> “Kila Mzanzibari anayo haki ya kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, ama moja kwa moja au kwa kupitia Wawakilishi waliochaguliwa kwa hiari”.

Wawakilishi tuliochaguliwa kwa hiari ndio sisi Mhe Mwenyekiti, tunasimamia maslahi yao Wazanzibari. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nafahamu *reference* yake Mhe. Waziri anasema kwenye orodha ya mambo ya muungano iliyomo kwenye nyongeza ya kwanza kifungu cha 2 kinazungumzia mambo ya nchi za nje, nafahamu Mhe. Mwenyekiti. Vile vile nataka nimhakikishie kwamba na mimi pia nimejifunza sheria.

Lakini hoja yangu ni kwamba katika haya mambo ya Afrika ya Mashariki yapo mambo ambayo serikali ya Muungano hata kama viwanja vyao ni suala la muungano lakini haina mamlaka nayo haya, kwanza msingi mkuu wa mahusiano yetu Zanzibar na Tanganyika ni mkataba wa Muungano, huu umesema kwa mambo yasiyokuwa ya Muungano Zanzibar serikali yake itakuwa inayo *thuluth jurisdiction* na wamo wanasheria humu watusaidie katokana hili.

Katiba ya Muungano kifungu 102 kinasema Zanzibar kwa mambo yasiyokuwa ya Muungano serikali yake inakuwa na mamlaka kamili, katiba ya Zanzibar katika Mamlaka ya Baraza la Wawakilishi kifungu 78 kinasema nguvu za kutunga sherika kwa mambo yote yasiyokuwa ya Muungano katika Zanzibar yatakuwa mikononi mwa Baraza la Wawakilishi, haya mambo 13 Mhe. Mwenyekiti katika yake 17 sisi ndio wenye mamlaka kamili, kwa hivyo ninachosema nakubali anavyosema yeye kwamba Mkataba wa Afrika ya Mashariki huu hivi sasa pengine hautoi nafasi ya *membership*.

Nasema nilichoomba na nadhani akikubaliana na hicho ningeridhika na hata sasa hivi akinipa kauli hiyo nitaridhika nitakaa kitako na nitaunga mkono hoja hii. Serikali ya Mapinduzi ichukua hatua ya angalau kufanya mawasiliano ya *secteriet* ya Afrika ya Mashariki kuona kwamba suala hili kuhusu Wazanzibari upo uwezekano kiasi gani kukubaliwa, na nasema niliwahi kuzungumzia na Wajumbe wa Afrika ya Mashariki wamesema wako tayari kulisiliza hili,

Mwisho nimalizie kwa kusema kwamba tusipeleke masuala haya kwa hopa kwamba tusubiri mchakato wa katiba, mchakato wa katiba utakuja lakini mchakato wa katiba hauzuii hivi sasa mamlaka ya Serikali ya Zanzibar ambayo yanatolewa hivi sasa kwa mambo yasiyo kuwa ya muungano, namuomba Mhe. Waziri anikubalie hilo tu mimi. Kwamba yatafanywa mawasiliano na Kamati ya Afrika ya Mashariki kuona uwezekano huu halafu hayo mengine yatakuja katika vikao vinavyofuata. Mhe. Mwenyekiti ahsante sana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nadhani Mhe. Ismail Jussa Ladhu atakubaliana na mimi kwamba sote Mhe. Waziri wa Nchi hapa Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais yeye nwenyewe na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa maana ya Baraza la Mapinduzi ni waumini wa maslahi ya Zanzibar kama ambavyo yeye mwenyewe ni muumini. Lakini hoja yake iko katika msingi wa kikatiba na iko

katika msingi wa kisheria. Sasa maslahi tuliyonayo au hamu yetu ya maslahi nadhani msingi mkubwa ni kufuata sheria ni kufuata taratibu ziliopo, hoja yake ni kuitaka serikali iwasiliane na *secretariet* ya Jumuia ya Afrika ya Mashariki kutaka uanachama, hiyo ndio hoja yake ya msingi, Mheshimiwa uanachama wa jumuia yoyote ile hata *NGOs* inategemea masharti ya jumuia yenyewe. Sasa masharti ya Jumuia ya Afrika ya Mashariki yamo katika mkataba wa Jumuia ya Afrika ya Mashariki.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu najua anajua vizuri kuusoma mkataba huu, masharti yake ibara ya kwanza ibara ya pili, ibara ya tatu na nne ya mkataba huu yapo wazi kwamba wanaoweza kuwa wanachama ni *member state* na imetajwa *member state* wenyewe kwamba ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jamhuri ya Kenya, Jamhuri ya Uganda, na nchi nyengine ambazo zitajiunga.

Naamini Mhe. Ismail Jussa Ladhu anajua kanuni za tafsiri kwamba waliotajwa humu ni Jamhuri hata zile nchi zilizotajwa na nyengine ambazo zitajiunga kwa vile zilizotangulia mwanzo ni Jamhuri na nchi itakayojiunga inatakiwa iwe Jamhuri nadhani hapingi katika hilo, kwamba Zanzibar ni nchi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini sio jamhuri. Tumekubaliana kuungana na kwamba tunawakilishwa na Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti hili sio geni masuala ya kazi sio masuala ya Muungano Mhe. Mwenyekiti, lakini tunapokwenda kisheria Zanzibar si Mwanachama kwa kushirikiana na serikali ya Jamhuri ya Muungano kwamba uwakilishi huu una matatizo sio katika mkataba wenyewe, matatizo yale ni ndani ya katiba yetu. Msingi ni matatizo yetu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano haikuweka misingi hiyo na kwa sababu haikuweka misingi hiyo haikuweza kuweka misingi miziru wakati mkataba ulipoanzishwa kuwezesha Zanzibar kuweza kuwa mwanachama.

Kwa sababu hiyo Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Ismail Jussa Ladhu atuamini kwamba sisi ni waumini wenzake lakini tusifikishe pahala serikali yetu tukaitaka itoe tamko badala ya kuondoa tatizo tukaongeza tatizo naomba Mwanasheria msomi mwenzangu akubali katika hilo kwamba tusitoe tamko ambalo litaleta tatizo. Lakini zipo njia la kulishughulikia hili na zinachukuliwa na huo mchakato wa katiba mimi nadhani ndio utakaosaidia kuondoa tatizo hili moja kwa moja. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo ya Mwanasheria Mkuu nadhani ujumbe wangu na wananchi wa Zanzibar kwa jumla ambao na mimi nawasemea katika hili umefika, na nategermea tutapata

jibu la suala hili katika vikao vya mbele na naondoa hoja hii naomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Tunakushukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu, tunakushukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu na Waziri katika Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Kiafungu	401	Idara ya Mipango sera na utafiti	140,162,000
Kifungu	501	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	336,993,000
Kifungu	601	Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa	838,210,000
Kifungu	701	Idara ya Huduma za Makamo wa Pili wa Rais	285,404,000
Kifungu	801	Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga chama Mkuu wa serikali	361,753,000
Kifungu	1901	Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kwa mara nyengine tana, wakati nikichangia hoja hii ya Makadirio ya mapato na Matumizi ya Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais nilizungumzia suala linalohusu uratibu wa SMZ kwa upande wa kushughulikia masuala ya kero za Muungano kwenye suala zima la GDS. Nikafanya majumuisho, kwanye majumuisho yaliyotolewa na Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambaye mwenyewe alikiri hapa kwamba kuna fungu linalopitia katika sekta ambalo Zanzibar inashindwa kufaidika nalo pamoja na kutengewa asilimia 4.5.

Mhe. Mwenyekiti, nilipendekeza basi kwa sababu mbili, moja inaonekana Tanganyika kwa kutumia jina la Tanzania inatumia mwemvuli huu kwa kuombea misaada kisekta kwa mambo ambayo sio ya Muungano na ikafaidika peke yake bila ya Zanzibar kufaidika, kwa sababu misaada hii imekuwa ikiratibiwa kupitia vikao vinavyoitwa CG, baina ya nchi washirika wa maendeleo na Jamhuri ya Muungano. Na nikasema kwa sababu katika baadhi ya mazungumzo ya baadhi yetu wanazungumzia uwezekano wa Serikali ya Zanzibar kama itaomba, nilipendekeza hapa kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ianzishe mpango huu.

Katika majumuisho yote ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais sikulisikia likitolewa maelezo yoyote hili, nilikuwa naomba kupatiwa maelezo juu ya hili, hasa kama nilivyosema Zanzibar inapoteza mambo mengi sana hapa hata katika yale mambo ambayo tayari yameidhinishwa. Lakini kunapotokea masharti ya nchi wahisani Tanzania ikaadhibiwa kwa mfano kama Norway iliwahi kuondoa misaada baada ya kutokea ufisadi kwenye msaada ule wa Maliasili na sisi tunaathirika pia.

Naomba kauli ya serikali itolewe kwamba je, italifanyia kazi pendekezo langu la kwamba Zanzibar ianzishe au iombe kupitia jumuia ya kimataifa kupitia UNDP na Mashirika mengine kuanzisha *Conservative Group Meeting* kwa Zanzibar kwa mambo yote yasiyokuwa ya Muungano. Mhe. Mwenyekiti naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, hili hatuna mjadala tunakubaliana vizuri mimi na Mhe. Ismail Jussa Ladhu, hatuna mjadala kabisa. Kwa taarifa tu Mhe. Mwenyekiti hatua zimeanza za serikali kwa msingi huo anaosema Mheshimiwa, kwa hivyo maana yake tunakubaliana na ushauri wake.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimeridhia tuendelee.

Kifungu 1901	Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ	202,080,000
Kifungu 0102	Idara ya Maafa	148,413,000
	JUMLA YA FUNGU	**2,116,000,000**

FUNGU 16 BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

Kifungu 201	Utawala Unguja	7,442,268,000
Kifungu 301	Afisi Kuu Pemba	1,687,657,000
	JUMLA YA FUNGU	**9,129,925,000**

TUME YA UCHAGUZI - ZANZIBAR

FUNGU 30 MATUMIZI MENGINEYO

Kifungu 201	Utawala Unguja	628,449,000
Kifungu 301	Afisi Kuu Pemba	132,251,000
	JUMLA YA FUNGU	**761,000,000**

AFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS

FUNGU 05 AFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS

Kifungu 401	Idara ya Mipango sera na Utafiti	715,000,000
	JUMLA YA FUNGU	**715,000,000**

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara ya Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makisio hayo. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji waliokubali hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue Mkono, wanaokataa. Walikubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Mhe. Spika: Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kazi nzuri hiyo mliyoimaliza hivi punde, nafikiri kwa mwenendo huu tulioanza na Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais tutafanya kazi vizuri, nataka niwahikikishie Waheshimiwa wajumbe kwamba Mjumbe anapohoji fungu haina maana kwamba yeye anapinga, isipokuwa anahitaji ufafanuzi ili kile tunachokipitisha kiwe na uhakika juu ya maelezo ambayo yamo ndani ya hotuba na kutokana na michango mizuri ambayo waheshimiwa wajumbe wameitoa. Hiyo ni haki ya Mjumbe wala tusimuone kwamba anakuwa mkorofi au mkaidi hapana ni haki isipokuwa ni utaratibu tunaitumia nafasi hiyo kwa utaratibu mzuri, nidhamu na kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Nashukuru sana Waheshimiwa wajumbe kwa mashirikiano makubwa.

Katibu: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizopangwa kutekelezwa kwa siku hii ya leo sasa zimekamilika.

Mhe. Spika: Katibu anatuarifu kwamba tumeimaliza na mimi nakushukuruni. Sasa kabla sijaahirisha kikao hiki kuna tangazo moja, nimeombwa na Mhe. Katibu wa Wawakilishi wanaotoka Chama cha Mapinduzi niwatangazie kwamba ule uchaguzi wa kumchagua katibu Wawakilishi hao pamoja na wajumbe wengine wa NEC utafanyika siku ya Jumapili tarehe 26/6/2011. Tunategemewa tuwe tumeshafika pale saa 3.00 lakini pia watatufanyia kazi yetu ya wawakilishi wa Chama cha Mapinduzi.

Waheshimiwa wajumbe baada ya hayo nakushukuruni kwa mashirikiano makubwa katika kufanya shughuli zetu. Ahsanteni.

(Saa 1.30 Usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe
27/6/2011 Saa 3.00 Asubuhi)